SIRI PART 3

JASUSI/GAIDI

SEASON 3

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

1.MISS TANZANIA
2.I WAS WRONG
3.TEN CHAPTERS
4.I DO
5.SERENA
6.BEFORE I DIE
7.BEYOND PAIN
8.PENIELA
9.QUEEN MONICA
10.THE FOOTBALL
11.I DIED TO SAVE PRESIDENT
12.KIAPO CHA JASUSI
13.KIKOSI CHA SIRI
14.SIRI

MAWASILIANO
0764294499

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Kwa muda wa miezi mitatu tumekuwa tukizunguka sehemu mbali mbali duniani tukifanya utalii.Katika safari yetu hiyo tulipiga picha nyingi sana lakini kitu cha ajabu ni kwamba nilipozitafuta picha tulizopiga mimi na Abu katika safari yetu sikupata hata picha moja.Nilihifadhi picha nyingi katika kompyuta yangu nyingine zilikuwepo katika kamera na hata katika simu

yangu lakini huko kote hakukuwa na picha hata moja.Hiki kitu kimenishangaza sana mama namna picha zilivyotoweka.Hakuna mtu yeyote aliyeingia chumbani kwetu zaidi yetu sisi hivyo naamini aliyefuta picha hizo lazima atakuwa Abu Zalawi.Nimejiuliza maswali mengi kwa nini akafuta picha zetu?Nimeshindwa kupata jibu ndiyo maana nataka unieleze kuhusiana na huyu mtu ni wa aina gani? Tafadhali mama”

akasema Najma na Habiba akavuta pumzi ndefu

“Mambo yamekwisha haribika.Tayari Najma amekwisha hisi kitu kuhusu Abu zalawi.Nadhani ni wakati wake wa kuufahamu ukweli” akawaza Habiba

“Najma kuna jambo ambalo nataka nikueleze kuhusu Abu Zalawi.Kwanza kabisa ni kwamba Abu Zalawi hatarejea tena.Ameondoka” akasema Habiba na sura ya Najma ikabadilika

“Unasemaje mama ?! akauliza Najma

“Najma Abu Zalawi hatarejea tena.Ameondoka”

“Mama sijakuelewa”

“Najma kuna mambo mengi ambayo huyafahamu kuhusu mimi” akasema Habiba na kumtazama Najma ambaye alionekana kuchanganyikiwa

“Maisha yangu yamejaa siri nyingi ambazo nyingine nitakueleza lakini nyingine nitakwenda nazo kaburini.Nina sababu yangu ya kufanya hivyo” akasema Habiba na kunyamaza tena akamtazama Najma

“Siri ya kwanza ni kuhusu huu utajiri wangu.Utajiri wangu huu ambao ninautumia katika kufadhili makundi mbali mbali ya kigaidi niliurithi kwa baba yake Abu Dahir lakini naye utajiri huu hakuupata hivi hivi.Leo nitakupa siri ya huu utajiri wangu” akasema Habiba na kunyamaza akamtazama Najma

“Asili ya utajiri wangu huu ni Marekani.Wao ndio waliomuwezesha baba yake Abu Dahir na alipofariki mimi ndiye niliyerithi utajiri

huo.Kwa nini Marekani walimpa utajiri huu mkubwa? Akauliza Habiba lakini Najma hakujibu kitu chochote

“Ndani ya shirika la ujasusi la Marekani CIA kuna kitengo ambacho kinajishughulisha na mashirikiano na makundi ya magaidi.Kitengo hiki ndicho kilichotuwezesha kuwa na utajiri huu mkubwa na lengo kuu la kutupa utajiri huu ni kwa ajili ya kuyafadhili makundi ya kigaidi katika operesheni zao mbali mbali zenye maslahi kwa Marekani

hivyo basi kwa muda huu wote nimekuwa nikifanya kazi na Marekani.Ufadhili huu ambao tumekuwa tukiwapa makundi ya magaidi ni maelekezo ya Marekani” Sura ya Najma ilibadilika alifungua mdomo wake akataka kusema kitu lakini maneno hayakutoka

“Nimekustua Najma.Lakini umefika wakati wa wewe kufahamu kila kitu.Nimeamua kukushirikisha siri chache kuhusu mimi” akasema Habiba

“Nimefanya kazi na Marekani kwa muda mrefu na

sasa nimechoka.Sitaki kuendelea tena kuwa mfadhili wa makundi ya kigaidi ndiyo maana nikamleta Abu Zalawi ili aweze kulimaliza jambo hili.Kuna mambo ambayo huyafahamu kuhusu Abu Zalawi na leo nitakufahamisha”Habiba akanyamaza kidogo halafu akasema

“Abu Zalawi jina lake halisi anaitwa Mathew Mulumbi ni mtanzania”

“Mungu wangu ! akasema Najma.Habiba akaendelea

“Abu Zalawi si gaidi kama nilivyokufahamisha awali bali ni jasusi”

“Jasusi ? ! Najma akashangaa

“Ndiyo ni jasusi.Najma kuna mengi ambayo ningetaka kukueleza lakini nitazungumza nawe siku nyingine hayo machache yanatosha kwa leo.Kubwa ambalo nataka ulifahamu ni kwamba Abu Zalawi au Mathew alikuwa hapa kwa ajili ya kazi maalum na sasa wakati wake umefika wa kwenda kutekeleza majukumu yake na kazi hiyo

anayokwenda kuifanya ni kwa ajili ya usalama wenu wewe na kaka yako.Abu ndie mkombozi wenu kwani akifanikiwa katika misheni hiyo itakuwa ni salama yenu lakini akishindwa maisha yetu yatakuwa shakani.Abu Zalawi hatarudi tena”

“Unamaanisha nini mama?

“Misheni anayokwenda kuifanya ni misheni ya hatari kubwa sana na uhakika wa kurudi salama katika misheni hiyo ni mdogo” akasema Habiba

“Mama kwa nini ukanifanyia hivi? Kwa nini ukanitaka niolewe na Abu Zalawi wakati ukijua ni mtu wa namna gani?Kwa nini ukaniacha nikazama mapenzini na Abu Zalawi halafu unamuondoa? Akauliza Najma

“Nilikuwa na sababu zangu kukutaka uolewe na Abu Zalawi.Bila kuolewa naye asingekubali kukaa nasi hapa kwa ajili ya misheni ambayo nimemtuma akaifanye.Amekaa nasi hapa hadi ulipofika muda

wake wa kuondoka kwa sababu yako”akasema Habiba

“Mama wewe ni shetani.Una roho ya kishetani ! Huna ubinadamu hata kidogo.Mama wewe ni mkatil……” Akasema Najma na Habiba akamnasa kofi

“Haya yote niliyoyafaya ni kwa sababu yenu.Nafanya kila hatua kuwalindeni ili muwe salama vinginevyo ninyi nyote hivi sasa mngekwishauawa.Kuanzia sasa anza kuzoea hali hii.Abu Zalawi ana mke wake na

watoto hawezi kurudi tena.Kumpoteza Abu si mwisho wa mais…”akasema Habiba na Najma akatoka mbio huku akilia.

“Nimemuumiza sana Najma.Sikutaka aufahamu ukweli hu lakini kwa hatua aliyokuwa ameifikia ni lazima aufahamu ukweli.Itamchukua muda mrefu kukubaliana na ukweli h….” Habiba akastuka baada ya mmoja wa walinzi wake kuingia mle ndani akikimbia

“Kuna nini ?akauliza Habiba kwa wasi wasi.

“Mama umesikika mlio wa risasi katika nyumba ya Abu Zalawi ! akasema Yule mlinzi na Habiba akatoka mbio akiongozana na Yule mlinzi na kukuta walinzi wengine tayari wamekwisha fika katika nyumba ile ya Mathew.Habiba akiwa na wale walinzi wakaenda chumbani kwa Najma walinzi wakavunja mlango akaingia ndani.Najma alikuwa amelala katika dimbwi la damu.Hakuwa na uhai tena.Alijipiga risasi ya kichwa.Habiba akaanguka na kupoteza fahamu.

ENDELEA.....

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Saa tisa za alasiri televisheni ya taifa ilikatisha kipindi kilichokuwa kinaendelea na kujiunga na matangazo ya moja kwa moja kutoka ikulu jijini Dar es salaam ambako Rais wa jamhuri ya muungamo wa Tanzania alitarajia kutoa hotuba kwa watanzania.Kama ilivyokuwa siku

iliyotangulia,simu janja zote ambazo zilikuwa zimewashwa muda huo ziliunganishwa na matangazo yale ya moja kwa moja kutoka ikulu kwa lengo la kumuwezesha kila mwananchi kusikiliza ujumbe ambao Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania alitaka kuwapa watanzania.Tayari wanahabari walikwisha weka sawa kamera zao na aliyekuwa akisubiriwa ni Rais

Mlango ulifunguliwa na Rais Dr Fabian Kelelo akajitokeza akiwa ameambatana na Mufti wa

Tanzania Sheikh Seleman Majid.Muongozaji wa shughuli ile alitoa maelezo machche na kumkaribisha Rais aweze kuzungumza na watanzania.Rais alianza kwa kuwatania kidogo waandhishi wa habari kisha akaendelea

“Ndugu watanzania wenzangu awali ya yote ninamrejeshea utukufu Mungu wetu aliye juu kwa kutukutanisha tena siku hii.Poleni sana wale wote ambao mmeendelea kuwapoteza wapendwa wenu kufuatia vurugu zinazoendelea

na wale wote ambao mnauguza majeraha nawatakiwa uponaji wa haraka.

Ndugu watanzania,jana nilizungumza nanyi kwa kirefu na kuwasisitiza umuhimu wa kutunza amani yetu.Ninashukuru sana kwa wengi kunielewa na taarifa niliyoipata ni kwamba vurugu zimepungua na hii ni dalili njema kwamba tunaelekea kuzuri.Bado naendelea kuwasihi ndugu watanzania tuachane na vurugu hizi ambazo hazina maslahi kwetu na hata kwa dini

zetu.Tunachokivuna katika machafuko haya ni hasara badala ya faida.Ndugu zetu wengi wamepoteza maisha,wengine hawajulikani walipo,wengine wamepata ulemavu wa kudumu na wengine wanaendelea kuuguza majeraha hospitali.Wengi wetu tumepoteza mali,nyumba zimechomwa moto,majengo ya serikali yamechomwa na kuharibiwa,miundo mbinu imeharibiwa,biashara zimefungwa nk.Ndugu zangu kwa ujumla tunachovuna katika machafuko haya ni

hasara kubwa na tuna kazi kubwa ya kuijenga nchi yetu baada ya machafuko haya kumalizika” Rais akanyamaza kidogo halafu akaendelea

“Jana baada ya kumaliza kutoa hotuba yangu,nilipigiwa simu na Mufti wa Tanzania akaniomba tuonane leo tuzungumze.Leo kuanzia asubuhi nilikuwa na kikao kirefu naye na kubwa tulilolijadili ni kuhusiana na vurugu hizi zinazoendelea nchini namna tutakavyoweza kuzmaliza.Imekuwa ni desturi yetu kukaa mezani kila pale

inapojitokeza mikwaruzano baina ya dini zetu na mara zote katika mazungumzo ya pamoja tumekuwa tukimaliza tofauti na amani ikamalaki.

Tumezungumza mambo mengi katika kikao hicho kirefu na tumekubaliana kuwa na kikao kikubwa kitakachowahusisha viongozi wakuu wa dini zote hapa nchini ili tutafute muafaka.Naahidi kikao hicho kitafanyika mapema sana ili tukae meza moja serikali na viongozi wa dini tujikwamue hapa tulipokwama na maisha

yarejee kama kawaida.Kwa kuwa mambo mengi nilizungumza jana leo naomba nimpe nafasi Mufti ana neno la kuzungumza na watanzania.” akasema Dr Fabian na kumkaribisha mufti wa Tanzania Sheikh Seleman Majid ambaye alianza kwa dua kisha akaendelea

“Ndugu zangu,awali ya yote nami nataka nianze kwa kuwapa pole nyingi wale wote ambao wamepoteza ndugu zao hadi sasa katika machafuko haya yanayoendelea hapa nchini kwetu na wale wote

waliopata majeraha mbali mbali nawaombea wapate nafuu ya haraka.

Ndugu zangu watanzania kwa siku kadhaa sasa nchi yetu imekumbwa na machafuko makubwa kabisa kuwahi kutokea hapa nchini.Machafuko haya yalianzia katika nchi ya jirani na yakaenea kama moto wa nyika hadi kufika hapa Tanzania.Ndugu zangu dunia inashangaa nini kimetokea Tanzania?Katika historia ya nchi yetu hakujawahi kutokea machafuko kama haya

yanayoendelea ya waumini wa dini kushambuliana.Mheshimiwa rais alieleza kwa kirefu jana namna ambavyo watanzania tumekuwa tukiishi kwa amani na upendo mkubwa licha ya tofauti zetu za kidini.Tumeishi kindugu tukishirikiana katika mambo mbali mbali sherehe,misiba n.k. Hatujawahi kubaguana hata siku moja kwa imani zetu.Nini kimetufikisha hapa? Swali hili ameliuliza Rais jana wakati anatoa hotuba yake na kwa swali hilo ndiyo lilinifanya

nitake kuonana na mheshimiwa Rais ili kwa pamoja tutafute majawabu ya nini kimetufikisha hapa.

Tumekuwa na kikao kirefu na tumezungumza kwa upana kuhusu jambo hili.Tumekubaliana kwamba tuwe na kikao kikubwa cha viongozi wakuu wote wa dini ili kwa pamoja tuweze kuzungumza na kutafuta muafaka lakini wakati kikao hicho kikiandaliwa tumekubaliana kwamba sisi viongozi wa dini tuwahamasishe waumini wetu

watulie na waache vurugu.Suala hili ni pana zaidi ya tunavyodhani hivyo basi tunataka kuipa serikali nafasi iweze kulishughulikia hili jambo na kupata chanzo chake.Tunapoendelea kushambuliana na kuuana tunaifanya serikali ishindwe kulishughulikia suala hili hivyo Rais ametuomba kila kiongozi wa dini ajitahidi kuhakikisha anawahamasisha waumini wake watulie waache vurugu ili serikali ishughulikie kutafuta chanzo cha jambo hili.

Ndugu zangu kufuatia maelekezo hayo ya Rais,niko hapa kuzungumza na ndugu zangu wa upande wa waislamu kuwasihi wasiendelee kushiriki katika vurugu.Uislamu ni dini ya amani na hata tunaposalimiana tunasema Assalam alaikum maana yake amani iwe nawe. Dini ya Uislamu ina mitazamo inayofanana na dini nyingine kuhusu suala hili la amani na usalama.Katika mtazamo wa Uislamu usalama una maana ya amani na utulivu katika jamii. Neno amani kwa ujumla limezungumziwa katika karibu aya 140 za Qur'ani ambacho ni

kitabu kitakatifu cha Mwenyezi Mungu.Usalama na amani vina mfungamano na Mwenyezi Mungu Muumba. Mwenyezi Muumba mwenyewe amejitaja kuwa ni "Assalam" kwa maana ya amani na Mwenye amani na salama na kwa msingi huo kila usalama na amani ni mwangwi wa dhati yake tukufu. Dhati ya mwanadamu pia daima huwa katika hali ya kustawi na kufanya harakati za kuelekea kwenye amani na utulivu kamili ambao haupatikani ila kwa amani na usalama , yaani dhati ya Mwenyezi Mungu

Muumba.Aya ya 208 ya Suratul Baqara inasema:

Enyi Mlioamini! Ingieni katika usalama nyote. Wala msifuate nyayo za She'tani; hakika yeye kwenu ni adui aliyewazi.

Vilevile aya ya 61 ya Suratul Anfal inasema:

Na (wapinzani wako) wakielekea kwenye amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.

Neno "Islam" pia linatokana na msingi wa neno

"Silm", na kwa hakika lina maana ya kumfuata Mwenyezi Mungu ambaye Yeye mwenyewe ndiye amani na usalama mutlaki na utulivu kamili.

Neno jingine ni "sulh" ambalo lina maana na amani, maelewano na uhusiano mwema baina ya wanadamu. Uislamu umetumia neno hilo ukitaka kuwepo upendo, kuheshimiana, kujiepusha na uchokozi na uhasama na kuchupa mipaka ya wanadamu wengine.

Ili kuweza kupatikana amani na uadilifu, Uislamu umeweka safari yenye awamu

tatu tofauti. Kwanza ni usalama na amani ya ndani ya nafsi. Katika awamu hii watu wote wa jamii wanatakiwa kutakasa nafsi zao na kuzipamba kwa taqwa na uchamungu.Katika awamu hii, muumini anapaswa kukomesha mpambano na vita liyopo baina ya matamanio na matakwa yake ya kinafsi na yale ya kiroho, na kufikia amani na usalama wa ndani ya nafsi ili pande hizo mbili za kinafsi na kiroho ziishi pamoja kwa amani na kumsaidia mwanadamu kufikia kilele cha ukamilifu. Ni baada ya hapa ndipo mwanadamu

anapokuwa tayari kwa ajili ya harakati ya kijamii na wanadamu wenzake kuelekea kwenye malengo aali na ya juu zaidi. Aya ya 103 ya Suratu Aal Imran inasema:

“Na shikamaneni na Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote kwa pamoja, wala msifarikiane”

Kwa msingi huo amani ya ndani ya nafsi ndiyo msingi wa ukamilifu wa kimaadili na kiroho kwa ajili ya kuwa na taathira kubwa zaidi katika jamii ya Kiislamu.

Awamu ya pili ya amani na usalama katika Uislamu ni amani na usalama wa jamii. Baada ya kuwa tayari kinafsi kwa kuitakasa na kuisafisha, mwanadamu huwa ametengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya muungano mpana zaidi wa kijamii na wanadamu wenzake. Hapa ndipo inapokuja amri ya Mwenyezi Mungu inayowataka Waislamu kuwa na umoja na kujenga udugu. Sehemu moja ya aya ya kwanza ya Suratul Anfal inasema:

“Basi mcheni Mwenyezi Mungu na msuluhishe mambo baina yenu, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni waumini.”

Kwa utaratibu huo Waislamu hutoka katika minyororo ya ubinafsi, ubaguzi, dhulma na sifa nyingine mbaya na kuwa watu wema na wenye faida kwa jamii.

Awamu ya tatu ya amani na usalama inahusiana na usalama na amani kwa wasio Waislamu. Miongoni mwa misingi na kanuni

zinazotawala jamii ya Kiislamu ni kuishi kwa amani na usalama na wasio Waislamu. Kinyume na fikra na dhana za wanafikra wengi wasio Waislamu na propaganda chafu za nchi za Magharibi, Uislamu ni dini ya amani na kuishi kwa usalama na wasio Waislamu. Hii ni pamoja na kwamba, huwezi kupata hata aya moja ya Qur'ani inayowalazimisha watu kukubali dini hiyo kwa vita na mabavu. Vita katika Uislamu vina sura ya kujihami na kujilinda mbele ya mashambulizi yanayolenga jamii ya Waislamu au watu

wengine wanaodhulumiwa au kwa ajili ya kuzuia uchokozi na hujuma za adui.

Suala la kuishi kwa amani na usalama na wasio Waislamu limesisitizwa sana katika aya za Qur'ani tukufu na hadithi, sira na mwenendo wa Mtume na Aali zake watoharifu. Suala hili pia limejengeka juu ya nguzo ya utukufu wa kiumbe mwanadamu. Katika mtazamo wa Uislamu wanadamu wasio Waislamu wana heshima na utukufu wa kidhati na kimaumbile kutokana na kushirikiana kwao na Waislamu katika maumbile na

ubinadamu japo wanatofautiana katika dini na imani. Uhakika huu unathibitishwa na sira, mwenendo na maisha ya Mtume Muhammad (saw).

Mfano wa wazi wa mwenendo huo wa amani na suluhu na wasio Waislamu ni Mapatano ya Ungwana yaliyofikiwa baina ya Mtume (saw) na washirikina wa Makka kabla ya kutangazwa dini ya Uislamu, Mapatano ya Hudaibiyya, mwenendo wa Mtume Muhammad (saw) na jinsi alivyokuwa akiamiliana na tawala na wafalme wa maeneo mbalimbali kama Iran

na Roma na kutumia njia ya kutuma barua kwa watawala na wafalme wa zama hizo baada ya kuunda dola la Kiislamu mjini Madina. Kwa mfano tu Mtume (saw) alisema katika amri aliyompa Amru bin Hazm wakati alipomtuma Yemen kwamba: *Kila Myahudi au Mkristo atakayekubali Uislamu na kudhihirisha Uislamu halisi atakuwa mmoja kati ya waumini, atakuwa na haki sawa na za Waislamu na kushirikiana nao katika vipindi vyote vya shida na raha. Na kila mtu atakayeamua kubakia katika dini yake ya Uyahudi*

au Unaswara kamwe hatalazimishwa kuacha dini yake, kwa sababu ujumbe wa dini na risala za Mitume wote wa Mwenyezi Mungu ni kuleta amani, uadilifu, kueneza masuala ya kiroho,kumkamilisha mwanadamu na kumfikisah kwenye saada na ufanisi", mwisho wa kunukuu.

Kwa msingi huo, katika mtazamo wa Uislamu suala la usalama na kuishi kwa amani na wanadamu wengine wenye itikadi na imani tofauti, ni jambo lenye thamani na umuhimu mkubwa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba,

ni katika mazingira ya amani na usalama ndipo wanadamu wanapoweza kuelekea kwenye ukamilifu wa kimaada na kiroho, bali hata kuweza kumjua na kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Hivyo suala la kujenga na kuimarisha amani na usalama na vilevile juhudi za kulingania amani na usalama wa kimataifa na kuishi pamoja kwa amani wanadamu wote kwa msingi wa Tauhidi na kumpwekesha Mwenyezi Mungu, uadilifu na usafi wa nafsi bila ya kujali dini, rangi, na tofauti zao nyingine ndio lengo la mwisho la Uislamu na

wafuasi halisi wa dini hiyo. Ni wazi kuwa, kufuata mafundisho ya dini hiyo kunaweza kuwa suluhisho la kumwondoa mwanadamu katika kinamasi cha vita, mapigano na migogoro ya dunia ya sasa.

Ndugu zangu waislamu nimejaribu kutoa ufafanuzi mrefu kidogo kuhusu uislamu na amani.Dini zote hapa duniani zinahubiri amani.Hata akija kiongozi wa dini ya kikristu ataeleza namna biblia takatifu inavyosisitiza amani.Ninawataka ndugu waislamu na wasio waislamu

mnaonisikiliza hivi sasa kokote mliko wekeni silaha zenu chini na turejee kuishi kwa amanai kama ilivyokuwa hapo kabla.Tuiachie serikali ilifanyie uchunguzi jambo hili tujue nani katufikisha hapa? Nani waliotufarakanisha hadi ndugu tukaanza kuuana? Nawasihi tuweke mbele maslahi ya nchi yetu.Tuna nchi moja tu na tazameni kilichotupata baada ya kuvuruga amani.Tumekosa hata sehemu ya kukimbilia kwani sisi kwa miaka mingi tumekuwa ni kimbilio la wale

wote ambao amani imepotea katika nchi zao.

Mufti alimaliza hotuba yake kwa kuendelea kuwasisitiza waumini wa dini ya kiislamu na wa dini nyingine kuachana na vurugu ili amani irejee.Baada ya kumaliza kutoa hotuba Mufti na Dr Fabian wakaenda kupata chakula cha mchana pamoja.

WASHINGTON DC – MAREKANI

Saa tano za asubuhi, Mark Piller makamu wa Rais wa Marekani aliwasili katika nyumba kubwa aliyokuwa akiishi jenerali Akiki Rwamirama.Lilikuwa ni jumba kubwa la kifahari lililokuwa na viwanja vya michezo mbali mbali kama vile mpira wa kikapu,mpira wa wavu na tenisi.Kulikuwa na miti mingi kulizunguka jumba hilo na kulifanya kuwa na utulivu

mkubwa,ni sauti za ndege mbali mbali ndizo zilisikika.

Jenerali Akiki hakuwa na taarifa kama Mark Piller angekwenda kumtembelea.Alikuwa ndani ya sebule kubwa akitazama runinga akifuatilia taarifa za habari za vyombo mbali mbali vya habari duniani na kubwa alilokuwa analifuatilia ni taarifa za kuhusiana na kile kilichokuwa kinaendelea Afrika mashariki hususan nchini Uganda.

Mlango mkubwa wa sebuleni ukagongwa na mmoja

wa walinzi wake akaenda kuufungua akakutana na walinzi wa makamu wa Rais.Nje tayari msafara wa makamu wa Rais ulikwisha wasili na alikwisha shuka akipiga hatua kuelekea ndani.Jenerali Akiki alipojulishwa kuwa ni makamu wa Rais amefika akainuka haraka na kwenda kumpokea

“Mheshimiwa Rais habari yako” akasema Mark Piller

“Mark niite Akiki inatosha.Hayo mambo ya Rais yamekwisha pita.Mimi si Rais

tena wa Uganda” akasema Jenerali Akiki

“Jenerali Akiki sisi tunaendelea kukutambua kama Rais halali wa Uganda hivyo tutaendelea kukupa heshima yako ya Rais” akasema Mark

“Nashukuru sana Mark.Karibu”

“Ahsante jenerali Akiki.Tunaweza kutembea tafadhali” akasema Mark na Jenerali Akiki akamuongoza wakaelekea katika uwanja wa gofu.

“Jenerali Akiki vipi maisha yako yanakwendaje hapa?Unayafurahia?akauliza Mark Piller

“Maisha yanakwenda vizuri sana mheshimiwa makamu wa Rais. Ninayafurahia maisha.Tayari akili yangu imekwisha anza kuzoea maisha haya.Kwa ujumla hakuna tatizo lolote.Ninashukuru sana kwa namna mnavyonihudumia.Ninapata kila ninachokihitaji”akasema Jenerali Akiki

“Ninafurahi kusikia hivyo mheshimiwa Rais.Ninakuahidi utaishi maisha mazuri kama uko peponi.Utapata kila unachokihitaji na utayasahau maisha yako yaliyopita” akasema Mark Piller

“Ahsante Mark.Sikutegemea kama baada ya kuondolewa madarakani ningekuwa na maisha mazuri kama haya.Washenzi wale wametaifisha mali zangu zote na bila ninyi ningekuwa masikini wa kutupwa” akasema Jenerali Akiki

“Niliwahi kukwambia Jenerali Akiki kwamba yanapofanyika mapinduzi rais aliyepinduliwa mara nyingi lengo huwa ni kumuua lakini kama akinusurika akakimbia basi mali zake zote ndani na nje ya nchi hutaifishwa na serikali iliyochukua madaraka.Lakini hilo lisikuumize kichwa kwa sasa wewe ni tajiri na utakuwa na mali mara mbili zaidi ya zile ulizokuwa nazo ulipokuwa madarakani.Hata kama ukitaka familia basi unao uwezo wa kuanzisha familia

tena kubwa.Kila kitu kinawezekana mheshimiwa Akiki”akasema Mark Piller

“Mambo yanaendeleaje Afrika Mashariki ?akauliza Jenerali Akiki

“Mambo yanakwenda vizuri mheshimiwa Akiki.Meli zetu kubwa za mafuta zimepanga foleni katika bandari ya Tanga zikipakia mafuta.Kwa ujumla kila kitu kinakwenda vyema”

“Safi sana.Nataka ikiwezekana mchukue mafuta yote yaliyopo Uganda muyalete huku kwa watu

ambao wana shukrani na utu.Nimeijenga Uganda lakini shukrani zake ni hizi.Mark kama upo uwezekano wa kuongeza zaidi uchukuaji wa mafuta fanyeni hivyo tafadhali”akasema Jenerali Akiki

“Jenerali Akiki hilo ndilo lililonileta hapa kwako.Jana nilikuwa na mazungumzo marefu na Rais kuhusiana na mpango huu unaoendelea.Katika mazungumzo yetu tumekubaliana kwamba tutanue zaidi operesheni

hii.Unajua Afrika Mashariki ni tajiri sana.Tunataka tusiishie kwenye mafuta peke tunataka twende mbali zaidi tuingie hadi katika rasilimali nyingine kama vile madini.Nchi kama Tanzania imebarikiwa madini ya kila aina.Nchi kama jamhuri ya kidemokrasia ya Congo nayo vile vile ina madini ya thamani.Tanzania kwa mfano ina madini ya dhahabu,almasi,na mengine mengi bila kusahau madini ya Tanzanite ambayo hayapatikani sehemu nyingine yoyote duniani zaidi ya

Tanzania pekee.Tunataka operesheni yetu sambamba na mafuta iende pia katika maeneo hayo niliyoyataja.Nimekuja hapa kwako kupata ushauri unadhani nini tufanye kutanua operesheni hii Afrika mashariki? Akauliza Mark Piller

“Mheshimiwa makamu wa Rais tena imekuwa vizuri umefika.Muda mfupi kabla hujafika hapa nilikuwa natazama kile kinachoendelea Afrika mashariki.Leo kuna

jambo limetokea nchini Tanzania”

“Kumetokea nini Tanzania ?akauliza Mark Piller

“Rais wa Tanzania amekutana na Sheikh mkuu wa Tanzania na wamekuwa na kikao kirefu wakizungumzia vurugu zinazoendelea.Kikao hicho kinaonekana kuwa na mwelekeo mzuri wa kumaliza vurugu hizo zinazoendelea.Nimezisikiliza hotuba aliyoitoa Mufti na kwa kiasi kikubwa inaweza kuwashawishi waumini kuachana na vurugu

zinazoendelea.Kwa kawaida waumini wa dini ni watiifu mno kwa viongozi wao hivyo kama wameambiwa na kiongozi wao waache vurugu basi watafanya hivyo.Watanzania ni wepesi sana wa kumaliza mambo kwa amani na kwa mujibu wa taarifa ambayo imetolewa leo,tayari vurugu zimeanza kupungua nchini Tanzania na hii inatokana na hotuba ya jana ya Rais Dr Fabian" akanyamaza akamtazama Mark Piller

“Mpango huu uliojadiliana na Rais wako ni mpango mzuri sana na wenye manufaa kwa Marekani lakini ili mpango huo ufanikiwe tunaihitaji mno Tanzania.Vurugu lazima ziendelee nchini Tanzania ili majeshi ya Marekani yaendelee kukaa nchini humo na kama ikiwezekana basi wanajeshi waongezezwe zaidi.Tanzania haitakiwi ipate amani kwani ikiwa shwari hakutakuwa na ulazima wa vikosi vya Marekani kuendelea kuwepo na hivyo hatutaweza tena kuendelea na uchukuaji

wa mafuta na rasilimali nyingine” akasema Jenerali Akiki

“Nini unashauri kifanyike Jenerali Akiki? Tunategemea sana ushauri wako kwa kuwa wewe unalifahamu vyema eneo la Afrika mashariki.Ushauri wowote utakaoutoa tutauzingatia” akasema Mark Piller

“Kunatakiwa kufanyike kitu cha haraka sana kuhakikisha hali inaendelea kuwa tete nchini Tanzania ili vikosi vya Marekani viendelee kukaa huko kwa muda mrefu

zaidi na kama ikiwezekana viongezwe vikosi vingine” akasema Jenerali Akiki

“Nini basi unashauri kifanyike kwa haraka?Mimi na mheshimiwa Rais tulifikiria kuanzisha kikundi cha waasi ambacho tutakiwezesha kwa silaha na zana nyingine za kijeshi ambacho kitaendesha mapigano na serikali za Afrika mashariki ili tupate nafasi ya kuongeza wanajeshi zaidi katika eneo la Afrika Mashariki.Unaonaje kuhusu mpango huo?akauliza Mark Piller

“Huo ni mpango mzuri lakini si muafaka kwa sasa.Kuanzisha kikundi cha waasi ni mpango wa muda mrefu.Si jambo jepesi kuanzisha uasi hasa katika nchi kama Tanzania.Kwa nchi ya jamhuri ya kidemo krasia ya Congo kule hakuna shida kwani wamekwisha zoea mambo kama hayo lakini kwa sasa tunalenga zaidi Tanzania hivyo wazo la kuanzisha kikundi hicho cha uasi tuliweke pembeni tutalishughulikia

taratibu”akasema Jenerali Akiki

“Vipi kuhusu kuwatumia IS kufanya mashambulio mbali mbali ya kigaidi na kuua watu?akauliza Mark Piller

“Hilo nalo ni wazo zuri lakini bado si mpango mzuri tunaouhitaji kwa sasa.Tunatakiwa kufanya kitu cha haraka”

“Nini basi unashauri kifanyike kwa haraka jenerali Akiki?akauliza Mark Piller na Jenerali akiki akainamisha kichwa akafikiri kisha akasema

“Hapa Marekani mnao wanasayansi wa hali ya juu.Nataka muwatumie wataalamu hao kutengeneza kirusi ambacho kitakuwa ni hatari na ambacho kinaweza kusababisha maangamizi makubwa kitakachokwenda kusambazwa nchini Tanzania”

“Kirusi? Akauliza Mark Piller

“Ndiyo Mark.Mnatakiwa kutengeneza kirusi ambacho kinaweza kuwa hatari zaidi na kwenda kukisambaza nchini Tanzania ambacho kitasambaa kwa haraka zaidi na

kusababisha vifo vya watu wengi.Baada ya hali kuwa mbaya Marekani itaongeza wanajeshi Tanzania kwa lengo la kwenda kutoa msaada wa kibinadamu.Faida za mpango huu ni kwamba vikosi vya Marekani vitaongezwa na kukaa kwa muda mrefu Afrika mashariki na kuendelea kuchukua mafuta na rasilimali nyingine kama madini” akasema Jenerali Akiki

“Jenerali Akiki wazo lako ni zuri lakini linaonekana ni la hatari kubwa.Wasi wasi wangu ni vipi kama kirusi hicho

kitaweza kuvuka katika mipaka ya Tanzania na kusambaa sehemu mbali mbali duniani na hatimaye kikafika hadi Marekani? Tunaweza kuwa tumetengeneza silaha ambayo inakuja kutuua sisi wenyewe.Wanajeshi wetu walioko Tanzania wanaweza wakaambukizwa ugonjwa huo wakafa au wakaja kusambaza virusi hivyo huku Marekani”

“Mark Piller hiyo ndiyo njia pekee na ya haraka ambayo mnaweza mkaitumia ili vikosi vya Marekani viendelee kukaa Afrika

Mashariki na hasa Tanzania.Wanasayansi wenu watakapotengeneza kirusi hicho hatari watatengeneza pia na kinga yake na wanajeshi watakaokuwa Tanzania na wale watakaopelekwa huko watapata kinga hiyo hivyo wao hawatadhurika na hicho kirusi" akasema Jenerali Akiki.Mark Piller alishindwa ajibu nini wakabaki wamesimama wakitazama farasi kila mmoja akiwaza lake.

"Unalionaje wazo hilo Mark?akauliza Jenerali Akiki

“Jenerali Akiki ninashindwa kukupa jibu la haraka haraka kwani mpango huu ni mkubwa na wa hatari sana”

“Nini hofu yako Mark?akauliza Jenerali Akiki

“Hofu yangu ni kwamba tunaweza kutengeneza kirusi hicho hatari halafu kikageuka na kuwa kisu cha kutuangamiza sisi wenyewe.Kitu kama kirusi kinaweza kusambaa kwa haraka sana na kufika hadi Marekani kitu ambacho hatutaki kitokee na ndiyo

maana umeona Marekani hatupigani vita nyumbani tunamfuata adui huko huko aliko.Tunataka raia wetu wawe salama siku zote ndiyo maana ninahofu kwamba tunaweza kutengeneza kirusi na kikasambaa na kufika hadi Marekani na kuua watu wetu" akasema Mark Piller

"Hakuna haja ya kuwa na hofu Mark.Nimesema wanasayansi watengeneze kirusi na kinga yake na kila juhudi lazima zifanyike kuhakikisha kwamba kirusi hicho hakivuki nje ya mipaka

ya Tanzania.Mzilenge nchi za Tanzania,Uganda na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.Tena mkitaka kufanikiwa zaidi tengenezeni kirusi ambacho kitasambaa kwa njia ya hewa ili kiweze kusambaa kwa haraka zaidi.Nakuhakikishia Mark kwamba hii ndiyo njia pekee nyepesi ya kuweza kuongeza vikosi Afrika mashariki na kuendelea kuchota rasilimali.Njia nyingine kama makundi ya waasi hizo zitakuja baadae" akasema Jenerali akiki

“Jenerali Akiki naomba nilichukue suala hili na kwenda kujadiliana na wenzangu tuone namna tutakavyoweza kulitekeleza lakini ni suala zuri na ahsante sana kwa wazo hili zuri” akasema Mark Pillller

“Mark muda unakwenda kwa kasi na taratibu amani imeanza kurejea Tanzania na kama Tanzania ikiwa na amani basi hata Uganda nako kutakuwa na amani.Hampaswi kuacha jambo hili likatokea .Wakati wakiendelea na mikutano yao ya kutafuta

amani wanatakiwa wapigwe tena pigo lingine kabla majeraha yao hayajapona” akasema Jenerali Akiki

“Ahsante sana jenerali Akiki tutalizingatia hilo.Ninakwenda kuzungumza na wenzangu halafu nitakupa mrejesho nini tumekubaliana.

RIYADH – SAUDI ARABIA

Kiza kimeanza kutanda katika anga la jiji la Riyadh.Katika makazi ya Habiba Jawad idadi ya watu waliofika kuhudhuria msiba

wa mwanae Najma aliyezikwa mchana wa siku hiyo baada ya kujiua kwa kujipiga risasi ilikuwa kubwa.Ulikuwa ni msiba mkubwa kwa Habiba Jawad ambaye huyu alikuwa ni mtoto wake wa pili kufariki baada ya Edger Kaka.

Wakati watu wakiendelea na maombolezo Habiba Jawad aliyekuwa katika mojawapo ya nyumba zilizopo katika makazi yake akiwa na akina mama waliofika kumfariji, simu yake ikaita akaitoa haraka haraka kutazama mpigaji kisha akaikata ile simu.Taratibu

akainuka na kuaga anakwenda maliwato.Hakutaka mtu yeote amsindikize.Alitoka ndani ya ile nyumba akafuata ujia kuelekea katika nyumba yake na moja kwa moja akaenda katika ofisi yake akawasha runinga kubwa na akaonekana David Walker.

“Habari yako Habiba” akasema David Walker

“Nzuri David habari yako”

“Habiba unaonekana hauko sawa leo.Kuna tatizo lolote?akauliza David

“Nina msiba David.Mwanangu amefariki jana na leo tumemzika”

“Pole sana Habiba.Hukutujulisha kama una msiba”

“Usijali David.Nini kinaendelea huko? Akauliza Habiba

“Habiba kuna jambo ambalo limejitokeza na tunahitaji msaada wako”

“Sema David nini mnahitaji?akauliza Habiba

“Tumekuwa tunafuatilia kwa karibu sana kile kinachoendelea Tanzania na

siku ya leo Rais wa Tanzania amekutana na kiongozi wa dini na kubwa walilolizungumza ni kuhusiana na vurugu zinazoendelea katika ukanda huo wa Afrika mashariki.Mazungumzo hayo ya leo kati ya rais na kiongozi huyo yanaonekana kwa na mwelekeo wa kumaliza vurugu zile za kidini zinazoendelea Afrika Mashariki.Endapo vuruguzile zitamalizika basi hakutakuwa na ulazima wa vikosi vyetu kuendelea kuwepo Afrika mashariki na lengo letu ni kuendelea kukaa hapo kwa

muda mrefu na hata kuongeza wanajeshi zaidi.Kwa hiyo tumeamua kufanya kitu cha haraka ambacho kitatuwezesha kupeleka vikosi zaidi vya jeshi na kukaa Afrika mashariki kwa muda mrefu zaidi" akasema David Walker

"Mmekuja na mpango gani? Habiba akauliza

"Tunataka kutengeneza kirusi ambacho kitafanya maangamizi makubwa ambacho kitakuwa hatari kuzidi kirusi cha Ebola.Tutakwenda kukisambaza kirusi hicho

Tanzania na baada ya hali kuwa mbaya tutatuma vikosi zaidi vya jeshi kwenda huko kwa lengo la kutoa msaada lakini papo hapo operesheni zetu zikiendelea kama kawaida”

“David hili la kusambaza kirusi huoni kama ni jambo la hatari?Ni vipi kama kirusi hicho kitavuka mipaka na kusambaa sehemu nyingine duniani?Mnao wanajeshi wenu kule ni vipi kama wakipata virusi hivyo? Akauliza Habiba

“Hilo tayari tumekwisha lijadili kwa kirefu

sana.Mwanasayansi anayeandaa kirusi hicho tumempa maelekezo ya kuhakikisha kwamba atakapokamilisha kutengeneza kirusi hicho aandae na kinga yake kwa ajili ya wanajeshi wetu na tahadhari endapo kirusi hicho kitavuka mipaka ya Afrika Mashariki na kuenea sehemu nyingine duniani.Hilo halina tatizo kabisa Habiba”

“Nini natakiwa kufanya kwa upande wangu?akauliza Habiba ambaye hakuonekana kutaka maongezi marefu

“Kwa upande wako tunataka utusaidie kupata mtu ambaye atapeleka kirusi hicho Tanzania.Tunataka mtu kutoka kundi la IS”akasema David

“David kwa nini lazima awe ni mtu kutoka IS?akauliza Habiba

“Habiba hili ni shambulio la kibaolojia hivyo basi mtu huyo hapaswi kuwa mmarekani.Tunataka kumtuma mtu wa kundi la IS ili hata kama akigundulika basi ijulikane kuwa ni kundi la IS ndio waliofanya shambulio

hilo.Nataka ufanye makubaliano na kundi la IS wape fedha za kutosha waweze kutupatia huyo mtu ambaye anatakiwa hapa Marekani haraka sana ili aanze kuandaliwa.Mtu huyo atawekewa kwanza kinga ya kumkinga dhidi ya kirusi hicho halafu atapandikizwa kirusi hicho ambacho atakwenda kukisambaza Tanzania” akasema David Walker

“Lini huyo mtu anahitajika?akauliza Habiba

“Tunamuhitaji haraka iwezekanavyo.Tunataka kabla

ya amani haijarejea Tanzania basi tuwapige na hicho kirusi.Hatutaki kuwapa nafasi ya kupumua.Namuhitaji huyo mtu haraka sana.Fanya kila uwezalo mtu huyo aweze kupatikana haraka sana" akasema David

"Sawa David nitajitahidi"

"Ahsante sana Habiba na pole sana kwa tatizo hili kubwa.Kuna chochote tunaweza kusaidia?

"Ahsante David.Tutawasiliana pale nitakapokuwa nimempata

huyo mtu” akasema Habiba na kuzima ile runinga

“Mauaji yanayoendelea hivi sasa nchini Tanzania bado hayatoshi na wanataka kusambaza tena virusi na kuendelea kuua watu.Yote hii ni kwa sababu ya kutaka kuchukua rasilimali ambazo Mungu amewajalia watu wa Afrika Mashariki.Lazima nitafute namna ya kufanya ili niweze kuzuia mpango huu usifanikiwe.Ningeweza kumpigia simu Mathew Mulumbi lakini sifahamu mahala alipo hivi sasa.Hata

hivyo lazima nifanye kitu.Huu lazima uwe ni mwisho wa hiki kikundi chenye kufanya maangamizi makubwa duniani" akawaza Habiba na kuwasiliana na mtu mmoja kutoka kundi la IS akampa maelekezo kama alivyokuwa ameelekezwa na David na mtu Yule akamtaka Habiba ampe muda alishughulikie lile suala kisha atamjulisha.Alimtajia kiasi cha fedha ambacho angetakiwa kukitoa kwa ajili ya suala lile.Baada ya kulimaliza hilo suala Habiba akarejea katika nyumba waliko akina

mama waliokuja kuungana naye katika msiba.

Saa tatu za usiku wakawasili Abu Dahir na mke wake Nawal.Kama ilivyokuwa kwa Mathew na Najma nao pia walikuwa mapumzikoni.Habiba Jawad aliwapa wanae wote mapumziko ya miezi minne.Abu Dahir na Nawal hawakuweza kuwahi mazishi ya Najma kutokana na kutopata taarifa kwa haraka.Baada ya kuwasili Abu Dahir alikwenda kuungana na waombolezaji wengine

waliofika pale nyumbani kuwafariji.Nawal yeye alikwenda kuungana na akina mama waliokuwa wanamfariji Habiba.

Saa tano za usiku tayari watu wengi walikwisha ondoka.Ni watu wachache tu waliokuwa wamebaki na ndipo Abu Dahir alipoweza kupata nafasi ya kuzungumza na mama yake ili aweze kumueleza kile kilichotokea hadi kupelekea Najma kujiua kwa kujipiga risasi.Habiba Jawad akawataka Abu Dahir na Nawal waelekee nyumbani

kwake akawakaribisha katika sebule yake

“Mama utatusamehe sana kwa kushindwa kuwahi mazishi ya Najma.Tuliipata taarifa kwa kuchelewa na tulijitahidi sana kwa kila namna ili tuweze kuwahi leo lakini ilishindikana ” akasema Abu Dahir

“Usijali Abu.Nilifahamu hamtaweza kuwahi mazishi” akasema Habiba

“Mama nini hasa kilichotokea? Kwa nini Najma alijiua?Abu Zalawi yuko wapi?akauliza Abu Dahir

akionekana kuwa na shauku sana ya kutaka kufahamu kila kitu kuhusiana na tukio lile.

“Poleni sana vijana wangu kwa hiki kilichotokea.Mpaka sasa bado siamini kama kweli Najma binti yangu wa pekee amekwenda na hatutamuona tena.Najma ameondoka na afya na uzuri wake.Imeniumiza sana” akasema Habiba Jawad

“Nini hasa kimetokea mama hadi kupelekea Najma kuchukua maamuzi haya magumu namna hii? Akauliza Abu Dahir

“Ni hadithi ndefu Abu lakini lazima nikiri kwamba mimi ndiye niliyesababisha kifo chake”

“Wewe ndiye uliyesabisha kifo chake? Kivipi mama? Abu Dahir akauliza

“Sikumuua kwa mkono wangu lakini kuna maneno nilimueleza na hayo ndiyo yaliyopelekea akachukua maamuzi yale ya kujiua”

“Ulimweleza nini mama? Akauliza Nawal na Habiba akamtazama Abu Dahir kisha akasema

“Nilimueleza ukweli”

“Ukweli? Abu Dahir akashangaa

“Ndiyo Abu.Dada yako nilimueleza ukweli”

“Sijakuelewa mama.Ukweli upi uliomueleza hadi akaamua kujipiga risasi? Abu Dahir akauliza

“Kuna mambo mengi ambayo wewe na ndugu zako hamkuwa mkiyafahamu hasa kuhusu mimi na kile kinachoendelea katika maisha yangu.Nadhani ni wakati wa kuweka mambo wazi ili wewe pia ufahamu” akasema Habiba na Nawal akasimama

“Nawal unakwenda wapi? Habiba akauliza

“Ninadhani mazungumzo haya yanawahusu zaidi ninyi” akasema Nawal

“Hapana Nawal kaa.Wewe pia ni mwanafamilia na ni sehemu ya haya ninayotaka kuyazungumza.Umefika wakati wa kila kitu kuwekwa mahala peupe” akasema Habiba

“Huyu mama anataka kufanya nini tena?Mbona muelekeo wake siuelewi?akajiuliza Nawal

“Mama kabla hujaendelea nataka kufahamu yuko wapi Abu Zalawi? Abu Dahir akauliza

“Abu Zalawi hayupo na hajui kama mke wake Najma amefariki dunia”

“Hajui kuhusu kifo cha Najma? Akauliza Nawal

“Ndiyo hajui chochote kuhusu kifo cha Najma”

“Mama nashindwa kuelewa.Hawa walikwenda mapumzikoni kama tulivyofanya sisi.Nini kili.....”

“Niliwarudisha mimi” akasema Habiba na kumkatisha Abu Dahir

“Nilimuhitaji Abu Zalawi hivyo nikawasiliana nao na kuwataka warudi nyumbani mara moja.Baada ya kurejea mimi na Abu Zalawi tulifanya safari ya kwenda Marekani na Abu Zalawi alibaki huko”

“Alibaki huko? Nawal akauliza

“Ndiyo.Alibaki huko na ninapenda kuwajulisha kwamba AbuZalawi hatarejea tena hapa kwetu.Amekwisha ondoka katika maisha yetu”

“Mama sijakuelewa.Nini kinaendelea hapa? Mama naomba tafadhali unieleze kila kitu.Naona kuna mambo mengi yamejificha hapa”Akasema Abu Dahir

“Abu kama unavyofahamu kwamba baba yako alikuwa mstari wa mbele sana katika kupigania haki na aliuawa akiwa katika mapambano ya kudai haki za wapalestina.Baada ya kifo chake nilivaa viatu vyake na kuendelea na harakati za kudai haki.Nimekuwa nikitoa msaada wa kifedha kwa

vikundi mbali mbali vinavyoendesha harakati za kudai haki za wapalestina kutoka kwa taifa la Israel.Si vikundi vya kipalestina tu ambavyo vimekuwa vikipokea msaada kutoka kwangu katika kufanikisha harakati mbali mbali za kudai haki bali nimekuwa nikifadhili makundi mengine kama vile IS kufanikisha mipango yao mbali mbali.Kundi la IS linajulikana kama kundi hatari zaidi la kigaidi kwa sasa duniani na kitendo cha kulifadhili kimenifanya

niwindwe na mashirika mbali mbali ya kijasusi na hasa Mossad.Pamoja na kuwindwa huko na Mossad lakini hadi leo hii hawajawahi kunikamata.Umeshawahi kujiuliza swali kwa nini? Akauliza Habiba na Abu Dahir akatikisa kichwa kwamba hajaui.

“Kuna siri imejificha hapa kwa nini sijawahi kukamatwa licha ya kutajwa kuwa mfadhili mkubwa wa makundi ya ugaidi duniani” Habiba akanyamaza na kuwatazama Abu Dahir na Nawal

“Siri ambayo hamuifahamu ni kwamba ninafanya ufadhili huu kwa makundi ya magaidi kwa niaba ya Marekani”

“Marekani ? Abu Dahir akashangaa

“Ndiyo Abu.Mimi ni wakala wao.”

“Marekani wanafadhili ugaidi? Abu akazidi kushangaa

“Ni vigumu kuamini Abu lakini huo ndio ukweli”

“Marekani imekuwa ikiendesha vita dhidi ya ugaidi duniani na tumekuwa tukiona namna inavyopata mafanikio

makubwa katika vita dhidi hiyo.Iweje kwa upande wa pili wawe na ushirika na magaidi? Akauliza Abu

“Hiyo ni siri kubwa Abu Dahir.Ni siri ambayo hata Rais wa Marekani haifahamu” akasema Habiba na kunyamaza kidogo

“Ndani ya shirika la ujasusi la Marekani CIA kuna kitengo maalum ambacho kinashughulika na jambo hilo.Ni kitengo cha siri sana na hata waliomo ndani ya CIA hawakifahamu” Habiba

akanyamza baada ya Nawal kuonyesha mshangao

“Kitengo hiki kazi yake kubwa ni kushughulikia mahusiano na makundi ya kigaidi kwa maslahi ya Marekani.Baba yako ndiye aliyekuwa akitumiwa katika kufadhili ugaidi na aliuawa baada ya kwenda kinyume na matakwa ya Marekani.Baada ya kuuawa nilivaa viatu vyake na kuendelea na kile alichokuwa anakifanya”

“Siamini hayo unayonieleza mama.Kwa muda

huu wote mmekuwa mkifanya kazi kwa niaba ya Marekani?

“Ndiyo Abu.Tumekuwa tukifanya kazi kwa niaba ya Marekani.Alianza baba yako na mimi nimefuata na utajiri huu wote tulionao umetokana na hicho tunachokifanya.Wameniwezesha utajiri mkubwa niweze kuutumia kufadhili ugaidi kwa niaba yao.Hawataki kujulikana”

“Kwa nini ukakubali mama kubeba jukumu hili kubwa mabegani mwako?Kwa nini ukakubali kuchafua jina lako

kwa kuwa mfadhili wa ugaidi duniani wakati kumbe wafadhili wakuu wa ugaidi wapo? Akauliza Abu Dahir

“Ilikuwa ni lazima nifanye hivyo Abu.Hii imekuwa ni siri yangu kubwa sana na sikupanga kuwaeleza lakini imebidi mfahamu kila kitu” akasema Habiba

“Kwa nini umeamua kutueleza mama? Akauliza Nawal

“Kwa sababu ni wakati muafaka kwa ninyi kufahamu kile kinachoendelea” akajibu Habiba

“Kama nilivyokueleza Abu kwamba baba yako ndiye aliyekuwa wa kwanza kuifanya kazi hii na mimi niliendelea pale alipoishia yeye.Nimeifanya kazi hii kwa muda mrefu kwa maslahi ya marekani na sasa umefika wakati ambao sitaki kuendelea tena na hiki ninachokifanya kwani hakipendezi machoni pa Mungu.Nimekwisha kuwa mzee sasa na ninahitaji kujiweka karibu na Mungu wetu na sitaki tena kuendelea kukatili roho za watu wasio na hatia.Katika makubaliano yetu

na kikundi hiki ni kwamba nitaifanya kazi hii ya kufadhili ugaidi kwa niaba yao hadi pale nitakapovuta pumzi yangu ya mwisho na ndiyo maana wameniwezesha kuwa na utajiri mkubwa sana.Kitendo chochote cha kutaka kujiondoa katika jambo hili ni kuhatarisha usalama wangu na wa familia yangu.Hivi tuzungumzavyo ninyi wanangu wote mnafuatiliwa na muda wowote ambao nikijaribu kwenda kinyume na matakwa yao watawaondoa ndiyo maana nimekuwa kimya

sijawahi kuwaeleza kuhusu jambo hili.Nataka muwe salama” akasema Habiba

“Unataka tuwe salama? Akauliza Abu Dahir kwa ukali

“Abu chunga ulimi wako unapozungumza nami ! akafoka Habiba akionekana kutopendezwa na namna mwanae alivyouliza kwa ukali

“Mama ingekuwa vyema ungeendelea kubaki na siri hii na ukafa nayo.Kuamua kutueleza ukweli ni kuhatarisha zaidi maisha yetu.Tazama umemueleza

ukweli Najma na akaamua kujiua” akasema Abu Dahir

“Abu imenilazimu niwaeleze ukweli ili hata ikitokea nikiondoka leo mjue ni kitu gani kilikuwa kinaendelea katika maisha yangu” akasema Habiba na kunyamaza akamtazama Abu

“Ili niweze kujiondoa katika jambo hili ilinilazimu kuja na mpango maalum na hapo ndipo nilipoamua kuwaleta hapa Abu Zalawi na Nawal” akasema Habiba na kunyamaza.Nawal alionyesha wasi wasi mwingi

“Abu Dahir,kuna jambo ambalo hujalifahamu bado” akasema Habiba

“Mama una siri nyingi umetuficha.Tafadhali kama umeamua kueleza ukweli tueleze kila kitu” akasema Abu Dahir

“Ni kuhusu Abu Zalawi na Nawal” akasema habiba

“Mama” akaita Nawal

“Nawal muache mama aseme anachotaka kukisema” akasema Abu Dahir

“Nawal usiwe na hofu.Nataka kila kitu kiwe wazi leo” akasema Habiba

“Endelea mama.Kuna nini kuhusiana na hawa watu wawili? Akauliza Abu Dahir

“Abu Zalawi na Najma nimewatoa katika lililokuwa kundi la Ammar Nazari brigades.Wawili hawa ni majasusi na walikuwa katika misheni maalum na siyo magaidi.Niliamua kuwachukua na kushirikiana nao kwa ajili ya kw……”

“Mama sijakuelewa.Umesema Nawal na Abu Zalawi ni majasusi na si magaidi?Nawal si alikuwa mke wa Ammar Nazari?

Akauliza Abu Dahir na kabla Habiba hajajibu Nawal akasimama

“Ni kweli Abu Dahir hiki anachokisema mama yako” Akasema Nawal na kutazama na Abu

“Siamini masikio yangu ! akasema Abu Dahir

“Mama yako ameamua kuweka kila kitu wazi hivyo hakuna haja ya kuficha chochote.Ni kweli mimi na Abu Zalawi ni majasusi na tulikuwa katika kundi la Ammar Nazari Brigades kwa misheni maalum.Mimi ni

jasusi toka CIA Marekani na mwenzangu Abu Zalawi anatokea Mossad.Jina lake halisi ni Mathew Mulumbi na si Abu Zalawi kama anavyojulikana.Katika kundi la Ammari Nazari Brigades mimi nilikuwa na kazi ya kumsaka gaidi mmoja ambaye ana undugu na Ammar Nazari ambaye aliwahi kufanya mauaji makubwa Marekani na kukimbia hivyo niliuganishwa na Ammar na nikawa mke wake.Abu Zalawi yeye alitokea Mossad na alikuwa na misheni maalum aliyotumwa

kuitekeleza ambayo ni kumuua Habiba Jawad.Mossad wanafahamu kwamba Habiba amekuwa akifadhili makundi mbali mbali ya wanamgambo wa kipalestina ambao wamekuwa wakiendesha mashambulio mbali mbali ndani ya Israel hivyo wanamtafuta sana Habiba na wakamtumia Abu Zalawi ili kuungana na Ammari Nazari na kutengeneza njia ya kufika kwa Habiba Jawad.Baada ya Ammar Nazari kuuawa na vikosi vya Israel mimi na Abu tuliondoka na kuanza harakati

za kumsaka Habiba Jawad lakini tulipofika hapa misheni ikabadilika.Ile mipango ya kumuua Habiba Jawad ikatoweka na badala yake tukajikuta tukiungana na Habiba Jawad katika mipango yake na kuwa wanafamilia” akasema Nawal na Abu Dahir akaonekana kuchanganyikiwa.

“Abu Zahir anachokisema mama yako ni……” akasema Nawal na Abu akamnyamazisha

“Nyamaza ! akasema Abu Dahir kwa sauti kali

“Wewe na huyu mwanamke wote mko sawa.Wote mama yenu mmoja.Wote ni mashetani waongo wakubwa.Nawal nilikupenda sana na nikawa tayari kufanya chochote kwa ajili yako.Kwa nini nawe ukashiriki uongo huu mkubwa wa mama? Na wewe mama kwa nini ukanishawishi nimuoe Nawal wakati ukifahamu kwamba ni jasusi? Kwa nini hukunieleza ukweli? Akafoka Abu aliyekuwa amepandwa na hasira

“Nilikuwa na sababu maalum za kutaka umuoe Nawal”

“Ulikuwa unachunguza maisha yetu mimi na Najma ndiyo maana ukatutaka tuwe na mahusiano na hawa majasusi ? Abu akauliza

“Hapana sijawahi kuwachunguza.Nilitaka kuwalinda”

“Mama wewe una roho ya kishetani kabisa ndiyo maana hujawahi kusikitika hata siku moja kwa watu wanaouawa na magaidi ambao unawafadhili.Najuta kuzaliwa

nawe Habiba ! akasema kwa ukali Abu Dahir na Nawal aliyekuwa karibu yake akamnasa kofi

“Iwe ni mara ya kwanza na ya mwisho kumtusi mama yako.Pamoja na yote anayoyafanya na aliyoyafanya huyu bado ni mama yako na ataendelea kuwa mama yako daima.Huyu ndiye aliyekubeba tumboni mwake miezi tisa na akakulea hadi umefika hapa ulipofika.Nakuonya tena ukithubutu kumtusi mama yako mbele yangu

nitakufundisha adabu.Hapa unaponiona mimi sina uwezo wa kuzaa mtoto.Nimekwisha ondolewa kizazi.Unajua ni uchungu gani ninaupata kwa kukosa mtoto?Usirudie tena kumtusi mama yako ! akasema Nawal kwa ukali huku akilengwa na machozi.Abu Dahir akamtazama Nawal kwa macho ya mshangao.

“Huna kizazi?! Akauliza akiwa ameshika shavuni mahala aliponaswa kofi

“Ndiyo sina kizazi na siwezi kupata mtoto ! akajibu Nawal bila hofu

“Nawal toka tumefunga ndoa tumekuwa katika jitihada mbali mbali za kutafuta mtoto na umekuwa unanihakikishia kwamba tutapata mtoto hivi karibuni ! Oh Mungu wangu ! akasema Abu kwa masikitiko

“Ulikuwa ni uongo.Sina uwezo wa kubeba mimba ! akasema Nawal.

Ghafla Abu Dahir akainua taa ya mezani iliyokuwa katika meza ndogo pembeni na pale alipokuwa amekaa na kumpiga nayo Nawal ikapasuka.Abu Dahir akachukua birika na kumrushia Nawal

akalikwepa.Abu alionekana kama vile amepatwa na kichaa

“Ninyi wanawake leo mtanitambua mimi ni nani ! akafoka Abu huku akirusha vitu kumpiga navyo Nawal

“Abu acha ujinga huu tafadhali ! akafoka Habiba

“Wewe mama ndiye uliyeyataka haya yote.Una roho mbaya sana! Akafoka Abu na kuinua chungu cha maua kilichokuwa dirishani kwa lengo la kumpiga nacho mama yake lakini Nawal alikwisha isoma dhamira yake akajiinua pale chini alipokuwa akaruka

na kukipiga teke chugu kile kikaanguka na kuvunjika.Nawal ambaye hasira zilikwisha mpanda akamrukia Abu mateke mawili mfululizo yaliyomrusha Abu hadi ukutani akajigonga kwa kishindo na kuanguka chini halafu akamfuata Habiba

“Mama uko sawa?Hajakuumiza huyu?akauliza Nawal

“Nimeumia kidogo.Ahsante kwa kuniokoa” akasema Habiba na Nawal akageuka kumtazama Abu Dahir ambaye alikuwa amelala

pale chini akionekana kutokuwa na fahamu.Haraka haraka akamfuata na kujaribu kumtikisa huku akimuita jina lake lakini hakuitika.Akageuka kumtazama Habiba Jawad ambaye naye alionyesha hofu baada ya kuiona sura ya Nawal,akainuka na kumfuata akamtazama Abu Dahir ambaye hakuwa na fahamu.Bila kupoteza muda Habiba akampigia simu daktari wake anayeishi pembeni ya nyumba yake ambaye alifika mara moja akampima Abu kisha akasema

“Anatakiwa akimbizwe hospitali haraka sana !

Habiba akainuka akachukua simu na kuwapigia wasaidizi wake ambao walifika haraka haraka na kumchukua Abu Dahir wakamuingiza garini wakamkimbiza hospitali.Habiba na Nawal nao wakaingia garini wakaelekea hospitali.

“Mama ni vipi kama nimempiga Abu sehemu mbaya? Akauliza Nawal akionekana kuwa na hofu

“Usijilaumu Nawal.Ulifanya ulichopaswa

kukifanya.Kama usingefanya vile Abu angenipiga na kile chungu na pengine ningeweza hata kupoteza maisha.Kwa sasa tumuombee ili aweze kuwa salama.Sitaki kupoteza tena mtoto mwingine.Nimekwisha poteza watoto wawili tayari na nimebaki na huyu mmoja" akasema Habiba na kufuta machozi

"Lakini mama kwa nini uliamua kufanya hivi ulivyofanya?Kwa nini uliamua kuwaeleza ukweli wanao?akauliza Nawal

“Ilikuwa lazima wafahamu Nawal.Sikutaka kuendelea kuwaficha kwani endapo ningefariki dunia bila kuwaeleza ukweli yawezekana nao wangeendelea kufanya kile ambacho mimi na baba yao tumekuwa tunakifanya.Sitaki watoto wangu waendelee kufadhili ugaidi,sitaki waendelee kumwaga damu za watu kama nilivyofanya mimi” akasema Habiba

“Ulifanya kitu kizuri kuwaeleza ukweli lakini kwa bahati mbaya mambo hayakwenda kama ulivyokuwa

umekusudia” akasema Nawal.Habiba akafuta machozi na kusema

“Nadhani Mungu ananiadhibu kwa mambo niliyoyafanya.Nimefanya mambo mengi maovu.Damu nyingi imemwagika kwa sababu yangu na haya ndiyo mapigo ninayoyapata.Naomba Mungu asimchukue Abu Dahir kwani ni mtoto pekee niliyebaki naye” akasema Habiba na kuchukua simu akampigia mmoja wa madaktari katika hospitali alikoelekeza apelekwe Abu

Dahir akamjulisha kuwa mwanae amepatwa na matatizo na anapelekwa pale hospitali akaomba ashughulikiwe haraka

Abu Dahir alifikishwa hospitali ambako tayari wauguzi walikuwa wamejiandaa wakimsubiri,akashushwa haraka haraka katika gari na kuweka katika kitanda kikakimbizwa ndani katika chumba cha wagonjwa mahututi ambako alianza kupatiwa matibabu.Dakika chache baada ya Abu Dahir

kuingizwa katika chumba cha wagonjwa mahututi,Habiba Jawad na Nawal wakawasili.Habiba alifahamika pale hospitali akapokewa na kupelekwa sehemu ya kusubiri madaktari watakapomaliza kumuhudumia mgonjwa wake.

Baada ya dakika saba mlango wa chumba cha wagonjwa mahututi ukafunguliwa na daktari akatoka.Habiba akasimama na kumfuata daktari akamtaka waelekee ofisini kwake

“Kijana wangu anaendeleaje daktari?akauliza Habiba akionekana kuwa na hofu

“Mama Habiba tumejitahidi kadiri ya uwezo wetu lakini tumeshindwa kuokoa maisha ya mwanao.Uchunguzi wa awali unaonyesha ana jeraha kichwani.Nini hasa kilimtokea? Amepata ajali? Akauliza Daktari na Habiba Jawad akashindwa kumjibu.Yeye na Nawal wakakumbatiana wakilia.

“Ahsante Mungu kwa kila jambo.Wewe ndiye mwenye kutoa na kutwaa kwa muda uutakao.Hatuwezi kupingana na maamuzi yako japo tungependa tuendelee kuwa pamoja na Abu Dahir lakini nakushukuru kwa muda ambao umempa hapa duniani.Naomba utupe nguvu ya kulihimili jambo hili” akasema Habiba machozi yakimwagika

Habiba Jawad na Nawal wakapelekwa katika chumba ulikokuwa mwili wa Abu Dahir

“Saa chache zilizopita tulikuwa wote ndegeni tukirejea Riyadh kuhudhuria msiba wa dada yako,sikuhisi kama ulikuwa unayafuata mauti yako.Abu Dahir mimi ndiye nimesababisha kifo chako nitalia machozi gani kwa hili nililolifanya? Najua ulikuwa unanipenda sana lakini umekufa ukiwa na hasira nami baada ya kuufahamu ukweli kuhusu maisha ya mama yako na kuhusu mimi.Najuta kwa nini sikukueleza ukweli kuhusu mimi kuwa ni jasusi wa

CIA.Najuta kwa nini sikukueleza ukweli kama sina uwezo wa kukupatia mtoto kwani ni jambo hili ndilo lililokupa hasira zaidi.Nisamehe Abu Dahir huko uliko.Nisamehe ! akalia Nawal akiwa amesimama pembeni ya mwili wa Abu Dahir.Wote wawili Habiba na Nawal machozi yalikuwa yanawabubujika.Walitumia dakika kumi ndani ya kile chumba kisha wakatoka na kuondoka kurejea nyumbani

“Mama nimemuua mume wangu.Nimemuua mwanao

pekee aliyesalia” akasema Nawal wakiwa garini huku akimwaga machozi.Habiba akageuza shingo akamtazama Nawal na kumuinamisha kifuani kwake akamkumbatia

“Nawal narudia kukusisitiza kwamba haya yote yanayotokea ni mipango ya Mungu na hupaswi kujilaumu kwa hili lililotokea.Ilikuwa iwe hivyo.Abu Dahir aliandikiwa afe kifo cha namna ile hivyo hakuna namna ambayo ungeweza kukwepa.Lakini tambua kwamba haya yote yanayoendelea hivi sasa ni

matokeo ya maisha niliyoishi mimi.Ni mapigo yatokanayo na matendo yangu.Nimetesa watu wengi sana.Machozi ya akina mama waliopoteza watoto wao katika mashambulio yaliyofanywa na makundi ya kigaidi ambayo ninayafadhili hayajaniacha salama.Machozi ya watoto ambao wamebaki yatima baada ya kuwapoteza wazazi wao katika mashambulo ya kigaidi niliyoyafadhili haya ndiyo malipo yake.Nimepoteza watoto wangu wote niliowazaa na sasa nimebaki

mwenyewe.Pamoja na mapigo haya lakini Mungu hajaninyima kila kitu.Amewachukua watoto wangu lakini ameniletea watoto wengine ambao ni wewe na Mathew” akasema Habiba na Nawal akainua kichwa chake

“Mama umeongea kuhusu Mathew.Nataka kufahamu mahala alipo.Sijamuona katika msiba wa Najma” akauliza Nawal

“Mathew ameondoka hatarejea tena kama nilivyowaambia na hilo ni

moja kati ya mambo yaliyopelekea Najma akachukua maamuzi ya kujiua” akasema Habiba

“Mathew amekwenda wapi? Amekufa?

“Hapana hajafa.Nawal tutazungumza baadae lakini kwa sasa tujielekeze katika msiba wa Abu na tutakapomaliza tutazungumza” akasema Habiba

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Ndege ya jeshi aliyopanda Mathew iliwasili jijini Dar es salaam.Kutoka angani ni sehemu chache tu za jiji la Dar es salaam ambazo zilionekana kuwa na umeme.Sehemu kubwa ya jiji la Dar ilikuwa gizani kutokana na miundo mbinu ya umeme kuharibiwa katika machafuko yaliyokuwa yanaendelea.

“Nimezoea kuliona jiji la Dar es salaam kutokea angani likiwaka taa kila sehemu lakini leo hii jiji limetanda giza kila

sehemu.Kwa tamaa ya mali ambazo Mungu ametujalia ziwepo katika nchi zetu,mabepari wametufikisha hapa.Ni mara ya kwanza Tanzania tumefikishwa hatua hii ya kuchinjana wenyewe kwa wenyewe.Ninaapa kwa gharama zozote zile lazima kikundi hiki cha hawa watu waliotufikisha hapa kwa tamaa za mali yetu nikifutilie mbali na dunia lazima ifahamu kile ambacho mataifa makubwa yanafanya katika nchi ndogo.Huu ni unyama uliopitiliza.Ni unyonyaji usio

na mfano.Naamini haya ni maongozi ya Mungu hadi akanifikisha katika kundi hili ambalo limeigeuza nchi yetu uwanja wa mauaji.Tayari nimefahamu kuwa ni Marekani ndio waliotengeneza machafuko haya kwa manufaa yao.Hawako peke yao lazima kuna watu wa hapa nchini au katika nchi za Afrika mashariki ambao wanashirikiana nao katika kuanzisha na kuchochea vurugu hizi.Hawa ndio wanaotakiwa kusakwa kwa haraka sana na kujulikana ni akina nani na kama

tukifanikiwa kuwapata hawa basi tutakuwa tunaweza kusaidia kumaliza vurugu hizi.Kuna nguvu mbili hapa ambazo zimeifikisha Tanzania hapa tulipofika.Ipo nguvu ya ndani na nguvu ya nje.Inabidi kuanza na nguvu ya ndani kisha nitaendelea na wale wa nje.Naapa hakuna aliyeifikisha Tanzania hapa atabaki salama”akawaza Mathew na kumkumbuka Ruby

“Nilijaribu kumpigia simu Ruby lakini hakupatikana.Nina wasi wasi sana na usalama wake.Gosu

Gosu naye sijui anaendeleaje.Nawahitaji sana hawa watu kama watakuwa wazima katika kuhakikisha tunaiokoa nchi yetu kutoka katika machafuko.Ninachoelewa hawa jamaa kwa vile wamekwisha ingia Afrika Mashariki lazima wataotesha mizizi na kuhakikisha kwamba wanaendelea kuchota utajiri wetu.Naomba niwakute wote wako salama" akawaza Mathew na kutaarifiwa kwamba ndege inakaribia kutua katika uwanja wa ndege

wa Julius Nyerere ambao toka vurugu zilipoanza ulikuwa umefungwa na ukilindwa na wanajeshi .

Ndege ile ya jeshi la Marekani ikiwa na vifaa mbali mbali vya wanajeshi wa Marekani waliokuwa nchini Tanzania ikatua salama.Mizigo ikapakuliwa na kuingizwa katika magari kisha wanajeshi waliokuja na ndege ile wakaingia katika magari maalum ya jeshi la Marekani na msafara ukaondoka kuelekea katika kambi yao

Mathew Mulumbi akiwa ni mmoja wao

“Hawa jamaa hawajui kama hapa nimefika nyumbani.Watakapogundua kwamba mimi ni mtanzania tayari watakuwa wamechelewa sana lakini kwa sasa ngoja niendelee kujifanya mimi ni mgeni wa hapa Tanzania ili niendelee kuusoma mtandao wao” akawaza Mathew na kuona namna alivyokuwa anachungwa.Ndani ya gari alilokuwa amepanda kulikuwa na wanajeshi wanne wenye

silaha na gari lile liliwekwa kati kati ya msafara.

“Nadhani wameelekezwa wanichunge ndiyo maana wameniweka katikati.Hawapaswi kuwa na hofu nitafanya walivyonieleza lakini watajuta sana na kumlaumu Habiba Jawad kwa kuwakutanisha na mimi.Safari hii ninataka nifanye kitu ambacho kitakuwa cha kihistoria.Tumeonewa vya kutosha na sasa ni wakati wa kuwaonyesha haya mataifa makubwa kwamba hata sisi tunao uwezo na tumechoshwa

na mambo wanayotufanyia” akawaza Mathew akiyaelekeza macho yake nje

“Dar es salaam haikuwa hivi.Hili ni jiji lililokuwa linakesha lakini muda huu barabara tupu hakuna watu mitaani.Sipati picha namna maisha yalivyo magumu hivi sasa.Maduka yamefungwa,upatikanaji wa chakula na mahitaji muhimu imekuwa ni shida lakini baadhi ya watu wachache wao wanaishi maisha mazuri na kupata kila wanachokihitaji wakisahau kwamba kuna

mamilioni ya watu wanaoteseka huku Tanzania na Afrika mashariki kwa sababu yao.Tunatakiwa kupambana kuhakikisha tunairejesha nchi yetu ilivyokuwa na ili kumaliza vurugu hizi ni lazima kuuchimbua mzizi wenyewe ambao ni kikundi kile kidogo ndani ya CIA” akawaza Mathew huku wakiendelea kukata mitaa ya jiji la Dar es salaam ambayo kwa usiku huu ilikuwa kimya.Mioto ya matairi na moshi mzito vilionekana katika baadhi ya

barabara na hata majengo yanayoungua moto pia yalikuwepo.Katika baadhi ya barabara walikuta zimefungwa kwa mawe makubwa

“Hali ilivyo Dar es salaam utadhani kuna filamu inatengenezwa kumbe ni hali halisi .Inasikitisha sana ! Narudia tena kuahidi kwamba wale wote waliotufikisha hapa hakuna atakayebaki salama.Tanzania hatukupaswa kufikishwa hapa.Lakini hili ni funzo kwa watanzania ili wawe macho kulinda amani yao.Wamekuwa wakihubiriwa

kwa miaka mingi kwamba siku amani hii ikipotea watajuta.Wamejaribu kuchezea amani na wameona madhara yake.Hakuna sehemu ya kukimbilia imelazimu wayakimbie makazi yao na kujificha katika makambi.Kwa haya wanayokutana nayo naamini hata akija tena mtu mwingine siku nyingine kutaka kuwarubuni kuchezea amani yao hawatajaribu tena” Mathew akatolewa mawazoni baada ya msafara wao kukutana na kundi kubwa la vijana waliokuwa wamebeba

mienge na silaha huku wakiimba.Ikalazimu wanajeshi wa Marekani kutumia risasi za moto kuwatawanya kwani baadhi yao walikuwa na silaha na walianza kushambulia magari katika ule msafara.Baada ya kundi lile la vijana kutawanyika magari yakaongeza mwendo na moja kwa moja wakaelekea katika uwanja wa uhuru ambako ndiko kulikuwa na kambi kubwa ya wanajeshi wa Marekani na vifaa vyao vyote vilikuwa vinahifadhiwa huko.Kambi nyingine ilikuwa

ufukweni mwa bahari ya Hindi.

Mathew alishushwa garini na kukabidhiwa kwa mmoja wa viongozi wa kambi ile ambaye alimpeleka hadi katika hema.

“Karibu Tanzania.Jina lako nani? Akauliza Yule jamaa

“Abu Zalawi” akajibu Mathew kikakamavu

“Abu Zalawi nimeelekezwa na viongozi wangu kwamba nikupokee na kisha nitakukabidhi kwa mtu ambaye atakuja hapa

kukuchukua.Umewahi kufika Tanzania kabla? Akauliza

“Hapana sijawahi” akajibu Mathew

“Hali ni mbaya sana hasa hapa Dar es salaam na jiji la Tanga pia.Nadhani umejionea hali halisi huko mitaani wakati mkija hapa”

“Ndiyo mkuu.Tumekutana na kundi kubwa la vijana wakiwa na silaha na kushambulia msafara wetu”

“Basi hiyo ndiyo hali tunayokutana nayo kila siku katika kujaribu kurejesha hali

ya amani tukishirikiana na vikosi vya ulinzi vya Tanzania”

“Endelea kupumzika na atakapofika mwenyeji wako nitakufahamisha” akasema Yule mwanajeshi na kutoka nje ya lile hema akamuacha Mathew peke yake.

“Naamini huyo mtu anayekuja kunichukua ni mmoja kati ya watu wa IS na atakuwa anatumiwa na CIA katika kuratibu na kuchochea hizi vurugu zinazoendelea.Imekuwa vyema wamenielekeza sehemu husika

kwani huyo jamaa ndiye wa kuanza naye” akawaza Mathew

****

Mathew alitikiswa bega na kustuka,alikuwa amepitiwa na usingizi.Saa yake ya mkononi ilionyesha ni saa tisa za usiku.

“Abu Zalawi muda wa kuondoka, mwenyeji wako tayari amefika” akasema Yule mwanajeshi aliyempokea Mathew kisha akamuongoza wakaenda hadi nje ya uwanja ambako kulikuwa na magari matatu.Katika gari la kati kati

kulikuwa na watu wanne wenye silaha wakiwa wamesimama wamelizunguka.Mmoja wa wale jamaa akamfungulia Mathew mlango akaingia ndani ambako alimkuta jamaa mmoja

“Abu Zalawi” akasema Yule jamaa

“Assad Ismail? Akauliza Mathew

“Farhad Seif” akasema Yule jamaa na Mathew akaonyesha wasiwasi

“Yuko wapi Assad Ismail? Akauliza

“Usihofu tafadhali.Karibu Dar es salaam” akasema Yule jamaa na gari likawashwa msafara ule wa magari ukaondoka katika uwanja wa uhuru ukitanguliwa na gari la jeshi la Marekani ambalo lilikuwa na mwanajeshi akiwa amejitokeza nje akiwa na bunduki kubwa tayari kukabiliana na makundi yoyote ya vurugu.

“Vipi safari yako? Akauliza Farhad

“Ilikuwa nzuri” akajibu Mathew na safari ikaendelea kimya kimya.

Walikatisha mitaa mbalimbali ya jiji huku wakikutana na magari ya doria ya polisi na jeshi hadi walipofika katika kituo cha basi cha Botha.Mahala hapa panaitwa jina hilo kutokana na awali mzungu mmoja kutoka Afrika Kusini aliyejulikana kwa jina moja tu la Botha kuishi eneo hilo na kujenga shule ya awali kwa watoto wadogo pamoja na kutoa huduma ya maji bure kwa wananchi waliokuwa wanamzunguka hivyo akawa maarufu.

Magari yalisimama na Farhad akashuka akaenda kuzungumza na wale wanajeshi wa Marekani akaagana nao wakageuza gari wakaondoka.Farhad na wenzake nao wakaendelea na safari yao

“Mbona wale wanajeshi wamerudi? Huko tuendako ni salama?akauliza Mathew

“Una hofu yoyote? Akauliza Farhad

“Wakati tukielekea katika kambi ya wanajeshi tumekutana na makundi makubwa ya vijana wakiwa na

silaha kwa bahati nzuri wanajeshi walikuwa na silaha kali wakawatawanya” akasema Mathew

“Usihofu Abu Zalawi uko salama.Hili ni eneo letu” akasema Farhad na safari ikaendelea kimya kimya huku eneo hili la kwa Botha likiwa kimya sana.Geti jeusi lilifunguliwa na gari zile zikaingia.Ndani kulikuwa na nyumba iliyopakwa rangi ya bluu halafu kukawa na majengo mawili yaliyoonekana kama mabohari.Mathew akaelekezwa kushuka garini

kisha akamfuata Farhad wakaelekea ndani ya ile nyumba.Kulikuwa na mlinzi mlangoni akawafungulia mlango wakaingia ndani.Sebuleni kulikuwa na watu wawili wamekaa chini katika zuria wakizungumza.

“Karibuni sana” akasema mmoja wa wale jamaa kwa lugha ya kiarabu.Mathew na Farhad wakaketi

“Pole na safari ndefu” akasema Yule jamaa aliyewakaribisha

“Ahsante sana nashukuru” akajibu Mathew

“Naitwa Marwan Hossam” akasema Yule jamaa

“Yuko wapi Assad Ismail?akauliza Mathew

“Usiwe na hofu utaonana na Assad kutakapopambazuka lakini kwa sasa unatakiwa upumzike kwa safari hii ndefu” akasema Marwan na kuinuka akampeleka Mathew katika mojawapo ya chumba akamtaka apumzike.

“Hii nyumba ndimo wanamoishi magaidi wa IS ambao jukumu lao kubwa ni kuendelea kuchochea machafuko.Mpaka sasa

wanaamini mimi ni gaidi mwenzao na kesho nitaonana na huyo Marwan mkubwa wao naamini atanieleza mengi” akawaza Mathew huku akikikagua kile chumba

“Wakati nikiendelea kuwasoma hawa jamaa natakiwa kutafuta namna nitakavyoweza kuwasiliana na akina Gosu Gosu ili niweze kuwapa taarifa za jambo hili linaloendelea.Sina hakika kama wanafahamu chanzo cha vurugu hizi.Haya yote lazima yafanyike kesho” akawaza Mathew na kujilaza kitandani

“Mathew hakikisha unafanikisha malengo yako.Ifanye dunia ikukumbuke kwa vizazi na vizazi.Maliza kundi la kigaidi la IS na makundi mengine.Kisafishe kikundi hiki kidogo cha watu hawa ambacho ndicho kinachohatarisha amani ya dunia.Hii ni misheni kubwa na ya hatari.Lolote linaweza kutokea katika misheni hii mimi ninakuombea uimalize salama na kila pale nitakapokuwa na uwezo wa kukusaidia nitafanya

hivyo.Jambo la mwisho baada ya kumaliza misheni hii kama utakuwa salama tafadhali usirejee tena Riyadh.Nenda nyumbani kaendelee na maisha yako.Kaungane tena na familia yako kwani lengo lako litakuwa limetimia kuhusu kupambana na ugaidi.Kuhusu Najma usiwe na hofu nitazungumza naye na ataelewa.Narudia tena usirejee Saudi Arabia kwani hadi wakati huo sintakuwepo tena" Mathew akiwa amejilaza

kitandani akayakumbuka maneno ya Habiba Jawad

“Habiba hana uhakika kama nitamaliza salama operesheni hii ndiyo maana akaniambia kwamba ile ilikuwa ni mara yetu ya mwisho kuonana.Habiba amekuwa akiniambia kwamba atakufa hivi karibuni lakini hakuwahi kunieleza nini hasa kinachomsumbua ingawa ukimtazama huwezi kugundua chochote kama afya yake ina matatizo.Ninamuomba Mungu aniwezeshe niikamilishe salama operesheni hii na

lazima nirejee Riyadh kumuona Najma na pili kujua maendeleo ya Habiba na kama atakuwa amefariki basi nitapenda kuliona kaburi lake kwani mama Yule anastahili pongezi kwa mambo ambayo amenifanyia.Yeye ndiye aliyenifikisha hapa nilipofika hadi nikafahamu mambo mengi na mengine makubwa kabisa ambayo wengi duniani hawayajui" akawaza Mathew halafu akazima taa na kusimama mlangoni akatega sikio kama kuna mtu yeyote yuko mlangoni alipohakikisha

kuko shwari akaenda dirishani na kulichunguza kama ni dirisha analoweza kupita lakini ilikuwa ni dirisha imara ambalo halikuwa na uwazi kwa mtu kupita.

“Ngoja nipumzishe kichwa na kesho nitajua nini cha kufanya” akawaza Mathew na kupanda kitandani

****

Kumepambazuka na kijua tayari kimeanza kuchomoza.Asubuhi hii Tanzania iliamshwa na taarifa

mbaya za kifo cha Mufti wa Tanzania ambaye aliuawa usiku yeye na familia yake baada ya nyumba yake kushambuliwa kwa mabomu.Ilikuwa ni taarifa iliyostua wengi na kuleta hofu kubwa.

Kitasa cha mlango wa chumba cha Mathew kikaminywa kwa nguvu lakini alikuwa amefunga mlango kwa ndani.Mtu aliyeminya kile kitasa akagonga mlango kwa nguvu na Mathew akainuka na kwenda kufungua.Alikuwa ni Marwan

“Habari yako Abu Zalawi?akauliza Marwan

“Habari nzuri Marwan”

“Amka kumekucha.Jiandae kwa ajili ya kuianza siku” akasema Marwan na kumuelekeza Mathew bafu akaenda kuoga halafu akakaribishwa sebuleni kwa ajili ya kupata kifungua kinywa.Mle sebuleni kulikuwa na watu zaidi ya kumi wote wakipata kifungua kinywa.Mathew akawasalimu kisha naye akaketi na kupata chai.Baada ya kupata kifungua kinywa wale watu karibu wote

wakatoka na kwenda katika zile nyumba mbili zilizojengwa kwa mfano wa bohari Mathew akabaki na Marwan

“Yuko wapi Assad ?Mathew akauliza

“Usihofu Abu Zalawi utaonana naye.Atafika hapa muda si mrefu”

“Haishi hapa?

“Hapana yeye haishi hapa”

“Nimeona kuna watu wengi hapa,shughuli gani inafanyika katika nyumba hii?akauliza Mathew

“Abu Zalawi unaonekana unataka kufahamu mambo

mengi kwa wakati mmoja.Jielekeze katika kile kilichokuleta hapa na kama kuna swali lolote unataka kuuliza utamuuliza Assad atakapofika” akasema Marwan na kutoka akamuacha Mathew peke yake mle sebuleni.Mathew akasimama na kuchungulia nje akaanza kuyasoma mazingira ya mahala pale

“Inaonekana hii ni sehemu ambako wanapanga mikakati yao ya kigaidi.Katika yale majengo mawili mfano wa bohari kuna nini? Ngoja

nimsubiri Assad anaweza akanieleza kila kitu kuhusiana na mahala hapa” akawaza Mathew na kuendelea kuangaza angaza macho.

Geti lilifunguliwa na gari la jeshi la Marekani likaingia huku nyuma yake kukiwa na gari lingine lenye rangi nyeusi.Kutoka katika lile gari jeusi wakashuka watu wawili na mmoja wao akaufungua mlango wa kati kati na jamaa mmoja aliyevaa kanzu ya kijivu na koti jeusi akashuka.Kichwani hakuwa amevaa kofia na kichwa chake

hakikuwa na nywele hata moja.Macho yake aliyafunika kwa miwani myeusi.Mkononi alikuwa ameshika sigara akivuta.Akaagana na wanajeshi wale wa Marekani wakaondoka.Jamaa Yule aliyeshuka garini akasalimiana na Marwan wakazunguma kwa dakika chache halafu wakaelekea katika zile nyumba mbili mfano wa bohari.Mathew alikuwa dirishani akiwatazama.

Baada ya dakika kumi wakatoka katika zile nyumba

na kuingia sebuleni,Mathew akasimama

“Abu Zalawi ! akasema Yule jamaa aliyeongozana na Marwan huku akimpa mkono Mathew wakasalimiana

“Nasikia umekuwa unaniulizia sana ukitaka kuniona.Ndiye mimi Assad Ismail.Karibu sana Tanzania” akasema Assad

“Nashukuru sana Assad” akajibu Mathew

“Hii sura yako si ngeni.Umewahi kutembelea nchi yoyote ya Afrika Mashariki?akauliza Assad

“Ndiyo niliwahi kwenda Kenya.Nilikwenda kumuua mkurugenzi wa Mossad katika ukanda wa Afrika Mashariki”

“Ndiyo maana nilipokuona tu nikahisi kama nimewahi kukuona sehemu Fulani.Umewahi kufika Tanzania?

“Hapana ni mara ya kwanza ninafika Tanzania”

Mathew akajibu

“Karibu sana Abu Zalawi.Nimefurahi kukutana nawe.Nimeelezwa kwamba Habiba

Jawad ndiye aliyekupendekeza uje huku” akasema Assad huku akiendelea kuvuta sigara

“Ndiyo ni Habiba ambaye alinipeleka Marekani na kunikutanisha na CIA ambao wamenituma huku”

“Vizuri sana.Vipi maendeleo ya Habiba?

“Habiba anaendelea vizuri sana”

“Nafurahi kusikia hivyo.Hebu nipe historia yako kwa ufupi namna ulivyokutana na Habiba hadi akakuamini kiasi hiki” akasema Assad

“Baada ya kumuua mkuu wa Mossad kanda ya Afrika Mashariki na kati nilikamatwa na Mossad nikafungwa gerezani kwa miaka mitatu na hapo ndipo nilipokutana na Ammar Nazari kiongozi wa kundi la Ammar Nazari Brigades.Nilifanikiwa kutoroka gerezani nikiwa na Ammar na nikajiunga katika kundi lake.Nikiwa katika kundi hilo nilitekeleza mashambulio kadhaa likiwemo lile la kituo cha mabasi jijini Jeruslaem.Vikosi vya Israel vilishambulia makazi ya

Ammar na kufanikiwa kumuua mimi nilitoroka nikiwa na Nawal mke wa Ammar na huyo ndiye aliyenielekeza kwamba tumtafute Habiba Jawad kwa ajili ya kupata hifadhi kwani alikuwa ni rafiki wa Ammar.Tulifanikiwa kuonana na Habiba Jawad akatupa hifadhi na ndipo alipoanza kunishirikisha katika shughuli zake akatokea kuniamini baada ya kuridhiswa na utendaji wangu wa kazi.Hiyo ndiyo historia fupi ya namna nilivyoweza kukutana na

Habiba Jawad” akasema Mathew

“Abu Zalawi mimi naitwa Assad Ismail.Ninasimamia kundi la IS kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki na kati makazi yangu ni Mombasa.Nimekuja Tanzania kwa ajili ya operesheni maalum.Nadhani ulipokwenda Marekani umefahamishwa kile kinachoendelea hapa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla”

“Ndiyo.Nilielezwa kwa kifupi sana na kuambiwa kwamba nitapata maelezo

kamili nitakapofika hapa.Hata maelekezo yote kuhusiana na kazi ninayokuja kuifanya hapa Tanzania nimeambiwa kwamba nitayapata kutoka kwako” akasema Mathew na Assad akaonyesha kushangaa

“Hawakukueleza unakuja kufanya nini Tanzania? Akauliza Assad

“Wamenieleza kwamba ninakuja kulipua ubalozi wa Marekani lakini kila kitu kuhusiana na misheni hiyo nimeambiwa kwamba nitapata kutoka kwako” akasema Mathew

“Nitakueleza kwa kifupi ili uweze kupata picha ya kile kinachoendelea hapa Tanzania.Ni kwamba Marekani wana mipango yao hapa Afrika Mashariki na ili iweze kufanikiwa wamelazimika kututumia sisi kwa malipo ya fedha na silaha.Kumekuwa na upungufu mkubwa wa mafuta duniani kutokana na wazalishaji kupunguza kiwango kwa lengo la kupandisha bei katika soko la dunia.Sababu hiyo ndiyo iliyopelekea Marekani kugeukia Afrika Mashariki

ambako kuna rasilimali ya mafuta kutoka Uganda nchi ambayo ina akiba kubwa sana ya mafuta ambayo husafirishwa kwa bomba kutoka Hoima hadi jijini Tanga hapa Tanzania.Ili kuweza kuyapata mafuta hayo ililazimu kuliingiza eneo la Afrika Mashariki katika machafuko na machafuko ambayo yanaweza kusambaa kwa haraka mama moto wa petroli ni machafuko ya kidini.Katika nchi hizi tatu Tanzania,Kenya na Uganda dini kubwa ni mbili wakristu

na waislamu hivyo kwa kushirikiana na baadhi ya wanasiasa na baadhi ya viongozi wa dini tuliweza kufanya mauaji ambayo yalileta uhasama mkubwa na waumini wa dini hizo mbili wakaanza kushambuliana wakichomeana nyumba za ibada na hata kuuana.Machafuko hayo yalianza Uganda na kuenea Tanzania na Kenya lakini sana tumelenga nchi za Tanzania na Uganda kwani ili Marekani waweze kupata mafuta ya Uganda lazima watumie

bandari ya Tanga hivyo lazima nchi hizi mbili ziingie katika machafuko.Hicho ndicho ambacho tumekuwa tunakifanya hapa Tanzania na ndiyo maana nimeondoka Mombasa kuja hapa Tanzania kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri kwani misheni hii ni ya fedha nyingi sana" akasema Assad

"Hongera sana Assad kwa kazi kubwa uliyoifanya.Nchi kama Tanzania ni nchi ngumu sana kwa watu wake kuingia katika machafuko makubwa

kama haya yanayoendelea” akasema Mathew

“Ni kweli.Haikuwa rahisi.Ililazimu kushirikiana na wanasiasa na baadhi ya viongozi wa dini kutengeneza mtandao wa kuchochea vurugu ndipo tukafanikiwa na kwa mara ya kwanza Tanzania imeingia katika machafuko ya wenyewe kwa wenyewe.Hata hivyo watanzania hawajazoea vurugu kwani kulianza kujitokeza dalili za amani kurejea.Rais wa Tanzani alikutana na mufti wa Tanzania wakawa na

mazungumzo marefu na baada ya mazungumzo hayo mufti akazungumza na waislamu na kuwataka wasijihusishe na vurugu.Kwa kiasi kikubwa watu wameonekana kumuelewa na vurugu zimeripotiwa kupungua sana kwa usiku wa kuamkia leo.Kwa siku ya leo Rais alipanga kuendelea na mikutano na viongozi wengine wa dini ya kikristu.Kwa kiasi kikubwa juhudi za kutafuta amani zinaonekana kuanza kuzaa madini na kazi yetu ni kuhakikisha kwamba amani

haipatikani Tanzania ili vikosi vya Marekani viendelee kukaa Afrika Mashariki kwa muda mrefu zaidi na ili kuvuruga jitihada za kutafuta amani ambazo zimeanza kuonekana usiku wa leo tumemuua mufti wa Tanzania kwa bomu" akasema Assad na Mathew akahisi mwili unamsisimka akajikaza asiweze kuonyesha namna alivyostuka.

"Hii haiwezi kujenga taswira kama kuna kikundi cha watu ambacho kinalenga viongozi wa dini?Unadhani waislamu wataamini kwamba

ni wakristu ndio waliomuua kiongozi wao? Akauliza Mathew

“Usiwe na hofu Abu Zalawi.Tumekwisha jipanga vizuri na kila kitu kitakwenda vizuri.Kwa hili tulilolifanya ni kama kumwagia petrol katika moto ambao umeanza kuzimika na moto ukapata nguvu mpya.Tunao watu wetu ndani ya wakristu na waislamu pia ambao huchochea vurugu hizi.Kwa mfano kwa mauaji haya ya Mufti wapo watu ndani ya uislamu ambao

watawachochea waislamu kulipiza kisasi” akasema Assad

“Tuachane na hilo nataka kufahamu kuhusiana na kazi yangu niliyokuja kuifanya” akasema Mathew

“Ulichokuja kukifanya huku Tanzania kama ulivyoelezwa ni kulipua ubalozi wa Marekani hapa Tanzania.Tayari maandalizi ya bomu litakalotumika yameanza.Litakuwa ni bomu kubwa ambalo litasababisha uharibifu mkubwa sana.Kuna raia wa Marekani ndani ya ubalozi huo pamoja na raia wa

nchi nyingine waliojihifadhi hapo wakisubiri vurugu zipungue na wengi watapoteza maisha kufuatia shambulio hilo litaipa sababu Marekani kuongeza vikosi zaidi Tanzania" akasema Assad na kunyamaza baada ya watu wawili kuingia mle ndani wakazungumza na walipotoka Assad akaendelea.

"Hawa jamaa waliotoka ni wataalamu wanao unda bomu utakalolitumia kulipua ubalozi huo wa Marekani" akasema Assad

“Kwa sasa ubalozi wa Marekani unalindwa na wanajeshi wao walioko hapa nchini.Mpango wa namna utakavyoingia katika ubalozi huo uko namna hii.Kwanza kabisa naomba ufahamu kuwa suala hili linawahusisha pia baadhi ya viongozi wa vikosi vya jeshi vilivyoko hapa Tanzania na kama ulivyoona wewe mwenyewe wamekuwa wakinipa msaada mkubwa.Kutokana na ushirikiano huo tutatumia gari la jeshi la Marekani kuweka bomu kisha utavaa sare za

jeshi hilo na kuonekana kama mwenzao.Wanajeshi watakaokuwa na gari hilo watadai kwamba walitekwa na gari lao kuporwa” Assad akanyamaza

“Wanajeshi watakaokuwa wakilinda ubalozi huo wakiliona gari la jeshi la Marekani hawatakuwa na wasi wasi na wataamini ni mwenzao.Watakuruhusu kuingia ndani kisha utakwenda kuliegesha gari hio mahala utakapoelekezwa.Ndani ya gari hilo utakuwa umebeba watoto ambao utadai kuwa

umewaokota njiani wakiwa hawana msaada.Ukisha egesha gari mahala utakapoelekezwa utashuka na kuondoka hapo ubalozini ukidai kwamba unawafuata watoto uliowaona wako katika hatari.Endapo watakuzuia unaruhusiwa kutumia silaha kuwamaliza walinzi hao.Ukisha toka ubalozini hapo utaelekezwa mahala ambako utakuta gari linakusubiri na hapo ndipo utakapolipua bomu na usiku huo huo utaondoka kuelekea nchini Kenya na siku itakayofuata utakamatwa na

makachero wa CIA na baada ya hapo sisi tutakuwa tumekamilisha jukumu letu kwa upande wako na tutaendelea na jukumu letu la kuchochea machafuko” akasema Assad

“Nimekuelewa Assad.Ahsante kwa mpango huu mzuri.Lini jambo hili litafanyika?Mathew akauliza

“Kwa sasa tunaendelea na utengenezaji wa bomu ambalo tutalitumia.Naamini hadi usiku wa leo litakuwa limekamilika kwani kuna vifaa vichache ambavyo tulikuwa

tunavisubiri na tayari tumevipata hivyo basi naamini hadi usiku wa leo wataalamu wetu wanaounda bomu hilo watakuwa wamekamilisha kazi.Kesho jioni tukio hilo litafanyika” akasema Assad

“Kuna muda mrefu hadi kesho jioni.Hakuna chochote ninachoweza kusaidia kufanya?akauliza Mathew

“Pumzika Abu kwani una safari ndefu sana.Una siku mbili tu leo na kesho za kupumzika kwani baada ya hapo utakabiliwa na kipindi

kigumu sana” akasema Assad

“Nalifahamu hilo Assad lakini mimi ni mtu wa kazi.Sijazoea kukaa bila kuwa na kazi yoyote.Nielekeze kama kuna kazi yoyote ninaweza kusaidia” akasema Mathew

“Abu Zalawi usihofu.Kila kitu hapa kinakwenda vizuri wewe tutakuomba upumzike hadi hiyo kesho jioni utakapoianza safari yako.Una kazi ngumu mno inakukabli mbele yako hivyo tumia muda huu kupumzika.Ninaomba nikakutambulishe kwa watu

wangu wakufahamu kwani wengine wanakuona hapa lakini hawakuelewi wewe ni nani” akasema Assad na kumchukua Mathew wakaenda katika moja ya nyumba iliyojengwa kama bohari.Ndani ya nyumba ile kulikuwa na nafasi kubwa na kati kati ya nyumba ile kulikuwa na meza kubwa iliyokuwa imezungukwa na watu zaidi ya kumi.Shughuli ya uundaji wa bomu ilikuwa inaendelea.Assad akawaomba wamsikilize kwa dakika chache

“Awali ya yote napenda kwanza niwashukuru kwa kazi nzuri iliyofanyika usiku wa leo ya kumuondoa Mufti wa Tanzania.Baada ya kutekeleza shambulio lile naamini sasa zile vurugu ambazo zilikuwa na mwelekeo wa kumalizika zitaanza upya.Jambo la pili ambalo nataka kuwajulisheni ni kwamba jana tumepokea mgeni hapa katika kambi yetu.Nadhani tayari nyote mmekwisha muona anaitwa Abu Zalawi.Anatokea Saudi Arabia.Alikuwa katika kundi la Ammar Nazari

Brigades.Amekuja hapa kwa kazi maalum ambayo ni kulitumia bomu hilo mnaloliandaa.Nimeona nimtambulishe kwenu ili mfahamu kwamba kazi hiyo inatakiwa imalizike kwa haraka ili kesho Abu Zalawi aifanye kazi iliyomleta hapa” akasema Assad na kumtaka Abu Zalawi kwenda kupumzika wakati shughuli ya uundaji wa bomu ikiendelea.Mathew akatoka na kuanza kuzunguka zunguka katika nyumba ile akiyasoma mazingira yalivyo

****

Inakaribia dakika arobaini sasa,Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Dr Fabian Kelelo akizungumza na Ruby kwa simu.Taarifa ya mauaji ya Mufti wa Tanzania ilimstua sana.Baada ya kumaliza kuzungumza na Rais simuni,Ruby akamgeukia Gosu Gosu

“Rais amechanganyikiwa kwa mauaji haya ya Mufti ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kutafuta

amani.Mauaji haya yameleta wasi wasi mkubwa sana wa kuongezeka kwa vurugu.Tuliamini muda si mrefu hali itakuwa shwari lakini kwa mauaji haya kuna uwezekano wa vurugu kuanza upya” akasema Ruby

“Swali la kujiuliza je ni watu wa imani nyingine ndio waliotekeleza mauaji hayo ya Mufti?Binafsi siamini kama ni watu wa imani ya kikritu ndio waliofanya mauaji haya” akasema Gosu Gosu

“Nakubaliana nawe Gosu Gosu mauaji haya ya Mufti wa

Tanzania hayaonekani kama yana mlengo wa kidini bali yanaonekana ni kutaka kuchochea zaidi vurugu ili waislamu waamini kuwa ni upande mwingine ndio waliotekeleza mauaji hayo na hapo waumini wa dini hizo wataendelea kushambuliana.Mauaji haya yametokea wakati kukiwa na kila dalili za machafuko kutulia.Rais alikuwa na program ya kuendelea kukutana na viongozi wakuu wa dini na alianza na mufti wakakutana wakazungumza na

Mufti akawasihi waislamu asiendelee na vurugu zile.Leo hii Rais alikuwa na mipango ya kukutana na viongozi wengine wa dini katika mwendelezo ule wa kutafuta amani lakini kwa hiki kilichotokea sina hakika kama mazungumzo hayo yataendelea tena kwani viongozi wakuu wa dini wataogopa kuzungumza na Rais kwa hofu ya kuuawa kama ilivyomtokea Mufti wa Tanzania.Hali inazidi kuwa tete” akasema Ruby

“Tunahitaji kuongeza juhudi za kuutafuta mzizi wa

vurugu hizi.Tukifanikiwa kuupata mzizi wake tutafahamu mengi.Tulimuomba Rais atusadie kupata taarifa za Joshua Lulangwa wa Uganda.Kuna chochote amekueleza?akauliza Gosu Gosu

“Ndiyo.Amesema kwamba taarifa alizopewa kutoka Uganda ni kuwa Joshua Lulangwa ametoweka na hajulikani alipo.Wanasema mara ya mwisho kuonekana nchini Uganda ni siku ambayo machafuko yalianza jijini

Kampala.Baada ya hapo hajaonekana tena na wala hajulikani alipo na toka wakati huo simu yake imezimwa” akasema Ruby

“Yale yale tuliyoyakuta kwa Karim na wenzake.Ruby ninahisi huu ni mtandao mmoja.Wote wana sifa zinazofanana.Wote simu zao zimezimwa mara tu machafuko yalipoanza na wote hawajulikani walipo.Swali ambalo bado hatujalipatia majibu ni je wanahusika kwa namna yoyote ile na vurugu

hizi zinazoendelea Tanzania na Uganda?akauliza Gosu Gosu

“Hapo ndipo tulipokwama Gosu Gosu.Tunatakiwa kutafuta kila namna ya kuweza kujikwamua hapo tulipokwama.Nina uhakika mkubwa sana kwamba kuna kitu hapa ambacho kama tukiweza kukifahamu basi kinaweza kutusaidia sana kujua mzizi wa vurugu hizi zinazoendelea”akasema Ruby

“Hapa ndipo ninapomkumbuka Mathew” akasema Gosu Gosu

“Me too.I miss him so much ! akasema Ruby na kuinamisha kichwa akazama mawazoni

“Mimi ni mwanajeshi nimefundishwa kupigana na kuua,sina utaalamu mkubwa katika mambo ya kipelelezi.Ninachofahamu mimi ni kushika silaha na kupambana.Wewe ni mchawi wa kompyuta na hujabobea sana katika mambo haya ya kiuchunguzi ndiyo maana kuna mambo tunashindwa kuyapatia majibu kama hili

linaloendelea sasa” akasema Gosu Gosu

“Uko sahihi Gosu Gosu.Mimi utaalamu wangu ni katika msauala ya kompyuta na mawasiliano.Masuala ya kipelelezi sijabobea huko japo nimefanya kazi katika taasisi za kipelelezi lakini nikiwa kama mtaalamu wa kompyuta.Lazima nikiri kwamba idara hii ya SNSA japo imekua ikifanya kazi zake vizuri na kwa mafanikio makubwa lakini hakuna mpelelezi mwenye kiwango cha juu ambaye anaweza

akakaribiana na Mathew Mulumbi” akasema Ruby

“Ruby hakuna ubishi kwamba tunahitaji sana msaada kwa hapa tulipofika na msaada pekee ambao tunauhitaji kuupata hivi sasa ni Mathew Mulumbi” akasema Gosu Gosu na ukimya ukapita halafu Gosu Gosu akasema

“Ruby tunafahamu mahala alipo Mathew na unazo namba za simu za mtu ambaye anaweza akatusaidia kutuunganisha naye.Mpigie muombe atuunganishe na Mathew tuzungumze naye

tumueleze hali halisi ilivyo kwa sasa hapa nchini.Ruby nina uhakika mkubwa Mathew akifahamu kile kinachoendelea hapa nchini hivi sasa lazima atakuja" akasema Gosu Gosu na Ruby akafikiri kidogo na kusema

"Gosu Gosu unachokisema ni cha kweli.Ngoja nimpigie Yule mwanamke aliyenipigia akajitambulisha kuwa ni mke wake" akasema Ruby na kuchukua simu yake akazitafuta namba za Najma akapiga lakini simu yake haikupatikana.Akapiga mara

ya pili jibu likawa lile lile simu ya Najma haikuwa ikipatikana

“Simu yake haipatikani.Nitajaribu tena baadae” akasema Ruby

“Tumekwama tena” akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu hatupaswi kushindwa.Machafuko yanakwenda kuanza upya na inaonekana wazi kwamba upo mtandao ambao unachochea machafuko hayo.Lazima kwa namna yoyote ile tuufahamu mtandao huo.Kwa sasa tuendelee kufuatilia hali ya vurugu inavyondelea jijini Dar

es salaam huku tukiendelea kuchimbua zaidi kuhusu hawa jamaa waliotoweka.Nina uhakika tunaweza kupata kitu Fulani” akasema Ruby

RIYADH – SAUDI ARABIA

Msafara wa watu waliokwenda makaburini kumzika Abu Dahir ulirejea katika makazi ya Habiba Jawad.Ilikuwa ni simanzi kubwa na watu wengi walifika kumpa pole Habiba kwa kuwapoteza watoto wawili ndani ya muda mfupi.Kifo cha

Abu Dahir kiliwasikitisha wengi.

Saa moja za jioni Habiba Jawad akaomba akina mama waliokuwa wanamsaidia kumpeleka katika nyumba yake kwani mwili wake haukuwa na nguvu hivyo alihitaji kutegemezwa.Akasaidiwa kunyanyuka kisha akategemezwa kuelekea katika nyumba yake.Aliomba aachwe katika sebule ya chini kabisa halafu akaomba aitiwe Nawal mjane wa Abu Dahir ambaye aliletwa kisha akawataka wale

akina mama wawaache wapumzike.Habiba akamtaka Nawal amsaidie wakaingia katika lifti kwani hakuwa na nguvu za kupanda ngazi.Waliingia katika sebule maalum ya Habiba akamuomba mtumishi wake amtengenezee kahawa ambayo ililetwa ndani ya muda mfupi.Habiba akanywa kidogo na kumtazama Nawal aliyekuwa ameinamisha kichwa huku machozi yakiendelea kumtoka

“Pole sana Nawal najua umeumia kwa kifo cha Abu

Dahir” akasema Habiba.Nawal akafuta machozi halafu akasema

“Mama mimi ndiye ninayepaswa kukupa pole.Unapitia kipindi kigumu sana mama yangu.Umewapoteza watoto wawili ndani ya kipindi kifupi.Hakuna ajuaye ni maumivu kiasi gani unayoyapitia hivi sasa na mimi ni mmoja wa waliochangia kukusababishia maumivu haya makubwa.Nisamehe sana mama sikukusudia kumuua

Abu Dahir.Imetokea bahati mbaya tu” akasema Nawal

“Nawal nimekwisha kwambia na ninarudia tena kukwambia kwamba katu usihisi hatia katika jambo hili.Halikuwa kusudio lako na ulikuwa unaniokoa mimi.Kama usingekipiga kile chungu kingenipata na yawezekana mimi ndie ambaye ningepoteza maisha badala yake.Siwezi kukulaumu badala yake ninapaswa kukushukuru.Haya yanayonitokea ni adhabu kufuatia mambo mabaya

niliyoyafanya.Watu wengi wamekufa kwa sababu yangu.Ninamini Mungu ananiadhibu na ninastahili adhabu hii.Nawal hakuna chochote kizuri nilichokipata kwa haya yote niliyoyafanya zaidi ya kuchuma dhambi.Awali waliponifuata wakaniambia wanataka kunitumia kufadhili makundi ya wanamgambo walinidanganya kwamba ni kwa ajili ya kulipiza kisasi kwa kifo cha mume wangu ambaye niliamini aliuawa na vikosi vya Israel kumbe aliuawa na

Marekani.Pamoja na kumwaga damu ya watu wengi lakini mume wangu hajarudi na sijapata amani niliyotegemea kuipata kwa kulipiza kisasi.Baadae nilikuja kugundua kwamba ni Marekani ndio waliomuua mume wangu na toka hapo nikawa na hasira sana nao na nikaanza kutafuta namna ya kulipiza kisasi hadi mlipojitokeza ninyi" akasema Habiba na kunyamaza

"Mama kuna kitu nataka kukwambia" akasema Nawal

"Sema usohofu Nawal"

“Baada ya haya yote yaliyotokea sidhani kama nitakuwa na amani kama nitaendelea kuishi hapa.Nimetafakari sana nimeamua kurejea nyumbani Marekani” akasema Nawal na Habiba aliendelea kukaa kimya akitafakari halafu akasema

“Nawal hapa ni nyumbani kwako.Wewe na Mathew ni watoto ambao nimebaki nao hivyo huna sababu ya kurejea nyumbani” akasema Habiba

“Mama Habiba nafahamu namna unavyotupenda mimi

na Mathew Mulumbi lakini utanisamehe kwa maamuzi haya.Naomba uniruhusu niende nyumbani” akasema Nawal

“Nawal bado ninakuhitaji sana” akasema Habiba

“Nafahamu mama lakini naomba uniruhusu niende nyumbani.Sintakuwa na amani hapa.Niache nikatulize akili na pale nitakapokuwa sawa nitarejea” akasema Nawal

“Nawal najua uko katika wakati mgumu kufuatia kifo cha Abu Dahir lakini nakuhitaji kwa ajili ya misheni

muhimu sana” akasema Habiba

“Misheni ipi mama?akauliza Nawal

“Halafu hujanieleza alipo Mathew.Yuko salama?akauliza tena Nawal

“Nilitaka kukueleza kuhusu Mathew lakini likatokea lile tatizo na kila kitu kikavurugika” akasema Habiba na kunyamaza kidogo

“Mathew yuko katika misheni kubwa hivi sasa”

“Misheni ipi mama,unaweza ukanieleza?

“Nilikueleza kwamba Marekani ndio waliomuua mume wangu wa pili ambaye ni baba yake Abu Dahir.Baada ya kulifahamu hilo niliumia sana na nikaanza mipango ya kukisambaratisha kikundi kidogo ndani ya CIA ambacho kimekuwa kinashirikiana na makundi mbali mbali ya kigaidi.Niliwarejesha akina Mathew waliokuwa katika kisiwa cha Fiji kwani nilimuhitaji Mathew kwa ajili ya operesheni hiyo muhimu”

“Ni operesheni ipi hiyo mama? Nawal akauliza

“Nadhani tayari umekwisha sikia kwamba Rais wa Uganda alipinduliwa na jeshi”

“Ndiyo nilisikia taarifa hizo tukiwa jijini Cairo kutazama mapiramidi” akasema Nawal

“Basi mpango ule ulisukwa na hiki kikundi kidogo ndani ya CIA kinachojihusisha na mashirikiano na makundi ya kigaidi.Mpango huu ni kuiwezesha Marekani kupata mafuta ya kutoka nchini Uganda na ili waweze kufikia lengo lao ililazimu kuchochea

vurugu za kidini na ndiyo chanzo cha machafuko makubwa yanayoendelea Afrika mashariki hivi sasa.Wanawatumia kundi la IS katika kuchochea machafuko hayo.Watu wanaendelea kuuana huku Marekani wakifurahia neema ya mafuta.Huu ni unyama mkubwa” akasema Habiba

“Mathew Mulumbi ameenda huko ndiyo maana hakuonekana katika msiba wa Najma? Akauliza Nawal

“Mathew Mulumbi yuko Afrika Mashariki lakini katika misheni tofauti”

“Ni misheni gani imempeleka Mathew huko?akauliza Nawal

“Marekani na Iran ziko katika mgogoro mkubwa hivi sasa na marais wa nchi hizo mbili wamekuwa wakitupiana maneno mazito ya vitisho.Katika mwendelezo huo wa kutoleana vitisho Rais wa Iran ametishia kuanza kuwashambulia washirika wa Marekani na baada ya hapo ataishambulia Marekani na

kuiharibu kabisa.Hilo limewatisha wamarekani na kuwafanya wasimamishe kwanza mipango yao ya kuishambulia kijeshi Iran kwa hofu kwamba yawezekana Iran ikawa inamiliki silaha kama kama inavyojitapa.Ukweli ni kwamba mpaka sasa Marekani bado hawana taarifa za uhakika kuhusiana na silaha ambazo Iran inazimiliki hivyo wameamua kumtumia Mathew Mulumbi katika misheni maalum”

“Wanamtumia Mathew Mulumbi? Nawal akashangaa

“Ndiyo Nawal.Nilitaarifiwa na kiongozi wa idara hiyo ndogo ndani ya CIA na kunitaka nimtafutie gaidi ambaye anafahamu mbinu za kijasusi kwa ajili ya kumtuma Iran kutekeleza kazi maalum.Kwa kuwa tayari nilikwisha kuwa na mipango ya kuimaliza idara hiyo niliamua kumpelekea Mathew Mulumbi.Wamempokea wakampima wakamuamini kuwa anafaa na tayari amekwisha tumwa kwenda kuanza kutekeleza misheni

hiyo ambayo inaanzia nchini Tanzania” akasema Habiba

“Mama hii ni misheni ya hatari sana umemuingiza Mathew.Atawezaje kuingia nchini Iran?Nawal akauliza

“Mipango imeandalia na ndiyo maana amekwenda nchini Tanzania.Kule anakwenda kulipua ubalozi wa Marekani kisha atakamatwa na dunia nzima itajua kwamba Marekani imemkamata gaidi ambaye amelipua ubalozi wake jijini Dar es salaam.Baada ya kumkamata watamuunganisha na wanasayansi wa Iran ambao

walitekwa na Marekani na baadae utatengenezwa mpango ili Mathew aweze kutoroka na wanasayansi hao wa Iran na hiyo itakuwa ni tiketi yake ya kuingia Iran.Kwa hicho alichokifanya kuwakomboa wanasayansi wa Iran atapokelewa kama shujaa na hapo ndipo atakapoanza kuifanya kazi aliyotumwa”

“Mungu wangu ! akasema Nawal

“Ni misheni ya hatari sana hii mama na sina hakika kama Mathew anaweza akafanikiwa.Kwanza jina lake

litachafuka na dunia nzima watamjua kuwa yeye ni gaidi na muuaji.Vipi kuhusu ndugu na familia yake?Unadhani wataumia kiasi gani?Vipi kuhusu nchi yake unadhani watamuamini tena baada ya taarifa kusambaa kwamba ni gaidi na amelipua ubalozi wa Marekani? Mama umeyafanya maisha ya Mathew yawe magumu sana na hata kama akikamilisha misheni hii maisha yake hayatakuwa sawa tena na wewe utakuwa umechangia kwa kiasi kikubwa kuyaharibu" akasema Nawal

“Nawal nafahamu hiki alichokwenda kukifanya Mathew ni kitu cha hatari sana lakini ni lazima aende katika misheni hii ili aweze kumaliza ugaidi duniani.Nimempeleka makusudi ili aweze kufahamu ni nani wanaofadhili makundi mbali mbali ya ugaidi duniani hivyo anatakiwa kuwa karibu nao awasome na kisha awamalize.Dunia nzima haijui kama mzizi wa ugaidi uko katika nchi inayopinga ugaidi kwa nguvu zote.Hili hata wamarekani wenyewe hawalifahamu kama mzizi huu

uko ndani ya nchi yao.Hawajui kama vita ambayo imekuwa ikiendeshwa na nchi yao na kupata ushindi ni kama hadaa kwao na kwa dunia.Watashangaa kujua kwamba mashambulio mbali mbali ambayo yamekuwa yakifanywa na magaidi katika nchi mbali mbali duniani.Ni jukumu la Mathew Mulumbi kuhakikisha kwamba dunia inafahamu kila kitu kuhusiana na hiki kinachofanywa na Marekani kupitia idara hii ndogo ndani ya CIA na ili aweze kuimaliza idara hii

ndogo lazima ashirikiane nao afahamu mambo yao na akusanye ushahidi wa kutosha kisha awamalize na dunia ijue kila kitu” akasema Habiba

“Nafahamu ni misheni ya hatari sana lakini ni lazima Mathew aifanye na kama akiikamilisha salama itakuwa na faida kubwa kwa dunia.Ninamuamini Mathew na kuna sauti ndani mwangu inayoniambia kwamba Mathew ataitekeleza misheni hiyo kama alivyotumwa.Mathew atakuwa salama.Nimejiuliza zaidi ya

mara elfu moja kama nimefanya kitu sahihi kumpeleka Mathew Mulumbi katika misheni hii? Jibu nililolipata ni kwamba nimefanya kitu sahihi.Mathew Mulumbi ni mtu sahihi.Ni kweli jina lake litachafuka baada ya kukamatwa kwa kulipua ubalozi wa Marekani jijini Dar es salaam lakini mwisho wa misheni hii jina lake litaandikwa kwa dhahabu.Dunia nzima itamuheshimu kwa kile atakachokifanya.Nawal umefika wakati wa kuifanya

dunia kuwa sehemu salama ya kuishi lakini ni nchi hizi kubwa ambazo zinafanya dunia isiwe sehemu salama kwa kuchochea machafuko hasa katika nchi za kiafrika na zile ambazo zimebarikiwa utajiri mkubwa” akasema Habiba

“Mama lazima na mimi uniunganishe na misheni hii.Mathew hawezi kuifanya peke yake.Anahitaji mtu wa kumsaidia.Tafadhali mama” akasema Nawal

“Hapana Nawal.Wewe una misheni nyingine ambayo unakwenda kuitekeleza

ambayo nayo ni ya muhimu sana” akasema Habiba

“Misheni ipi hiyo mama?akauliza Nawal

“Meli za Marekani zimepanga foleni jijini Tanga Tanzania zikipakia mafuta yatokayo nchini Uganda.Kumekuwa na dalili za kupatikana kwa amani nchini Tanzania na hii itaathiri kwa kiasi kikubwa uchukuaji wa mafuta kwani amani ikipatikana, Tanzania haitahitaji tena msaada wa vikosi vya Marekani na zoezi la uchukuaji wa mafuta

litakoma.Marekani wanahitaji vikosi vyao kuendelea kuwepo nchini Tanzania na Uganda ili waendelee kuchukua mafuta hivyo basi wamekuja na mpango mwingine ambao utawafanya waongeze vikosi zaidi nchini Tanzania" Habiba akanyamaza

"Hivi sasa wanasayansi wa Marekani wanatengeneza kirusi hatari ambacho kitapelekwa kusambazwa nchini Tanzania.Kirusi hicho ambacho bado hakijajulikana jina lake kinatarajiwa kusababisha maangamizi

makubwa na kupelekea Marekani kuongeza wanajeshi zaidi nchini Tanzania kwa ajili ya kutoa msaada hivyo vikosi vya Marekani kuendelea kukaa muda mrefu Afrika Mashariki.Nataka ukavuruge misheni hiyo” akasema Habiba

“Hiyo ni misheni ya hatari sana mama lakini niko tayari kuifanya kwa ajili ya kuzuia njama ovu za Marekani.Siamini kama nchi yangu imefikia hatua hii ya kutojali utu kwa ajili tu ya kujipatia mafuta.Huu ni ukatili mkubwa sana” akasema Nawal

“Wanaofanya hivi ni kundi la watu wachache sana na hata Rais wa Marekani hafahamu chochote kwani ni kundi linaloendeshwa kwa siri kubwa sana na Rais hapaswi kufahamu” akasema Habiba

“Hata kama ni kundi dogo lakini linaiwakilisha Marekani na endapo ikijulikana dunia haitaelewa kama ni kundi la watu wachache bali watakachofahamu kuwa ni Marekani.Nielekeze mama ni namna gani nitaweza kuzuia mpango huu usifanikiwe? Akauliza Nawal

“Wanataka kutumia mtu kutoka mtandao wa IS kwenda kusambaza kirusi hicho nchini Tanzania.Kesho mtu huyo atakuja hapa kwa ajili ya safari ya kuelekea Marekani kuandaliwa kwa zoezi hilo la kwenda kusambaza kirusi Tanzania.Itakulazimu kwenda nchini Tanzania” akasema Habiba na kumtazama Nawal

“Kuna machafuko makubwa na hadi sasa kiwanja cha ndege kimefungwa lakini ni lazima uende kwani bila kuzuia mpango huo usifanikiwe kirusi hicho

kinaweza kuwa hatari sana kwa dunia”

“Mimi niko tayari kwenda huko Tanzania mama siogopi machafuko.Nataka nikaonane na Mathew” akasema Nawal

“Misheni yako ni tofauti na ya Mathew na hutatakiwa kuonana na Mathew kwani unaweza ukavuruga misheni yake”

“Nani basi atakuwa mwenyeji wangu Tanzania?Sijawahi fika huko na kama ningeweza kuonana na Mathew ambaye yuko huko Tanzania angenisaidia sana”

“Kumpata Mathew ni ngumu kwa sasa lakini kuna mtu ambaye Mathew ana ukaribu naye yuko Tanzania.Tutawasiliana naye ili awe mwenyeji wako.Naamini tukimwambia kwamba wewe ni mtu wa karibu na Mathew lazima atakubali kukupokea” akasema Habiba

“Itakuwa vizuri kama akikubali”

“Ni mtu muhimu kwa Mathew hivyo lazima atakubali.Kesho huyo mtu ambaye atakwenda kusambaza

kirusi hicho Tanzania atafika hapa kabla ya kuelekea Marekani.Baada ya kumfahamu mtu huyo ni nani,utaondoka kuelekea Tanzania na nitaendelea kuwasiliana nawe kukupa taarifa za kila kinachoendelea kuhusianana mpango huo” akasema Habiba na ukimya mfupi ukapita

“Nawal hii ni misheni muhimu sana na haitakiwi kushindwa kwani ukishindwa kuzuia kirusi hicho kusambazwa basi kinaweza kuvuka mipaka ya Tanzania na

kuwa janga la dunia.Najua ni jukumu zito lakini ni lazima kwa namna yoyote ile ulitimize” akasema Habiba

“Mama usiogope nitalitimiza na kuhakikisha mpango huo haufanikiwi.Nifanyie maandalizi na kila kitu kitakapokuwa tayari nijulishe” akasema Nawal.

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Saa mbili za usiku jijini Dar es salaam Mathew na wenzake walimaliza kupata chakula cha usiku kisha haraka haraka masanduku ya silaha yakapakiwa katika magari halafu kila mmoja akashika bunduki yake na kuingia garini.Mathew akatakiwa kwenda chumbani kwake kupumzika.Hakutaka kuwauliza wanakwenda wapi lakini ni wazi kwa namna walivyojiandaa walikuwa

wanakwenda kufanya shambulio sehemu Fulani.Geti likafunguliwa magari yale yakatoka halafu jenereta likazimwa na kukawa giza.Ndani ya bohari dogo ambako shughuli ya uundwaji wa bomu ilikuwa inaendelea walikuwa wanatumia jenereta dogo lisilotoa sauti

Mathew aliingia chumbani kwake akaubamiza mlango ili walinzi wasikie kwamba tayari yuko chumbani

“Lazima nitoke hapa usiku huu nikawasake akina Ruby nijue kama wako salama au

vipi” akawaza Mathew na taratibu akaufungua mlango na kunyata kuelekea katika mlango wa jikoni ambao haukuwa umefungwa,akausukuma na kuingia ndani ya jiko akatulia kusikiliza kama kuna mtu yeyote,kulikuwa na ukimya mkubwa.Jikoni kulikuwa na mlango wa kutokea nje akakiminya kitasa taratibu mlango ukafunguka akatoka nje na kujibanza ukutani kusikiliza lakini hakusikia sauti yoyote zaidi ya sautio za wadudu.Mchana wa siku ile

aliutumia vyema kuyasoma mazingira ya mahala pale hivyo alikwisha fahamu ni wapi atapita.Kutoka pale jikoni akatembea kwa tahadhari hadi katika magari mawili mabovu yaliyokuwa yameegeshwa karibu na ukuta,pembeni ya magari yale kulikuwa na lundo la matofari yamepangwa,akapanda matofari yale na kuushika ukuta.Alijilaza juu ya ukuta na alipohakikisha kuko salama akajirusha nje bila kuoa ukelele.

“Sasa nielekee nyumbani kwangu.Kutoka hapa hadi nyumbani kwangu kuna umbali kidogo lakini nitajitahidi kukimbia na kutumia njia za mkato.Sina silaha yoyote lakini Mungu atanifikisha salama” akawaza Mathew huku akifuata uchochoro uliompeleka hadi barabarani.Mtaa wote ulikuwa kimya kabisa na giza.Ni sauti za mbwa wakibweka ndizo zilisikika.Bila upoteza muda Mathew akaanza kukimbia akielekea katika barabara kubwa

“Mimi si mgeni wa maeneo haya hivyo siwezi kupata taabu wakati wa kurudi” akawaza Mathew akiendelea kukimbia hadi alipoikuta barabara kuu akaanza kuifuata.Mpaka wakati huo hakuwa amekutana na mtu hata mmoja

“Bado mapema sana lakini jiji la Dar es salaam ni tupu,liko kimya wakati jiji hili limezoeleka ni jiji la kukesha.Lazima hili jambo limalizike haraka sana” akawaza Mathew akiendelea kukimbia.

Alikimbia kwa dakika hamsini na mara kwa mbali akashuhudia moto mkubwa na kusikia makelele ya watu.Akaendelea kukimbia kwa tahadhari kubwa hadi alipokaribia eneo lile akakutana na kundi la watu wakifurahia baada ya kulichoma gari.Wengine walikuwa na bunduki.Mathew akaungana nao lakini ghafla zikaanza kusikika risasi za moto na kundi lile likatawanyika.

“Twendeni huku ! akapiga ukelele jamaa mmoja

aliyekuwa na bastora mkononi,Mathew na watu wengine wanne wakaanza kumfuata

“Risasi zile zimetokea wapi?akauliza Mathew wakati wakikimbia

“Wanajeshi wamefika ! akajibu Yule jamaa mwenye bastora huku akihema kwa kasiWalikatisha vichochoro kadhaa na mara mmoja wao akajikwaa katika jiwe akaanguka na kuanza kupiga makelele ya kuvunjika mguu.Mathew akawataka wasubiri,akamuinua Yule

jamaa akamuweka begani akaanza kukimbia naye.Baada ya muda wakajikuta katika njia ya kuelekea bonde la mto Msanzi.Bado Mathew aliendelea kumbeba Yule jamaa mabegani hadi walipofika katika lundo la mchanga wakapumzika.Mathew akamuweka chini Yule jamaa na wote wakaanza kumtazama.Alikuwa amevunjika mguu na vile vile alichomwa na kipande cha chupa tumboni.Hali yake

haikuwa nzuri kwani alipoteza damu nyingi

“Tunamsaidiaje huyu?akauliza Mathew

“Tunasubiri wenzetu waje tujipange tuone namna ya kumsaidia huyu mwenzetu”akasema mmoja wa wale jamaa.

“Hapana hatuwezi kusubiri hadi wenzetu wafike tutampoteza huyu jamaa” akasema Mathew

“Unashauri nini?Mwingine akauliza

“Tumpelekeni hospitali”

“Hospitali?! Huoni hali ilivyokuwa mbaya huko mtaani?

“Mnataka tumuache huyu mwenzetu afie hapa?Mathew akauliza kwa ukali

“Hii si sawa hata kidogo.Hatuwezi kumuacha mwenzetu afe wakati tunao uwezo wa kumsaidia.Lazima tumpeleke hospitali” akasema Mathew

“Hospitali gani tumpeleke?Karibu hospitali zote zimejaa majeruhi”

“Tujaribu hospitali yoyote ile lakini hatuwezi kumuacha

mwenzetu hapa.Kama ninyi hamtaki mimi nitampeleka mwenyewe ! akasema Mathew kisha akamuinua Yule jamaa akaanza kuondoka naye.Wale jamaa wakashauriana halafu wakaamua kuambatana na Mathew wakasaidiana kumbeba Yule jamaa kupandisha kilima hadi walipofika barabarani.Mathew akamuweka begani Yule jamaa na kuanza kutembea haraka haraka wakiwahi hospitali.Wakati wakitembea Mathew akakiona kituo cha mafuta kandoni mwa barabara

“Hiki ni kituo cha mafuta?akauliza huku akimulika kwa tochi ya mmoja wa wale jamaa aliokuwa nao

“Ndiyo ni kituo cha mafuta,kwa nini umeuliza”akauliza mmoja wao

“Kuna gari zimeegeshwa pale.Tunahitaji gari kwani hatuwezi kuokoa maisha ya mwenzetu kama tukiendelea kutembea kwa miguu”

“Hatuwezi kupata gari hapa.Watu wameweka hapa magari yao kisha wakakimbia na funguo zao” akasema Yule jamaa

“Kuna yeyote ana kisu hapa?:akauliza Mathew na mmoja wao akampa kisu kidogo

“Wewe mwenye bastora nifuate” akasema Mathew kisha kwa tahadhari wakaelekea katika kituo kile cha mafuta na kunyata hadi katika magari yaliyokuwa yameegeshwa pale kituoni.Mathew akachagua gari moja lenye rangi nyeusi akakipiga teke kioo cha upande wa dereva kikavunjika akaingiza mkono ndani na kuufungua mlango.Akamtaka

Yule jamaa amulike tochi ya simu ndani ya gari,na kwa kutumia kisu akang'oa sehemu ya funguo kisha akakata nyaya na kuzichuna akazigusanisha na mara gari likawaka.Yule jamaa aliyekuwa naye hakuamini macho yake.Mathew akaliondoa gari wakampakia yule mgonjwa na safari ya kuelekea hospitali ikaanza.

"Umefanyaje hadi gari likawaka?akauliza Yule jamaa aliyekuwa na bastora

"Nina utaalamu kidogo na magari"akajibu Mathew na

kupunguza mwendo wa gari baada ya kukuta mawe makubwa barabarani.Wakashuka na kwenda kuyatoa mawe yale na safari ikaendelea.Walipita barabara kadhaa hadi walipofika katika hospitali ya Mtodora ambako kulikuwa na ulinzi mkali sana.Mathew akawajulisha walinzi kwamba kulikuwa na majeruhi garini na walipomuona haraka haraka wakafungua geti na akina Mathew wakaingia ndani.Haraka haraka majeruhi

Yule akachukuliwa na kwenda kuanza kupatiwa huduma.

“Nini kinafuata?Mathew akawauliza wale jamaa

“Kwa sasa ni kufuatilia kujua kama wenzetu wako salama na tujue tunakutana wapi” akajibu mmoja wa wale jamaa huku akitoa simu akawasiliana na watu kadhaa akawajulisha kwamba wao wako katika hospitali ya Mtodora kuna mwenzao wamempeleka pale ameumia.Alipomaliza kuzungumza Mathew akamfuata na kumuomba simu

yake awasiliane na mtu Fulani na alipompa Mathew akaziandika namba za simu za Ruby

“Nina bahati ubongo wangu una uwezo mkubwa wa kuhifadhi vitu kwani ninazikumbuka namba za simu za Ruby” akawaza Mathew na kupiga simu ikaanza kuita bila kupokelewa.Akapiga tena

“C’mon Ruby pick up ! akawaza Mathew na safari hii simu ikapokelewa.

“Hallow ! ikasema sauti ya upande wa pili ambayo

Mathew aliitambua ni sauti ya Ruby.

“Hallow Ruby ! akasema Mathew

“Nazungumza na nani?Ruby akauliza

“Ni mimi Mathew Mulumbi.Uko salama Ruby?

“Mathew?! Ruby akashangaa

“Ruby tuokoe muda.It’s me Mathew.Uko wapi tafadhali?

“Mathew?!! Ruby akauliza tena

“Sikiliza Ruby nahitaji kuonana nawe usiku huu.Ni

muhimu sana” akasema Mathew

“Wewe ni Mathew yupi?Mathew Mulumbi ninayemfahamu hayupo Tanzania”

“C’mon Ruby It’s me Mathew.Ni mimi mpenzi wako.Niko hapa Tanzania” akasema Mathew na sekunde kadhaa za ukimya zikapita kisha Ruby akauliza

“Uko sehemu gani Mathew?

“Niko hapa hospitali ya Mtodora” akajibu Mathew

“Sawa ninatuma watu waje hapo kukuchukua” akajibu Ruby na kukata simu.

****

Ruby alihisi mwili wote unamtetemeka baada ya kuzungumza na Mathew simuni.

“Huyu niliyeongea naye ni Mathew kweli?Lakini sauti ni yake .Kama kweli ni yeye amekuja lini Tanzania?Mathew mbona ana maajabu namna hii?Alinipigia simu Najma kutoka Saudi

Arabia lakini leo hii Mathew yuko hapa amewezaje kuingia nchini? Akawaza Ruby akiwa amejishika kiuno.

“Nilidhani ninamfahamu Mathew vizuri kumbe bado sana.Itanichukua muda mrefu kidogo kumfahamu huyu ni mtu wa namna gani” akawaza Ruby na kuchukua simu akampigia Gosu Gosu akamtaka aende mara moja ofisini kwake.Gosu Gosu ambaye alikuwa amekwenda katika chumba chake kupumzika akafika mara moja ofisini kwa Ruby

“Kuna nini Ruby?akauliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu nimetoka kuzungumza na Mathew muda mfupi uliopita”

“Umezungumza na Mathew? Akauliza

“Ndiyo nimezungumza naye.Yuko hapa Dar es salaam”

“Mathew yuko Dar es salaam?! Gosu Gosu naye akashangaa

“Ndiyo.Mathew yuko hapa Dar es salaam.Nimezungumza naye akiwa katika hospitali ya Mtodora”

“Is he okay? Akauliza Gosu Gosu

“I don’t know.Hajasema chochote kuhusu anafanya nini hapo hospitali ila amesema kwamba anataka kuonana nami usiku huu ni muhimu sana” akasema Ruby

“Ruby una uhakika mtu uliyezungumza naye simuni ni Mathew Mulumbi? Gosu Gosu akauliza

“Naifahamu sauti yake.Sina shaka ni yeye.Lakini swali ni je amefikaje hapa nchini? Ameingiaje? Ni juzi tu nimepigiwa simu na Yule

mwanamke Najma kutoka Saudi Arabia akisema kwamba Mathew alikuwa ananitafuta halafu leo hii yuko hapa nchini.Haya ni maajabu Gosu Gosu”

“Si maajabu Ruby.Ni kweli kabisa.Huyo ndiye Mathew Mulumbi ambaye haishiwi maajabu”

“Una uhakika ni yeye? akauliza Ruby

“Nina uhakika Ruby.Ninakwenda huko Mtodora kumchukua” akasema Gosu Gosu

“Hapana huwezi kwenda peke yako.Utaongozana na kikosi cha makomando wetu kwenda huko hospitali” akasema Ruby na kumuita ofisini kwake kiongozi wa kikosi kile cha makomando ambaye alifika haraka akamtaka achukue makomandoo wanne waongozane na Gosu Gosu kuelekea hospitali ya Mtodora kumchukua Mathew Mulumbi.

Haraka haraka waliingia katika gari lao maalum lisilopenya risasi wakaondoka kuelekea hospitali ya Mtodora

****

Gosu Gosu na timu ya makomando waliwasili katika hospitali ya Mtodora kisha wakamjulisha Ruby kuwa tayari wamewasili na Ruby akapiga namba ile ya simu ambayo aliitumia Mathew kuwasiliana naye.Simu ikapokelewa na sauti nyingine

“Samahani kaka kuna mtu mmoja ametumia simu hii kuwasiliana nami si muda mrefu sana.Uko naye karibu?Ninaweza kuzungumza

naye?akauliza Ruby akiwa na wasiwasi

“Sawa niko naye hapa karibu” akasema Yule jamaa na kumfuata Mathew akampatia simu

“Kuna mtu anataka kuzungumza nawe” akasema Yule jamaa na kumpa simu Mathew

“Hallo” akasema Mathew

“Mathew kuna watu nimewatuma hapo hospitali waje kukuchukua wakiongozwa na Gosu Gosu,tayari wamekwisha fika wako getini” akasema Ruby

“Ahsante Ruby” akasema Mathew na kukata simu akamfuata Yule jamaa

“Mimi ninaondoka.Hakikisheni mwenzenu amepata nafuu ndipo muondoke hapa hospitali” akasema Mathew ambaye alikuwa amechafuka damu

“Unakwenda wapi? Ni hatari sana huko mitaani” akasema yule jamaa ambaye hadi muda huo hawakuwa wamefahamishana majina yao

“Usijali nitakuwa salama” akasema Mathew na kuanza

kupiga hatua kuondoka halafu akageuka

“By the way gari lile mtalirejesha mahala tulipolichukua.Kingine nawashauri baada ya mwenzenu kupata nafuu rudini nyumbani msiendelee kushiriki katika vurugu hizi ambazo hazina manufaa yoyote kwenu” akasema Mathew na kuondoka zake akaenda getini na mara akasikia akiitwa

“Mathew”

Mathew aliitambua sauti ile akasimama kutazama

ilitoka wapi na mara akamuona mtu mmoja akiwa ameinua mkono akimuelekeza mahala alipo akamfuata

“Gosu Gosu ! akasema Mathew kwa furaha wakakumbatiana

“Mathew siamini kama nimekuona tena kaka yangu ! akasema Gosu Gosu

“Mimi ndiye siamini kama nimefanikiwa kuonana tena Gosu Gosu ukiwa katika hali hii.Vipi maendeleo yako?

“Ni kama unavyoniona.Ninaendelea

vyema kabisa” akasema Gosu Gosu

“Vipi kuhusu Ruby?Naye anaendeleaje?

“Naye vile vile anaendelea vyema kabisa” akasema Gosu Gosu na kumuongoza Mathew kuelekea katika gari ambalo kulikuwa na watu watatu wanne wamesimama nje wakiwa na bunduki .Gosu Gosu akawajulisha watu wale kwamba mtu waliyemfuata pale hospitalini ni Yule aliyeongozana naye.Mathew akawasalimu wale makomando kisha wakaingia

garini na safari ya kuelekea makao makuu ya SNSA ikaanza.

“Tunaelekea wapi?Ruby yuko wapi?akauliza Mathew

“Tunaelekea SNSA pale ndipo tumeweka kambi kwa sasa kufuatia vurugu hizi zinazoendelea” akasema Gosu Gosu

“Nawe pia uko SNSA? Akauliza Mathew

“Ndiyo niko SNSA Ruby aliniomba niwe msaidizi wake.Nilikubali ili kuhakikisha anakuwa salama muda wote kwani kazi anayoifanya ni ya

hatari kubwa” akasema Gosu Gosu

“Ahsante sana Gosu Gosu kwa kuhakikisha Ruby anakuwa salama.Vipi kuhusu Lucy naye yuko salama?

“Lucy yuko salama kabisa ninakwenda kila siku kujua maendeleo yake.Kwa bahati mbaya pale katika kambi yetu wanaoruhusiwa ni wafanyakazi tu wa SNSA vinginevyo ningemchukua pale ili awe salama zaidi” akasema Gosu Gosu

Walifika ofisi kuu ya SNSA salama.Hawakupata matatizo

yoyote njiani.Mathew aliongozana na Gosu Gosu wakaingia ndani na moja kwa moja wakaelekea katika ofisi ya Ruby ambaye hakujua kama tayari wamerejea.Alikuwa amejiegemeza katika kiti akionekana kuwa katika mawazo mengi.Gosu Gosu ndiye aliyemstua baada ya kugonga mlango na kufungua akaingia ndani huku Mathew akimfuata kwa nyuma.Ruby alipomuona Mathew akainuka na kumkumbatia kwa nguvu.

“Mathew my love ! akasema Ruby

“Habari Ruby” akasema Mathew

“Siamini kama kweli leo hii niko nawe tena.Huu ni kama muujiza kwangu” akasema Ruby

“Huu si muujiza Ruby.Ni kweli niko hapa” akasema Mathew lakini Ruby bado alisimama akiendelea kumshangaa

“Ruby nimefurahi kuwaona wewe na Gosu Gosu mko salama lakini sina muda

mrefu sana wa kukaa hapa” akasema Mathew

“Mathew tafadhali kabla hujatueleza chochote nihakikishie kama uko salama”

“Niko salama kabisa.Hizi damu nilimsaidia mtu aliyeumia nikamfikisha hospitali lakini mimi niko salama kabisa msihofu” akasema Mathew na kuketi kitini

“Nashukuruni ndugu zangu nimefanikiwa kuwaoneni tena mkiwa salama.Nilikuwa nahofia sana usalama wenu kwani ninyi ni

watu wangu wa pekee kabisa” akasema Mathew

“Tuko salama Mathew.Tumeweka kambi hapa katika ofisi yetu na wafanyakazi wetu wote wanaishi hapa” akasema Ruby

“Ruby nina muda mchache sana wa kuwepo nanyi hapa hivyo nataka nijielekeze moja kwa moja katika yale ya msingi.Nina mambo machache ya kuwaeleza moja ni kwamba nimeingia hapa nchini jana usiku.Nimekuja nchini kwa operesheni maalum.Pili ni kuhusiana na hizi vurugu

zinazoendelea hapa nchini hivi sasa.Nataka kujua kuna chochote mnakifahamu hadi sasa kuhusiana na vurugu hizi? Mmekwisha zifanyia uchunguzi?akauliza Mathew

“Ndiyo.Tumeanza kuzifanyia uchunguzi tayari ili kuupata mzizi wake” akasema Ruby na kumuelezea Mathew namna walivyofanya uchunguzi na mahala walipofikia katika uchunguzi wao

“Kwa hapo mlipofika ilikuwa lazima mkwame kwa sababu suala hili lina nguvu

kubwa kutoka nje ya nchi” akasema Mathew

“Ndani ya idara ya ujasusi ya Marekani CIA kuna idara ndogo ambayo inajishughulisha na mahusiano na makundi mbali mbali ya kigaidi duniani.Wanayatumia makundi hayo ya kigaidi kwa ajili ya manufaa ya Marekani.Wamekuwa wakilitumia sana kundi la IS katika eneo la Mashariki ya kati.Wanalitumia kundi hili kuanzisha mashambulio sehemu Fulani kisha hupeleka

vikosi vyao kwa kigezo cha kuwasaka magaidi kumbe wanakuwa na agenda ya siri nyuma yake na mara nyingi hufanya hivyo kwa nchi zile ambazo zinakuwa na utajiri wa kitu Fulani” Mathew akanyamaza akamtazama Ruby ambaye alikuwa anafuta machozi

“Machafuko haya yanayoendelea hapa nchini na Uganda ni mpango wa Marekani”

“Mpango wa Marekani?Ruby akashangaa

“Ndiyo Ruby”

“Marekani wamekitumia kikundi cha kigaidi cha IS kuchochea vurugu hizi zinazoendelea hivi sasa na lengo kubwa la kufanya hivyo ni ili wapate nafasi ya kuleta vikosi vyao hapa Tanzania na kuchukua mafuta kutoka Uganda.Hivi tuzungumzavyo meli kubwa za mafuta za Marekani zmepanga foleni katika bandari ya Tanga zikipakia mafuta kutoka Uganda”

“Jesus Christ ! akasema Gosu Gosu

“Mathew nakubaliana nawe na ahsante kwa kutufumbua macho kwani bila wewe ingetuchukua miaka kuweza kuligundua hili.Vurugu hizi zilianzia nchini Uganda kwa kiongozi mmoja wa dini ya kiislamu kuuawa kisha likatokea shambulio la bomu la kujitoa mhanga katika kanisa ambalo lilisababisha vifo vya watu wengi.Baada ya hapo wakristu wakaanzisha vurugu kwa kuchoma nyumba za ibada za waislamu na kisha wakaanza kushambuliana.Kwa hapa

Tanzania vurugu hizi zilianzia jijini Tanga ambako nako kulifanyika mashambulio katika makanisa na misikiti mashambulo yaliyowalenga viongozi wa dini na kupelekea waumini wa dini hizi mbili kuanza kushambuliana na machafuko yakaenea hadi jijini Dar es salaam.Ukitazama miji ambayo imekuwa na machafukoi makubwa kwa hapa Tanzania ni Dar es salaam na Tanga na baada ya maelezo haya ya Mathew sasa picha imeonekana kwamba vurugu hizi ziko kimkakati

zaidi.Huwezi kuchukua mafuta ya Uganda bila kudhibiti bandari ya Tanga na ndicho walichokifanya” akasema Ruby

“Lakini IS hawako peke yao.Kuna watu wa ndani ya nchi ambao wanashirikiana nao katika jambo hili na yawezekana miongoni mwao ni hao ambao tayari mmeanza kuwafanyia uchunguzi na hawajulikani mahala walipo.Suala hili halitaweza kumalizika hadi pale litakapochimbwa hadi mzizi wake.Tumekwisha fahamu nani walio nyuma ya hizi

vurugu lakini lazima vile vile kujua wanaochochea vurugu hizi hapa nchini ni akina nani na baada ya kuwabaini basi wawekwe wazi dunia iwajue na hii ndiyo itawafumbua macho wananchi kwamba walishawishiwa kuingia katika zile vurugu bila kujua” akasema Mathew

“Toka mwanzo niliamini kwamba hili suala linaweza kuwa na mkono kutoka nje ya nchi na sasa tumeufahamu ukweli” akasema Gosu Gosu

“Rais alikutana na kufanya mazungumzo na mufti wa

Tanzania halafu mufti akatoa hotuba yake akiwahusia waislamu kuachana na vurugu zile lakini usiku wa kuamkia leo aliawa” akasema Mathew

“Mauaji haya ya mufti yamekwamisha juhudi za kutafuta amani kwani viongozi wengine wa dini ambao walihitaji kuzungumza na Rais wameingiwa na woga” akasema Ruby

“IS ndio waliomuua mufti ili kuchochea vurugu hizi kwa maelekezo ya Marekani.Ilionekana vurugu zinaanza kupungua na

Marekani wanahitaji vikosi vyao kuendelea kukaa Afrika mashariki kwa muda mrefu zaidi hivyo walipanga mauaji yale ya mufti wakiwatumia IS ili kuwachochea waislamu na wakristu waendelee kushambuliana”

“Tumejiuliza sana kuhusu mauaji yale ya mufti tukakosa jibu.Tunashukuru Mathew kwa kutufumbua macho”

“Nimekuja hapa kuwapeni taarifa hizi ili ziwasaidie katika uchunguzi wa suala hili. akasema Mathew

“Mathew we need you ! akasema Ruby

“I know. I know”akasema Mathew na kumtazama Ruby

“Ruby I’m very sorry sintaweza kushirikiana nanyi katika suala hili.Nina misheni nyingine kubwa zaidi ambayo imenileta hapa Tanzania ila nitakachoweza kuwasaidia ni kuwapa taarifa muhimu ninazozifahamu na ninyi mtaendelea.SNSA ni idara kubwa naamini mtaweza kulifanikisha suala hili” akasema Mathew

“Mathew we real need you.Tumekwama na hatutaweza kulitatua jambo hili bila wewe” akasema Ruby

“Jambo hili lina pande mbili.Kuna upande wa ndani na upande wa nje.Ninyi mtashughulika na upande wa ndani mimi nitashughulikia upande wa nje.Upande wa ndani kuna kundi la IS na kuna watu ambao wanawasaidia IS kufanikisha lengo lao la kuchochea vurugu.Hapa mnatakiwa kuwatafuta watu hao ni akina nani pamoja na kulimaliza

kundi la IS hapa Tanzania.Kuwakamata watu wa ndani wanaoshirikiana na IS kuchochea vurugu hizi bado haitakuwa imesaidia kumaliza tatizo kwani nguvu ya nje ni kubwa zaidi na wanaweza wakafanya lolote ili mradi kuendeleza machafuko ili waendelee kuchota rasilimali.Mimi nitashughulika na nguvu hii ya nje.Mambo haya yote yanafanywa na kikundi kidogo cha watu ambao wao wanadai Marekani iko katika mikono yao na wanaiendesha

watakavyo.Kikundi hicho kidogo ndicho kinachoisumbua dunia hivi sasa na kusababisha machafuko kila sehemu.Kila ukifungua taarifa za habari hukosi kukuta kuna taarifa za tukio la kigaidi sehemu Fulani na mengi ya matukio haya yanafanikishwa na kikundi hiki.Umefika wakati wa kukimaliza kikundi hiki na kupunguza kama si kumaliza kabisa ugaidi duniani kwa sababu vikundi vingi vya ugaidi vinategemea ufadhili kutoka kwa kikundi hiki

kidogo.Ninaomba mniamini ndugu zangu kwamba ninakwenda kukimaliza kikundi hiki.Ni misheni ngumu na ya hatari sana lakini lazima niikamilishe.Wamemwaga damu ya ndugu zetu na siwezi kukubali damu ya mtanzania ikapotea bure lazima ilipwe hivyo nawataka muhakikishe mnawashughulikia watu wa ndani wakati mimi nikishughulika na watu wa nje.Kwa pamoja tutalifanikisha hili jambo" akasema Mathew

“Mathew ni asubuhi ya leo mimi na msaidizi wangu Gosu Gosu tulipokwama hatujui nini tufanye tulianza kukujadili kwamba laiti ungekuwepo ungetusaidia kutuondoa katika mkwamo huu kwani sisi hatuna ujuzi mkubwa katika masuala haya kama wewe.Nilimpigia Najma ili niweze kuzungumza nawe lakini simu yake haikuwa ikipatikana” akasema Ruby na sura ya Mathew ikabadilika baada ya kusikia jina la Najma likitajwa

“Umesema Najma? Akauliza Mathew

“Ndiyo”

“Najma yupi ulimpigia kutaka kuzungumza nami?

“Najma mke wako.Huna mke anaitwa Najma?akauliza Ruby na Mathew akavuta pumzi ndefu wakatazamana

“Kuna kitu unataka kukisema Mathew? Ruby akauliza

“Umefahamuje kuhusu Najma?Ulikuwa unanifuatilia? Mathew akauliza

“Ndiyo maana uliniambia nisikufuatilie ili nisifahamu

kama umebadili jina lako na unaitwa Abu Zalawi raia wa Saudi Arabia na pia umemuoa Najma? Akauliza Ruby

“Ulinifuatilia ukayafahamu haya?Kwa nini ukapuuza maelekezo yangu Ruby?akauliza Mathew akimtazama Ruby kwa macho makali.

“Sikukufuatilia Mathew.Ninaheshimu makubaliano yetu.Nilipigiwa simu na Najma mwenyewe akajitambulisha kwangu kama mke wako na kwamba ulikuwa unanitafuta simuni

hukunipata.Alinipigia kuuliza kama ninakufahamu lakini alikutaja kwa jina la Abu Zalawi na si Mathew Mulumbi.Nilimweleza sikufahamu na wala sina rafiki anaitwa kwa jina hilo.Baadae nilimpigia na kumtaka anitumie picha za huyo Abu akadai kwamba hana picha.Nilipatwa na wasi wasi labda Uingereza wameanza kunitafuta ikanilazimu kuingia mtandaoni kutafuta ndipo nikakupata" akasema Ruby akamtazama Mathew.Macho yake yalilengwa

machozi.Mathew akavuta pumzi ndefu kisha akasema

“Ni kweli.Yote aliyokwambia Najma ni kweli kabisa lakini hapa si mahali pake tutayazungumza hayo siku nyingine.Nataka tujielekeze katika jukumu lililo mbele yetu” akasema Mathew na Ruby akafuta machozi

“Mathew naomba utuamini kwamba tumekwama na tunahitaji sana msaada wako.Tafadhali endelea na misheni yako baada ya kuhakikisha kwamba tumelimaliza hili suala na nchi

iko salama.Nisingekuomba haya kama tungekuwa na uwezo huo” akasema Ruby

“Ruby siwezi.Misheni ninayokwenda kuitekeleza ni kubwa na yenye manufaa kwa dunia nzima.Ninakwenda katika misheni ya hatari kuliko misheni zote nilizowahi kushiriki”

“Mathew ni misheni ipi hiyo unayokwenda kuifanya ambayo ni muhimu kuliko kuisaidia nchi yako?akauliza Ruby

“Ninakwenda kukiondoa kikundi hiki kidogo ambacho

kimekuwa kikishirikiana na magaidi na kuharibu amani ya dunia”

“Mathew ..! akasema Ruby lakini Mathew akamkatisha

“Don’t say anything Ruby.Tayari ninafahamu kile unachotaka kukisema.Kikundi hiki ndicho mzizi wa haya machafuko yanayoendelea hapa nchini hivyo misheni hii pia ni mwendelezo wa kuisaidia nchi yetu na dunia” akasema Mathew na ukimya ukapita

“Kuna mambo ambayo mtayasikia kuhusu mimi lakini

nawaomba mtakapoyasikia msiyaamini hata kidogo.Niko katika misheni nzito na hayo yatakayotokea na kunihusisha mimi ni sehemu ya misheni hiyo.Utakuwa ni mshangao kwa wengi lakini ninyi nawaomba msishangae kuweni na imani na mimi.Baada ya kuikamilisha misheni hiyo nitarejea nyumbani”akasema Mathew na kuwatazama akina Ruby ambao kila mmoja alibaki na maswali kichwani

“Tuachane na suala hilo.Kuna mtu anaitwa Assad Ismail.Huyu anaongoza kundi

la IS katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na kati.Makazi yake ni Mombasa Kenya lakini kwa sasa yuko hapa nchini na ndiye anayesimamia jukumu la IS la kuchochea vurugu.Yeye na watu wake ndio waliomuua mufti jana na wao ndio waliofanya na wanaoendelea kufanya mauaji ya viongozi wadini ili kuchochea vurugu.Mnatakiwa kumpata huyu Assad kwani atawasaidia sana kufahamu mambo mengi kuhusiana na watu wanaoshirikiana nao hapa

nchini na mnaweza mkafahamu vile vile kuhusiana na wale ambao mnahisi wanahusika katika machafuko haya lakini wamepotea na hawajulikani walipo.Sifahamu Assad anaishi wapi hapa Dar es salaam lakini kuna mtu ambaye anaweza akawaongoza kujua mahala alipo Assad.Mtu huyo anaitwa Marwan Hossam.Huyu anaishi kwa Botha nyumba namba 604.Hii ni nyumba wanamoishi magaidi wa IS na mipango yao yote ya mashambulio hupangwa katika nyumba

hii.Mkivamia nyumba hii mtapata mambo mengi yanayoweza kuwasaidia kufahamu mambo mengi kuhusiana na hili suala” akasema Mathew

“Mathew tunashukuru sana kwa taarifa hii.Nashauri kwa nini tusiende kuvamia nyumba hiyo usiku huu tukiwa pamoja nawe kabla hujaendelea na misheni yako? Akauliza Gosu Gosu

“Kwa leo haiwezekani Gosu Gosu.Jambo hili mtalifanya usiku wa kesho baada ya mimi kuondoka.Mimi

ninamaliza misheni yangu kesho usiku na kuondoka na ninyi mtaenda kuvamia nyumba hiyo na kumkamata Marwan Hossam ambaye atawapeleka mahala alipo Assad”

“Kwa nini leo haiwezekani Mathew?Tunao makomando wetu ambao watatusaidia kuvamia nyumba hiyo”Ruby naye akasisitiza.

“Haiwezekani kwa sababu ninaishi ndani ya nyumba hiyo” akasema Mathew na mstuko uliowapata Ruby na Gosu Gosu ulikuwa mkubwa.

“Unashirikiana nao?akauliza Ruby akionyesha sura ya wasi wasi

“Ni sehemu ya misheni yangu ndiyo maana nikatangulia kuwaomba kwamba msistuke kwa mtakachokisikia kuhusu mimi hapo baadae” akasema Mathew

“Kitu gani umekuja kukifanya Mathew? Umewezaje kuingia hapa nchini? Akauliza Ruby

“Ruby natamani sana niwaeleze lakini sitakiwi kufanya hivyo.Ninawaomba

mniamini ndugu zangu.Naamini utafika wakati ambao nyote mtashikwa na butwaa lakini naomba ninyi wawili muendelee kuwa na imani nami.Yote mtakayosikia ni sehemu ya misheni yangu kubwa” akasema Mathew

“Mathew unatuogopesha sana kwa haya maneno yako.Nini kinakwenda kutokea?akauliza Gosu Gosu

“Usihofu Gosu Gosu utasikia tu.Nawaombeni ndugu zangu kwa sasa tuliweke pembeni hilo na tujielekeze katika hiki

kinachoendelea hapa nyumbani.Suala hili ni kubwa na ninawaomba muwe na umakini mkubwa sana mnapolishughulikia.Magaidi hawa wa IS wana silaha nzito na wanapata msaada kutoka kwa vikosi vya Marekani.Kwa mfano Assad anapotoka mahala anakoishi kwenda katika nyumba hiyo ambayo ni kambi ya magaidi husindikizwa na gari la doria la vikosi vya Marekani.Hali ni mbaya huko mtaani na kwa hili walilolifanya la kumuua Mufti litaongeza zaidi

machafuko haya.Usiku huu wameondoka tena na silaha nzito naamini kuna mahali wamekwenda kufanya shambulio” akasema Mathew

“Mathew nakushukuru sana kwa kuja.Kwa mara nyingine tena umedhihirisha ni namna gani ulivyo na umuhimu mkubwa kwa nchi hii.Hatukuwa tukifahamu chochote kuhusu haya yanayoendelea.Tulifika mahala tukakwama na hatujua wapi kwa kutokea lakini umetokea wewe na kutumulikia mwanga sasa tumepata sehemu ya

kuanzia.Naamini misheni hiyo uliyonayo ni muhimu sana kwani hujawahi hata mara moja kukataa kufanya misheni kwa ajili ya nchi yako.Tumekuelewa Mathew na tunakutakia kila la heri katika hiyo misheni yako ambayo kama ulivyotuhakikishia ni kwamba itakuwa na manufaa makubwa sana kwa nchi na dunia nzima.Sisi tutaendelea kusimama nawe na kukuombea uweze kumaliza salama operesheni hiyo.Muda wowote utakapohitaji msaada

wetu sisi tupo tayari kukusaidia” akasema Ruby

“Ruby ninashukuru kwa kunielewa.Muda wowote nitakapohitaji msaada wenu nitawasiliana nanyi haraka sana” akasema Mathew na ukimya ukapita

“Ruby na Gosu Gosu ninashukuru tena kwa kuonana nanyi ndugu zangu na kuhakikisha mko salama.Nilikuwa na wasiwasi mkubwa kuhusiana na usalama wenu lakini kwa sasa nina amani na hata huko nitakapokuwa nitakuwa na

amani kwamba ndugu zangu wako salama.Naomba sasa mniruhusu niondoke lakini naomba mnipatie mavazi nibadilishe” akasema Mathew na Gosu Gosu akaenda kumletea mavazi ya kubadilisha kwani nguzo zile alizokuwa amevaa zilikuwa zimechafuka damu.

“Mathew sijui niseme nini.Sijui ni……” akasema Ruby baada ya Gosu Gosu kuondoka

“Don’t say anything.Pray for me.I promise I’ll come back” akasema Mathew

“Mathew nina wasi wasi sana kuhusu usalama wako”

“Usihofu Ruby.Nitakuwa salama na nitarejea.Narudia tena kuwaomba hakikisheni kwa namna yoyote ile mnawapata hawa watu niliowapa taarifa zao ili nchi iwe na amani.Tanzania haikupaswa kuwa namna hii.Mambo kama haya tulikuwa tunayaona katika nchi nyingine lakini sasa yamefika kwetu.Hali ni mbaya sana huko mitaani.Nakuhakikishia Ruby kwa hiki walichokifanya

kumwaga damu za watanzania namna hii huku wao wakiendelea kushangilia neema ya mafuta kutoka Uganda hawatabaki salama.Nitahakikisha kikundi hiki kidogo cha hawa watu ninakifutilia mbali.Ni misheni ndefu na ya hatari lakini nitakufa nikijaribu.Bila kukiondoa kikundi hiki dunia haitakuwa mahala salama” akasema Mathew

“Mathew sijui kwa nini ninahisi baridi kila unapotamka kuhusiana na misheni hiyo ya hatari ambayo

umeshindwa kutueleza ni misheni gani.Kama ingekuwa ni kwa ridhaa yangu ningekuzuia usiende huko lakini siwezi.Oh Mathew ! akasema Ruby na kuinamisha kichwa machozi yalikuwa yanamtoka

“Ruby huu si wakati wa kumwaga machozi.Damu za watanzania wenzetu zinamwagika hivyo hatupaswi kumwaga machozi tunatakiwa kupambana kuhakikisha tunarejesha maisha kuwa ya kawaida” akasema Mathew na Gosu Gosu akaingia.Mathew

akavua zile nguo zilizochafuka damu na kuvaa nguo alizopewa na Gosu Gosu.Ruby akasimama na kumkumbatia Mathew

“Mathew please be safe my love” akasema Ruby

“I will” akajibu Mathew na kumuachia Ruby wakaongozana kutoka nje wakaelekea katika gari lile la makomando Mathew hakugeuka nyuma kumtazama Ruby akaingia garini na gari likaondoka,Ruby akarejea ofisini kwake akajifungia akilia.

****

Mathew aliwataka akina Gosu Gosu wamuache karibu na mtaa ilipo nyumba ile ya magaidi .

“Gosu Gosu tafadhali hakikisha Ruby anakuwa salama.Hakikisheni pia amani inarejea hapa nchini tayari nimekwisha wapa mwanga sehemu ya kuanzia” akasema Mathew

“Mathew ninakushukuru sana kwa taarifa hizi ulizotupa.Nakuahidi hakuna

atakayesalia.Tutawasaka wote hadi mtu wa mwisho” akasema Gosu Gosu

“Ahsante Gosu Gosu.Mbaki salama” akasema Mathew kisha akaanza kukimbia kuelekea katika mtaa alikofikia.Kulikuwa na ukimya mkubwa.Alifika katika nyumba yao akazunguka upande wa nyuma akapanda ukuta na kurukia ndani bila kutoa ukelele.Hakukuwa na mtu yeyote mahala pale akatembea kwa tahadhari kuelekea katika mlango wa nyuma akaufungua na kuingia jikoni kisha

akaelekea moja kwa moja chumbani kwake.Ilipata saa kumi kasoro za alfajiri.Mathew akajilaza kitandani.

“Ahsante Mungu kwa kunirejesha salama bila hawa watu kujua” akasema kwa sauti ndogo.

“Nimefurahi kuwakuta Ruby na GosuGosu wakiwa salama.Hiki ndicho kitu ambacho nilikuwa naomba sana kuwakuta watu hawa wako salama.Ninashukuru vile vile kwa Gosu Gosu kuungana na Ruby na hii inanipa uhakika mkubwa kwamba Ruby

atakuwa salama.Hata hivyo kuna kitu ambacho sikukitegemea kabisa.Najma kumpigia simu Ruby na kujitambulisha kuwa yeye ni mke wangu.Nilistuka sana.Sikutegemea kabisa kitu kama hiki kutokea.Sikutaka Ruby afahamu chochote kuhusu maisha yangu kule Saudi Arabia.Nimejaribu kumtuliza lakini ameumia.Kwa nini Najma alimpigia simu Ruby? Akajiuliza Mathew na kukumbuka kitu.

“Nakumbuka siku ile tuliporejea kutoka Fiji na

Habiba akanieleza kuhusu machafuko yanayoendelea hapa Tanzania nilitaka kumpigia simu Ruby kujua kama yuko salama lakini simu yake haipatikani nakumbuka Najma alikiona kitabu kile nilichokuwa nimeandika namba za simu na akaiona namba ya simu ya Ruby akaniuliza Ruby ni nani? Nadhani kuanzia pale alianza kuwa na mashaka na nilipoondoka akaamua kumpigia simu Ruby akitaka kumfahamu kama ni mpenzi wangu.Hata hivyo tumefikia

mwisho kwani Habiba alinitaka nisirejee tena Saudi Arabia.Kama misheni hii ikimalizika na nikabahatika kuwa mzima nitarejea Tanzania na kumuoa Ruby” akawaza Mathew na kuvuta pumzi ndefu

“Kuna nyakati ninaingiwa na hofu kubwa kuhusiana na misheni hii ninayokwenda kuifanya.Ni misheni ya hatari sana na itagharimu damu ya watu wengi” akawaza

“Lakini sipaswi kuogopa.Bila kuifanikisha hii misheni nchi zetu zitaendelea

kuwa uwanja wa vita.Machafuko yataendelea huku mabepari hawa wakiendelea kuchota mai zetu na kunufaisha nchi zao.Lazima nijitoe mhanga kuhakikisha hili haliendelei.” akawaza Mathew na kijiusingizi kikaanza kumpitia akalala.

****

Saa kumi na mbili za asubuhi ilimkuta Ruby akiwa bado ofisini kwake.Hakupata usingizi hivyo aliendelea kufanya kazi

usiku.Wafanyakazi walipoanza kuingia ofisini asubuhi walimkuta akiwa ofisini akiendelea na kazi.Saa mbili za asubuhi akawakusanya wote kwa ajili ya kuwapa taarifa muhimu.

“Habarini za asubuhi ndugu zangu.Naamini nyote mnaendelea vyema” Ruby akawasalimu wafanyakazi wa SNSA

“Usiku wa kuamkia jana watu wasiojulikana walimuua Mufti wa Tanzania ikiwa ni katika muendelezo wa mauaji ya viongozi wa dini ambayo

ndiyo chanzo cha vurugu hizi zinazoendelea.Kutwa nzima ya jana tulikuwa katika kutafuta nani waliomuua kiongozi huyo wa dini bila mafanikio lakini usiku wa jana tulipata taarifa kutoka katika chanzo chenye uhakika kwamba mauaji haya yanayoendelea yanafanywa na kikundi cha kigaidi cha IS" akasema na kunyamaza akawatazama wafanyakazi

"Vurugu hizi zote ambazo zinaendelea nchini hivi sasa IS ndio waliozichochea.Walifanya mauaji ya kule Tanga ambayo ndicho kilikuwa chanzo cha

vurugu kwa hapa Tanzania.Walihamia Dar es salaam na kuendelea na zoezi lile lile la kuua viongozi wa dini kwa ajili ya kuchochea vurugu baina ya waumini wa dini za kikristu na kiislamu.Juzi mufti wa Tanzania alikutana na Rais wakazungumza faragha na baadae wakazungumza na watanzania akawaomba waislamu wasiendelee na vurugu lakini usiku wa siku hiyo akauawa kwa bomu yeye na familia yake.Kwa nini Mufti aliuawa? Akauliza Ruby

“Hotuba aliyoitoa Mufti kuwataka watanzania wasiendelee kushambuliana na kuuana ilionekana kuwa na mapokeo mazuri kwani vurugu zilipungua kwa kiasi kikubwa baada ya hotuba ile na hii iliwapa hofu wale wanaotaka vurugu kuendelea ndiyo maana wakamuua” Ruby akanyamaza

“Haikuishia hapo katika mauajiya Mufti.Usiku wa kuamkia leo nyumba ya imevamiwa na watu wenye silaha kwa lengo la kufanya shambulio lakini walikutana

na upinzani mkali kutoka kwa askari polisi waliokuwa hapo wakilinda kwani serikali imeweka ulinzi mkali katika nyumba zote za watawa,shule za dini,makanisa na misikiti.Wavamizi hao waliokuwa na silaha nzito walishindwa kutekeleza lengo lao baada ya kuzidiwa nguvu na kukimbia huku wakitelekeza silaha zao.Waliofanya shambulio hilo tunaamini ni kikundi cha IS ambao lengo lao ni kuchochea vurugu.Wamemuua kiongozi wa waislamu ili

ionekane ni wakristu wamefanya hivyo na wakataka tena kuua watawa wa kikristu ili ionekane kwamba waislamu wamefanya mauaji hayo ili kulipiza kisasi kwa kiongozi wao kuuawa na lengo kubwa ili waumini wa dini hizi mbili waendelee kushambuliana” akanyamaza Ruby na kushika kitanza mbali akabonyeza na picha kubwa ikatokea katika runinga

“Anaitwa Assad Ismail.Huyu ni kiongozi wa IS katika eneo la Afrika Mashariki na kati na makazi

yake ni Mombasa Kenya ila kwa sasa yuko hapa nchini kwa ajili ya misheni ya kuchochea vurugu.Assad yuko hapa Dar es salaam lakini hatujui ni sehemu gani na huyu ndiye ambaye anaongoza kikosi cha magaidi wanaoua viongozi wa dini na kuchochea machafuko zaidi" akabonyeza tena kitanza mbali ikatokea picha nyingine

"Anaitwa Marwan Hossam.Huyu anaishi hapa Dar es salaam eneo la kwa Botha nyumba namba 604.Huyu ndiye anayefahamu mahala anakoishi Assad hapa

Dar es salaam.Kwa taarifa tulizo nazo ni kwamba nyumba hii ndimo ambao IS wamekuwa wakipanga mipango yao yote ya mauaji” akasema Ruby akatulia kidogo

“IS hawako peke yao.Kuna watu wanashirikiana nao katika kuchochea vurugu hizi.Watu hao lazima wapo hapa nchini.Kama mtakumbuka tumekuwa na zoezi la kuwafuatilia watu kadhaa ambao tunahisi wana mahusiano na vurugu hizi zinazoendelea lakini tumegundua wote

wametoweka na hawajulikani walipo.Tunaamini upo mtandao ambao unashirikiana na magaidi hawa katika kuanzisha vurugu.Swali ambalo tunatakiwa kujiuliza ni je IS wanafanya haya yote kwa faida ya nani?Je kuna nchi au kikundi cha watu kimewatuma wafanye haya? Hayo ndiyo maswali ambayo tunatakiwa kuyatafutia majibu.Usiku wa leo tunakwenda kuvamia nyumba hiyo wanamoishi magaidi wa IS na kumchukua Marwan Hossam ambaye atatusaidia kujua mahala alipo

Assad.Tukifanikiwa kumpata Assad tutajua kuhusu mtandao wa watu wanaoshirikiana nao katika kuchochea vurgu hizi wale wa ndani na nje ya nchi” akasema Ruby

“Mchana wa siku ya leo tutaelekeza drone yetu katika nyumba hiyo wanamoishi hao magaidi kufuatilia kila kinachofanyika hapo ndani huku makomando wetu wakijipanga namna ya kuingia ndani na kuwachukua magaidi hao.Mmoja wa madereva wetu atapeleka gari hadi mbele ya nyumba hiyo ili tuwe na

uhakika wa nyumba tunayoilenga.Mchana kutwa wa leo tutaanza kufuatilia kila kinachoendelea ndani ya nyumba hiyo na usiku wa leo kikosi cha makomando wetu kitavamia hapo.Tutachukua kila atakayekuwepo mahala hapo na kuja kuwafanyia mahojiano lakini mlengwa mkuu katika misheni hiyo ni Marwan Hossam ambaye atatuongoza kujua mahala alipo Assad Ismail" akasema Ruby na kutaka maandalizi yaanze mara moja kisha akaelekea ofisini kwake.

Baada ya dakika kumi akaingia Gosu Gosu

“Tayari dereva amekwisha ondoka na moja ya gari kuu kuu ambalo limewekewa mkanda maalum kwa juu ili kutuwezesha kumfuatilia.Baada ya kupata picha za nyumba hiyo wanamoishi magaidi makomando wataanza maandalizi ya namna wakatavyoweza kuingia humo ndani” akasema Gosu Gosu

“Good” akajibu Ruby

“Ruby kwa nini hujawaeleza ukweli kwamba ni

Marekani ndio wako nyuma ya haya yote yanayoendelea hapa nchini?akauliza Gosu Gosu

“Hapana hawapaswi kufahamu jambo hilo.Litabaki kati yetu kwa sasa.Nina hofu yawezekana jambo hili likivuja linaweza kuvurga kila kitu na tukashindwa kuwapata watu wanaojihusisha na machafuko hayo” akasema Ruby

“Ruby macho yako mazito sana.Hujalala usiku wa kuamkia leo.Unahitaji kwenda kupumzika kidogo” akasema Gosu Gosu

“Hapana Gosu Gsou siwezi kwenda kulala.Tuna kazi nyingi za kufanya kuhakikisha tunaupata mtandao wote wa watu wanaochochea vurugu hizi.IS wanaendelea kufanya mauaji hivyo lazima tuhakikishe kwamba tunawapata wote na kufahamu watu wanaoshirikiana nao” akasema Ruby

“Tutawapata Ruby usihofu.Mathew amekwisha tupa mwanga na kuanzia hapa tunajua wapi tuelekee” akasema Gosu Gosu

“Nilidhani ninamfahamu vizuri Mathew Mulumbi kumbe nilikuwa najidanganya.Bado simfahamu vizuri ni mtu wa aina gani.Mambo yake yananishangaza sana.Ni misheni gani aliyonayo ambayo inamfanya ashirikiane na hawa magaidi? Kitu gani kitatokea ambacho anasema tusikiamini tutakapokisikia?akauliza Ruby

“Lazima itakuwa ni misheni kubwa sana lakini tusubiri tutajua” akasema Gosu Gosu

RIYADH – SAUDI ARABIA

Bado watu waliendelea kufika katika makazi ya Habiba Jawad kumpa pole kufuatia vifo vya mfululizo vya watoto wake wawili Najma na Abu Dahir.Saa tatu za asubuhi gari moja lilifika katika makazi yale ya Habiba na watu watano wakashuka.Walipokewa na Sayid Omar ambaye alikuwa anawapokea wageni mbali mbali wanaofika pale nyumbani akawapeleka katika nyumba Fulani

akawakaribisha sebuleni nzuri halafu akamfuata Habiba Jawad akamjulisha kuwa wageni wamefika.Habiba akiwa ameongozana na Nawal wakaelekea katika nyumba walikopelekwa wale wageni.

“Yule mtu kutoka IS ameletwa” Habiba akamwambia Nawal.

Waliingia katika nyumba ile wakasalimiana na watu wale wakampa pole nyingi Habiba kwa msiba mzito uliompata.Baada ya hapo yakaanza maongezi kuhusiana na Yule mtu ambaye Habiba

alimuhitaji kutoka IS kwa ajili ya kwenda kutumika katika zoezi la kusambaza kirusi nchini Tanzania.Aliitwa Sattar Sayf Al Din.

Habiba na wale jamaa walikuwa na mazungumzo marefu yaliyochukua saa mbili kisha wakafikia makubaliano na wale jamaa wakamuaga Habiba wakaondoka ila Sattar akabaki.Baada ya wale jamaa kuondoka Habiba akamtaka Nawal kumpiga picha Sattar ili aweze kuzitma Marekani wamfahamu kwani alitarajia kuondoka jioni ya siku ile na

ndege kuelekea Marekani.Baada ya kuzipata picha zile akamkabidhi Sattari kwa Sayid Omar ili ampeleke katika mojawapo ya nymba za wageni akapumzike wakati safari yake ya kwenda Marekani ikiandaliwa.

“Tayari tumemfahamu mtu ambaye atatumiwa na Marekani kusambaza virusi nchini Tanzania” akasema Habiba

“Ndiyo mama” akasema Najma

“Kinachofuata ni wewe kwenda kumsubiri nchini Tanzania” akasema Habiba

“Hakuna tatizo mama mimi niko tayari kwenda huko Tanzania”

“Vizuri.Nitawasiliana na Yule mtu ambaye Najma aliwasiliana naye anaitwa Ruby ili nimuombe akupokee kwani ni mara yako ya kwanza kufika Tanzania” akasema Habiba

“Nitajuaje kama Sattar amewasili Dar es salaam? Naamini safari yake ya

Tanzania itakuwa ya kimya kimya sana” Akauliza Nawal

“Nitawasiliana na watu wa IS ili wanipe mawasiliano ya mtu wa IS aliyeko Dar es salaam.Ninaamini yeye atakuwa na mawasiliano na Marekani na lazima atafahamu kuhusu Sattar na jibu nitakalolipata nitakujulisha.Utakapofika huko jitahidi upate mawasiliano”akasema Habiba

“Nitajitahidi mama.Lakini ni vipi kama huyo mtu wa IS aliyeko Tanzania akakosa

taarifa za Sattar?akauliza Nawal

“Sattar lazima awe na mtu wa kumsaidia akiwa nchini Tanzania na mtu pekee ambaye anaweza akatumiwa ni aliye katika mtandao wa IS.Usihofu nitafanya kila niwezalo kupata taarifa za kuhusiana na Sattar” akasema Habiba

“Sattar anaondoka leo kwenda Marekani na hatujui ni lini ataondoka Marekani kwenda Tanzania hivyo wewe utaondoka Kesho hadi Nairobi Kenya.Uwanja wa ndege wa

Nairobi Kenya haujafungwa unaendelea kupokea ndege na kutoka pale utatafuta usafiri wa kukuingiza nchini Tanzania.Nitazungumza na Ruby nijue kama anaweza akakusaidia ukaweza kuingia Tanzania.Endapo hatakuwa na uwezo wa kukusaidia nitatafuta namna ya kuweza kukuingiza nchini Tanzania siwezi kushindwa” akasema Habiba halafu akaenda kuchukua kitabu ambacho Mathew alikuwa ameandika namba za simu akapekua na kuupata ukurasa ambao

ulikuwa na namba za simu za Ruby,akaziandika katika simu yake na kupiga.

“Simu inaita” akasema Habiba

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Ruby alihisi uchovu mwingi akakiegemeza kichwa chake kitini.Mara simu yake ikaanza kuita akanyoosha mkono akaichukua na kutazama mpigaji zilikuwa ni namba ngeni katika simu yake.

“Hizi ni namba za simu za Saudi Arabia.Huyu lazima atakuwa ni Najma.Ngoja nimsikie anachotaka kunieleza” akawaza Ruby na kupokea ile simu

“Hallow” akasema

“Hallow,naongea na Ruby?akauliza mwanamama wa upande wa pili.Sauti ile haikuwa ya Najma.Ruby akastuka kidogo

“Nani anaongea?akauliza Ruby

“Naitwa Habiba Jawad,ninapiga simu kutoka Saudi Arabia”

“Habiba Jawad?Ruby akauliza

“Ndiyo.Nazungumza na Ruby?akauliza Habiba na Ruby akawa kimya.Alistuka sana

“Hallow” akaita Habiba

“Hallow umesema wewe ni nani?Ruby akauliza

“Naitwa Habiba Jawad ninapiga simu kutoka Saudi Arabia.Wewe ni Ruby?akauliza Habiba

“Ndiyo naitwa Ruby.Umenifahamuje?Umetoa wapi namba zangu?akauliza Ruby

“Unamfahamu Mathew Mulumbi?akauliza Habiba na kuendelea kumstua zaidi Ruby

“Ruby ! akaita Habiba

“Nimekuuliza unamfahamu Mathew Mulumbi?akauliza Habiba

“Umemfahamuje Mathew Mulumbi?

“Mathew ni kijana wangu amemuoa binti yangu Najma ambaye alikupigia simu hivi majuzi” akasema Habiba na Ruby akahisi baridi ikimpenya

“Ruby sikiliza mwanangu.Ninamfahamu Mathew Mulumbi na anaishi

hapa kwangu na binti yangu Najma.Ni mimi niliyemtoa katika taabu na mateso aliyokuwa nayo na kuanza maisha mapya hivyo namchukulia kama mwanangu.Nimepata namba zako kutoka katika kitabu chake maalum” akasema Habiba

“Unahitaji nini Habiba?akauliza Ruby huku sauti yake ikionekana kutetema

“Nina shida naomba msaada wako”

“Msaada gani unauhitaji?

“Kuna binti yangu anakuja Tanzania.Ni mara yake ya kwanza hivyo nakuomba ukubali kumpokea na kumsaidia”akasema Habiba

“Binti yako anakuja Tanzania?Najma? Ruby akauliza

“Hapana si Najma.Anaitwa Nawal” akasema Habiba na Ruby akavuta pumzi ndefu.

“Ruby ! akaita Habiba

“Anakuja kufanya nini Tanzania? Akauliza Ruby

“Kuna kazi anakuja kuifanya.Nakuomba umpokee tafadhali na umsaidie.Kwa

kuwa uwanja wa ndege wa Dar es slaam umefungwa atalazimika kupita nchini Kenya atashukia jijini Nairobi na kutokea pale atatumia magari ya kawaida kuingia Tanzania kupitia mpaka wa Namanga akielekea Dar es salaam" akasema Habiba

"Hakuna haja ya kwenda kushukia jijini Nairobi.Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro umekwisha funguliwa kwa sasa na unaendelea kutoa huduma.Ndege zote ambazo zilipaswa zitue katika uwanja

wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es salaam sasa zinakwenda kutua uwanja wa Kilimanjaro.Mikoa ya Kaskazini hakuna vurugu kubwa kama ukanda huu wa pwani hivyo nashauri kama anakuja ashukie Kilimanjaro na mimi nitakwenda kumpokea hapo”

“Ahsante sana Ruby.Nitalifanyia kazi hiyo ili aweze kushukia uwanja wa ndege wa Kilimanjaro.Nategemea aondoke kesho asubuhi na

ndege ya shirika la ndege la Ethiopia”

“Mimi niko Dar es salaam lakini nitafanya utaratibu wa kuhakikisha huyo mwanao anafika Dar es salaam”

“Nashukuru sana Ruby .Ni namna gani nitaweza kukutumia fedha za kufanikisha jambo hilo?Sitaki uingie gharama kwa kutumia fedha zako.Kama kuna namna yoyote naweza kukutumia fedha nielekeze tafadhali” akasema Habiba

“Usijali mama.Huna haja ya kutuma fedha.Kwa kuwa

umemsaidia Mathew basi nami nitamsaidia mwanao.Unaweza ukaniambia anakuja kufanya nini Tanzania wakati huu wa machafuko?akauliza Ruby

“Kuna jambo muhimu sana linamleta hapo Tanzania.Tafadhali naomba umsaidie” akasema Habiba

“Nitamsaidia usijali”

“Sawa.Nitakutumia picha zake ili umfahamu” akasema Habiba na kuagana na Ruby

“Haya ni mambo gani yanaendelea? Mathew anashirikiana na Habiba

Jawad? Ruby akajiuliza.Alishangaa sana

“Nini kimetokea hadi Mathew akaamua kujiunga na Habiba Jawad?Huyu mama ndiye anayefadhili makundi ya kigaidi duniani. Dah ! ni vigumu kuamini ! akawaza Ruby

“Ninahisi mwili unakosa nguvu kwa kulifahamu hili.Mathew anafahamu kabisa Habiba Jawad ni nani lakini ameamua kushirikiana naye na kama haitoshi amemuoa hadi mwanae Najma.Nini kimemtokea Mathew Mulumbi

hadi akaamua kushirikiana na magaidi? Ndiyo maana alinionya nisimfuatilie kwa kuogopa ningeweza kugundua anashirikiana na Habiba Jawad mfadhili mkubwa wa ugaidi duniani.Kadiri ninavyoendelea kumfahamu Mathew ninazidi kugundua mambo mengine ambayo yananitisha na kunifanya nimuogope.Mathew ninayemuona sasa si Mathew Yule ambaye nilimfahmau miaka kadhaa iliyopita ambaye nilitokea kumpenda kupita ninavyojipenda

mwenyewe.Nadhani ninachokipata mimi ndicho alichokipata Peniela na akaamua waachane.Ninaanza kuona maamuzi ya Peniela kuachana na Mathew yalikuwa sahihi.Ninampenda sana Mathew kwa moyo wangu wote lakini sina hakika kama nina kifua cha kuvumilia haya yanayomzunguka" akawaza Ruby na kutazama juu

"Kama tayari ameanzisha mashirikiano na Habiba Jawad ni wazi ameamua kushirikiana na kundi la IS na hapa nchini anadai amekuja kwa ajili ya

misheni maalum.Lazima alichokuja kukifanya kinahusiana na kundi la IS.Nini amekuja kukifanya? Huyo Nawal naye anakuja kufanya nini?Naamini huyu Nawal naye kuna kitu anakuja kukifanya hapa Tanzania ambacho kinahusiana na IS" akaendelea kuwaza.

"Hapana siwezi kumuacha Mathew akapotea namna hii.Lazima nimsaidie japo hatapenda lakini lazima nifanye kitu kumsaidia kwani akiendelea kushirikiana na mtandao huu wa kigaidi

maisha yake yatakuwa mashakani.Siwezi kukubali Mathew awe gaidi.Kwa kuwa tayari amekwisha tuelekeza nyumba walimo magaidi wa IS nitaelekeza vikosi kuvamia nyumba hiyo na kuwachukua magaidi wote akiwamo Mathew.Atashikiliwa kwa muda ili kumuhoji kujua ni kitu gani kimemsababisha akabadilika kutoka Jasusi hadi Gaidi.Siwezi kuvumilia lazima haraka sana makomando wetu wakavamie nyumba hiyo" akawaza na kuchukua simu akampigia Gosu Gosu

akamtaka aende ofisini kwake mara moja

“Kuna nini Ruby? Akauliza Gosu Gosu

“Gosu Gosu ninazidi kuchanganywa na huyu Mathew”

“Kuna nini tena kuhusu Mathew?akauliza Gosu Gosu na Ruby akavuta pumzi ndefu

“Nimepokea simu muda si mrefu kutoka Saudi Arabia”

“Kutoka kwa Najma?akauliza Gosu Gosu

“Unamkumbuka Habiba Jawad?akauliza Ruby

“Habiba Jawad Yule mfadhili wa ugaidi?Ninamkumbuka” akajibu Gosu Gosu

“Huyo ndiye aliyenipigia simu”

“Habiba Jawad amekupigia simu?! Gosu Gosu akashangaa

“Ndiyo amenipigia simu”

“Amepataje mawasiliano yako?

“Ni mambo ya ajabu sana Gosu Gosu”

“Niambie Ruby.Habiba Jawad amepataje namba

zako?Alikupigia kwa dhumuni gani? Akauliza Gosu Gosu

“Habiba Jawad ni mama yake Najma ambaye ameolewa na Mathew” akasema Ruby na mstuko ukaonekana usoni kwa Gosu Gos

“Najma ni mtoto wa Habiba Jawad?

“Ndiyo.Habiba amenihakikishia kwamba Mathew anaishi kwake na amemuoa mwanae Najma”

“Haya ni maajabu.Inawezekanaje Mathew akajiunga na Habiba

ambaye anafadhili ugaidi?akauliza Gosu Gosu

“Nimejiuliza swali hilo sijapata jibu.Mathew anafahamu fika kwamba Habiba ni mfadhili wa ugaidi lakini amekubali kujiunga naye.Gosu Gosu,Mathew huyu wa sasa si Yule tuliyemfahamu.Hata siku moja Mathew Mulumbi hawezi akajiunga na magaidi ! akasema Ruby

“Yawezekana hii ni sababu kwa nini alikwambia usimfuatilie atakapoondoka” akasema Gosu Gosu

“Exactly.Alijua nitafahamu kuwa anashirikiana na Habiba Jawad”

“Mungu wangu ! Mathew kwa nini amefanya maamuzi haya ya kushirikiana na magaidi wa IS?

“Hata mimi najiuliza swali hilo sijapata jibu” akasema Ruby

“Habiba alitaka nini alipokupigia simu?

“Amenieleza kuwa mwanae anaitwa Nawal anakuja Tanzania akaniomba nimsaidie aweze kuingia salama”

“Mwanae anakuja Tanzania? Anakuja kufanya nini wakati huu wa machafuko?

“Hajanieleza anakuja kufanya nini ila amesema kuna jambo muhimu linalomleta hapa Tanzania. Akaniomba nimsaidie aweze kufika Dar es salaam.Naamini kinachomleta hapa ni mojawapo ya shughuli za IS kama ilivyo kwa Mathew”

“Anakuja lini?

“Kesho.Nitakwenda kumpokea katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro”

“Haya mambo yanachanganya sana” akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu huyu Mathew si Yule tumjuaye.Huyu ni Mathew tofauti kabisa.Hata siku moja Mathew Mulumbi hawezi kushirikiana na magaidi hivyo nimefanya maamuzi ya kutuma makomando wetu wakavamie nyumba ile mchana huu na wawachukue wote watakaowakuta akiwemo Mathew .Tutamshikilia sehemu salama kwa mahojiano ili atueleze kwa nini amefanya

maamuzi haya ya kushirikiana na magaidi?akasema Ruby.Gosu Gosu akafikiri kwa muda kisha akasema

“Hapana Ruby hatuwezi kufanya hivyo”

“Kwa nini Gosu Gosu?Mathew amebadilika na hatuwezi kumuacha akaendelea namna hii.Anashirikiana na magaidi na hata sasa kuna kitu wanapanga kukifanya hapa Dar es salaam siku ya leo ndiyo maana alituzuia tusivame ile nyumba hadi usiku wa leo.Kwa hiki anachokifanya Mathew

maisha yake tayari yapo hatarini na kama mtu wetu wa karibu ni jukumu letu kuhakikisha tunamsaidia.Yawezekana haoni hatari iliyoko mbele yake au anashirikiana nao kwa shinikizo.Tunatakiwa tufahamu kila kitu" akasema Ruby

"Ruby sikubaliani na wazo lako kwa sababu Mathew ni mtu anayejua nini anakifanya.Kama ameingia katika mashirikiano na magaidi basi ni kwa sababu maalum.Si mara moja Mathew

ameingia katika sehemu za hatari kwa ajili ya kufanikisha misheni muhimu.Naamini hata huku aliko sasa hajaenda kwa bahati mbaya,ana sababu maalum na kama unakumbuka jana amezungumza nasi na akatutahadharisha kwamba tutakachokisikia kuhusu yeye tusikiamini.Sasa nimeelewa kwa nini alitupa taarifa ile mapema kwani alijua tungeweza kufahamu mambo kama haya kuhusu yeye kushirikiana na magaidi.Alituandaa tusistuke tutakapogundua hilo na

alitupa maelekezo vile vile kwamba tusifanye chochote hadi usiku wa leo.Hii ina maana kwamba kuna misheni inaendelea na kama angekuwa hana nia njema asingefanya jitihada za kututafuta na kutupa taarifa muhimu.Ni yeye ambaye ametupa mwanga kuhusiana na vurugu hizi zinazoendelea na sasa tuna sehemu ya kuanzia.Hatua zozote za kwenda kinyume na maelekezo ya Mathew kinaweza kupelekea kwanza tukavuruga misheni ya Mathew na vile vile tunaweza

kujikuta tumevuruga kila kitu kuhusu misheni yetu” akasema Gosu Gosu

“Gosu Gosu !

“Hapana Ruby hatutafanya chochote tutafuata maelekezo ya Mathew.Ninamuamini Mathew sana na kama wewe umeanza kupoteza imani kwake mimi bado namuamini na nitaendelea kufuata maelekezo yake” akasema Gosu Gosu

“Papii,Mathew huyu si Yule ambaye tunamfahamu.Hata siku moja

Mathew Mulumbi tunayemfahamu hawezi akakubali kushirikiana na magaidi” akasema Ruby

“Ruby hakuna sababu yoyote ya kuvamia yumba wanayoishi Mathew na watu wa IS mchana huu.Operesheni itaendelea usiku kama tulivyopanga.Kitu kingine ambacho ninakiona cha msingi tumsubiri huyo mtoto wa Habiba Jawad anayekuja kesho anaweza akatueleza mambo mengi zaidi.Hatupaswi kwenda haraka haraka tutavuruga kila kitu.Kumbuka

tulikuwa tumekwama na hatukujua sehemu ya kuanzia lakini ni Mathew aliyekuja kutukwamua.Nakuomba Ruby tuwe na uvumilivu katika hili.Mathew anajua kwamba watu wake wa karibu lazima watafahamu kuwa anashirikiana na magaidi na wataumia hivyo alitutaka tusitetereke.Naomba tubaki hivyo” akasema Gosu Gosu na Ruby akabaki akimtazama

****

Licha ya kutokea kwa mauaji ya kiongozi mkuu wa waislamu Tanzania lakini jiji la Dar es salaam na viunga vyake halikuwa na vurugu ambazo zilitegemewa kutokea.Maelfu ya waumini wa dini ya kiislamu walihudhuria mazishi ya kiongozi wao yaliyofanyika mchana wa siku hiyo.Ulinzi ulikuwa mkali sana wakati wa mazishi hayo na viongozi waliokuwepo walitumia muda mwingi kuwaomba waumini wasilipize kisasi kwani kitendo hicho kingeongeza vurugu

zaidi na damu nyingi ingeendelea kumwagika.Walitumia muda mwingi zaidi kuhubiri uwepo wa amani kama njia ya kumuenzi kiongozi Yule aliyeuawa ambaye alipenda kuona amani inapatikana nchini.

Kiza kilianza kutanda angani bado jiji la Dar es salaam halikuwa na vurugu kama zilizokuwepo siku chache zilizopita.Saa moja na nusu geti la nyumba alimo Mathew Mulumbi na watu wa IS lilifunguliwa na gari mbili

zikaingia mojawapo likiwa ni gari la jeshi la Marekani.Kutoka katika gari lililokuwa mbele akashuka Assad Ismail na kusalimiana na Marwan.Wanajeshi wawili wakashuka kutoka katika lile gari la jeshi wakaongozana na Assad kuelekea ndani.

Mlango wa chumba cha Mathew Mulumbi ukagongwa akaenda kuufungua akakutana na Marwan ambaye alimtaka ajiandae kwani muda umefika.Mathew akatoka katika kile chumba akaelekea sebuleni akasalimiana na

Assad kisha wakaongozana kuelekea katika bohari lililokuwa likitumika kuunda bomu.Tayari bomu lilikuwa limekamilika.Assad akalikagua kisha akawapongeza wataalamu waliounda bomu lile halafu akaelekeza lipelekwe katika gari la jeshi.Ndani ya lile gari la jeshi kulikuwa na watoto wadogo sita wenye umri wa miaka mitano hadi nane.Gari lile likafunguliwa sehemu ya nyuma na bomu lile kubwa likawekwa vizuri.Wakati wataalamu wale wakiendelea na kuliweka

bomu katika gari Assad akamchukua Mathew wakarejea ndani.Mmoja wa wale wanajeshi akavua mavazi yake ya kijeshi na kumpa Mathew akavaa.

“Abu Zalawi sasa uko tayari kwa kazi uliyokuja kuifanya.Tumezungumza mengi mchana wa leo kuhusiana na kazi hii na nina imani hakutakuwa na usumbufu wowote.Vyovyote itakavyokuwa hakikisha bomu hilo linalipuka.Umenielewa Abu? Akauliza Assad

“Nimekuelewa Assad”

“Sawa.Basi kila kitu ni kama tulivyopanga.Nakutakia kila la heri” akasema Assad.Mathew akatoka mle ndani akiwa ameongozana na wale wanajeshi hadi katika gari lile akapewa maelekezo kadhaa na wale wanajeshi halafu akaingia garini akaliwasha na kuondoka

“Nawaonea huruma sana watoto hawa wadogo.Laiti ningekuwa na uwezo wa kuwasaidia ningefanya hivyo lakini hawa ndio watakaoniwezsha kuingia katika ubalozi wa

Marekani.Inauma sana lakini hakuna namna” akawaza Mathew akiendelea na safari ya kuelekea katika ubalozi wa Marekani.

****

Wakati Mathew Mulumbi akiwa njiani kuelekea ubalozi wa Marekani,katika makao makuu ya SNSA kikosi cha makomando kilikuwa kinajiandaa kwa ajili ya kwenda kuvamia nyumba wanamoishi watu wa IS waliyoelekezwa na

Mathew.Mchana kutwa walikuwa wameelekeza drone kubwa inayotumiwa na SNSA katika nyumba hiyo wakifuatilia kwa karibu kila kilichokuwa kinaendelea ndani ya nyumbe ile na kupanga mikakati namna watakavyoweza kuingia ndani.

Ndani ya jengo la SNSA kulikuwa na heka heka nyingi wakiwa wamejielekeza katika kuhakikisha operesheni ile inafanikiwa.

“Tusikilizane ndugu zangu” akasema Ruby aliyetoka kuagana na

makomando waliopanda helkopta kuelekea katika misheni yao.

“Toka asubuhi ya leo tulikuwa na zoezi la kuchunguza nyumba ambayo wanaishi watu wa IS na watu wale tunaowalenga Marwan na Assad tumewaona katika nyumba hiyo.Muda umefika na makomando wetu tayari wameondoka kuelekea huko.Ni jukumu letu kuhakikisha tunawasaidia kwa kila namna tuwezavyo.Operesheni hii ni muhimu mno na kwa namna

yoyote lazima iende kama ilivyopangwa hivyo kila mmoja ahakikishe kwa upande wake anafanya kila kinachotakiwa kuhakikisha makomando wetu wanafanikiwa” akasema Ruby na kutaka kazi ziendelee.

****

Mathew akiwa katika gari la jeshi la Marekani alikata kona ya kuelekea katika ubalozi wa Marekani.

“I must do this ! akawaza

Katika geti la kuingilia ubalozini hapo kulikuwa na

ulinzi wa wanajeshi wa Marekani.Gari lile alilokuwa analiendesha Mathew likasimamishwa na Mathew akawahi kuwaeleza kuwa ndani ya gari ana watoto ambao wamewaokoa katikati ya mapigano na akatumwa kuwakimbiza pale ubalozini kupata hifadhi ya muda kabla ya kupelekwa katika kambi maalum hapo kesho.Hakuna aliyetia shaka yoyote kuhusu gari lile wote walijua Mathew ni mwenzao.Geti likafunguliwa na gari likaingia ndani.

Mchana wa siku ile Mathew na akina Assad walitumia muda mrefu kujadili suala lile na kumpa Mathew maelekezo yote juu ya utekelezaji wa jambo lile.Mathew akaenda kuegesha gari mahala alikoelekezwa na kuwashusha wale watoto akawapeleka katika mahema yaliyokuwa yamewekwa nje ya ubalozi kwa ajili ya baadhi ya raia wa Marekani na wa nchi nyingine waliokwama Dar es salaam.Baada ya kuwakabidhi watoto wale Mathew akaelekea getini akaomba kutoka

akaeleza kuna watoto anawafuata ambao amewaona wakiwa njiani hawana msaada.Alielekezwa achukue gari lakini akadai kwamba hana haja ya gari anakwenda kwa miguu kwa sababu si mbali na pale ubalozini.Wanajeshi waliokuwa wanalinda getini hawakuwa na wasi wasi naye kwani waliamini kwa asilimia mia moja ni mwenzao hivyo wakamuacha akatoka.Akiwa na bunduki yake mkononi alikimbia akifuata barabara.Katika jengo moja la

mgahawa ambao ulikuwa umefungwa kuliegeshwa gari jeupe.Mathew alipolikaribia taa zikawashwa na kuzimwa ikiwa ni ishara akaliendea mlango ukafunguliwa akaingia ndani ambamo alimkuta Assad Ismail akiwa na watu wengine wanne.

“Nimekamilisha kazi” akasema Mathew

“Hakuna tatizo lolote? Hawakutia shaka?akauliza Assad

“Hakuna tatizo lolote.Waliamini mimi ni mwenzao” akajibu Mathew

“Safi sana” akasema Assad na kumpatia Mathew kifaa Fulani akakiwasha kikaanza kuanzika namba haraka haraka na kufikia sifuri.

“Bonyeza kitufe hicho chekundu ili kazi yako iwe imekamilika” akasema Assad na Mathew bila kupepesa macho akabonyeza kile kitufe na mlipuko mkubwa ukatokea na hadi mahala pale walipokuwa wakahisi mtikisiko kutokana na bomu lile lililolipuka kuwa zito.Assad akampa Mathew mkono

“Hongera Abu Zalawi umekamilisha kazi yako” akasema na kisha gari likawashwa wakaondoka.Walipishana na magari ya jeshi na zimamoto yakielekea mahala ulikotokea mlipuko.Assad alikuwa anaelekeza njia za kupita na kisha wakafika katika jengo la hoteli ambayo ilikuwa katika hatua za mwisho za ujenzi.Geti la hoteli ile kubwa likafunguliwa gari la akina Assad likaingia ndani na kuelekea moja kwa moja

mahala ilikokuwa imeegeshwa helkopta ya jeshi la Marekani.

“Abu Zalawi kazi yako hapa Tanzania imekamilika na sasa unaelekea Nairobi Kenya.Utaondoka na helkopta hii hadi nchini Kenya na mambo yataendelea kama nilivyokupa maelekezo.Tafadhali usiende kinyume na maelekezo niliyokupa” akasema Assad

“Ahsante Assad kwa ushirikiano na msaada mkubwa ulionisaidia katika kukamilisha kazi yangu” akasema Mathew na kumpa

mkono Assad wakaagana akaingia katika helkopta mlango ukafungwa na helkopta ikawashwa.Assad alisimama pembeni ya gari lake hadi helkopta ile ilipopaa na kuondoka.

****

Helkopta maalum ya operesheni za usiku ya makomando wa SNSA iliyotengenezwa kwa teknolojia ya hali ya juu ya kutokutoa sauti,ilifika usawa wa nyumba ile walimokuwamo watu wa

IS.Bado sehemu kubwa ya jiji la Dar es salaam ilikuwa gizani.

Makomando nane waliokuwa wamevaa miwani ya kuwawezesha kuona gizani wakashuka kwa miavuli huku kila mmoja akitua katika sehemu aliyoelekezwa kwani walikwisha fanya mazoezi mchana wa siku ile.Walinzi waliokuwa zamu usiku ule wakilinda nyumba ile hawakuweza kuwaona makomando wakishuka kutokana na giza na hii iliwasaidia makomando wale

waliokuwa na miwani ya kuonea gizani kuwaona na kuwamaliza kwa bunduki zao nzito zilizofungwa viwambo vya kuzuia sauti.Makomando wote walitua salama na hakukuwa na mtu hata mmoja aliyekuwa nje ya ile nyumba alibaki hai.Walimiliki eneo lote la nje la ile nyumba.Baada ya kujipanga vizuri makomando wanne wakaenda katika mlango wa mbele wa kuingilia katika ile nyumba na mmoja akachungulia ndani akawaona watu wanne wakiwa sebuleni wakizungumza.Hawakuwa na

habari kama wenzao waliokuwa nje wamekwisha uawa wote.Komando Yule akawapa ishara wenzake kwamba kuna watu wanne kisha wenzake wakasogelea mlango,kiongozi wao akakinyonga kitasa cha mlango ukafunguka wakajitoma ndani.Wale jamaa waliokuwa wamekaa katika zuria walipigwa na butwaa wakakosa la kufanya baada ya kujikuta wamezingirwa na wanajeshi wenye silaha nzito.Mmoja wa wale jamaa akageuka haraka ili aweze

kuchukua bastora yake lakini mkono wake haukufika katika bastora kwani kichwa chake kilifumuliwa kwa risasi toka katika bunduki nzito ya mmoja wa makomando.

“Yuko wapi Marwan Hossam? Akauliza kiongozi wa makomando.Wale jamaa hawakujibu kitu.

“Nawauliza tena yuko wapi Marwan?

Bado wale jamaa waliendelea kuwa kimya.Akaamuru wafungwe pingu.Wakati komando mmoja akijiandaa kuwafunga pingu

mmoja wa wale magaidi akainuka na kupiga ukelele huku akitaka kumvaa mmoja wa makomando lakini hakufanikiwa kitendo alichokusudia baada ya kunyeshewa mvua ya risasi na mara mlango mmoja ukafunguliwa.

“Omar kuna nin.....” akauliza jamaa aliyekuwa kifua wazi na kaptura akionekana kutoka kulala

“Omar ! akaita Yule jamaa huku akielekea sebuleni

“Yarkud ! Yarkud ! akasema mmoja wa wale

magaidi kwa lugha ya kiarabu akimtaka Yule jamaa akimbie.Yule jamaa akageuka na kutoka mbio akipita jikoni akaufungua mlango wa nyuma ili aweze kutoka lakini akapigwa teke zito akaanguka chini na kabla hajafanya chochote akajikuta amezungukwa na makomando wanne wakamuinua na kumfunga pingu.Walipommulika wakagundua kwamba Yule alikuwa ni Marwan Hossam.

“Tumempata Marwan ! SNSA ofisi kuu wakajulishwa

“SNSA tumempata Marwan” akasema Yule komando

“Hakikisheni mnawachukua wote mtakaowakuta hapo” akaelekeza Ruby.Marwan alipelekwa sebuleni akaunganishwa na wale wenzake wawili.Nyumba ile ikapekuliwa hakukuwa na mtu mwingine na kiongozi wa wale makomando akaelekeza makomando wake wakavamie yale majengo mengine mawili.Makomando wawili wakabaki wakiwalinda wale

magaidi na wengine wakaenda kuvamia katika yale majengo mawili.Watu waliokuwa ndani ya majengo yale mawili walikuwa wamejilaza wakipumzika hawakuwa na habari kama wangevamiwa.Walistukia wakiwa wamezingirwa na makomando na hawakupata nafasi ya kujitetea.Wote wakajikuta wakitiwa nguvuni.Upekuzi ukafanyika katika nyumba zile mbili na ikagundulika kwamba kulitengenezwa bomu kwani kulikutwa na baadhi ya vifaa

vya kutengenezea mabomu.Chumba cha Marwan Hossam kikapekuliwa na vitu kadhaa vikachukuliwa ikiwemo simu yake ya mkononi.

Baada ya kukamilisha kazi waliyotumwa walitoa taarifa ofisi kuu SNSA na helkopta ile waliyokwenda nayo ikashuka chini na kamba ikashushwa.Marwan akafungwa ile kamba maalum kisha akiwa ameshikwa na komando mmoja kamba ile ikapanda taratibu na Marwan akaingizwa katika helkopta

ikaondoka.Makomando wengine walibaki wakiwalinda wale magaidi wapatao tisa.

****

Helkopta ya SNSA ilitua katika sehemu yake ikitokea katika operesheni maalum ya makomando waliovamia nyumba ya magaidi wa IS.Mlango wa helkopta ukafunguliwa akashuka komando mmoja kisha akamshusha Marwan Hossam.Gosu Gosu akasogea na kumchukua Marwan

akaelekea ndani na helkopta ile ikaondoka kwenda kuwachukua watu wengine.Gosu Gosu akamchukua Marwan na kumpeleka katika chumba maalum cha mahojiano kilichopo mita kadhaa chini ya jengo lile akamfungia katika chumba chenye baridi kali kisha akamfuata Ruby aliyekuwa katika ofisi yake

“Ruby tayari tumempata Marwan hakuna haja ya kuendelea kusubiri .Tukaanze kumuhoji mara moja ili ikiwezekana usiku huu huu

tumpate pia Assad kwani hana taarifa kama wenzake wamevamiwa.Tukichelewa hadi kesho atagundua kilichotokea na atajificha itakuwa kazi ngumu kwetu kumpata” akasema Gosu Gosu kisha Ruby akaelekeza Marwan atolewe katika chumba kile cha baridi apelekwe katika chumba cha mahojiano halafu wakashuka chini

“Nina muda mrefu sijawahoji watu kama hawa,ana bahati mbaya sna Marwan ameingia katika anga

zangu.Leo atanena lugha zote anazozifahamu” akawaza Gosu Gosu wakiwa ndani ya lifti wakishuka chini.

MPENZI MSOMAJI MATHEW AMELIPUA UBALOZI WA MAREKANI NCHINI TANZANIA IKIWA NI MWANZO WA MISHENI NZITO YA KUELEKEA IRAN,JE MISHENI YAKE ITAFANIKIWA?

GOSU GOSU NA RUBY WAMEANZA KUUSAKA MTANDAO WA CHANZO CHA VURUGU TANZANIA JE

WATAFANIKIWA
KUWAPATA WOTE
WANAOHUSIKA?
NAWAL ATAFANIKIWA
MISHENI YAKE YA KUZUIA
KIRUSI KISISAMBAE
TANZANIA?
USIKOSE SEHEMU IJAYO..